Jumamosi Julai 13, 2019 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

# Nipashe

ISSN 0856 • Na. 0579969
www.ippmedia.com
MWANGA WA JAMII
www.twitter.com/nipashetz
www.facebook.com/nipashetz
www.instagram.com/theguardian_newspaper
LIKE & FOLLOW US






## Waziri ashtuka mil. 60/- kununua dawa ya mchwa

UKURASA 3



# Upimaji wa afya waibua mazito

• **Ni** uliofanywa na JKCI Sabasaba, asilimia 40 wagundulika na shinikizo la damu, 20 kisukari, wengine uzito mkubwa... *Uk.2*



Waziri Mkuu Kassim Majaliwa akimkabidhi zawadi ya picha ya Mlima Kilimanjaro, Naibu Waziri Mkuu wa Vietnam, Trinh Dinh Dung, baada ya mazungumzo yao ofisini kwake Magogoni jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: OWM**

## Wanafunzi 10 bora sayansi wapata ufadhili masomo

UK. 2


## YALIYOMO

**UKURASA WA 3**

**UAMUZI KESI KINA MALINZI JULAI 23**

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Kisutu, jijini Dar es Salaam imesema itatoa uamuzi...

**UKURASA WA 4**

**MAREKANI YAJITOSA MIMBA ZA UTOTONI**

MAREKANI imesema itaendelea kushirikiana na Tanzania katika kutatua changamoto...

**UKURASA WA 7**

**KIGOGO CCM KORTINI MADAI KUGHUSHI CHETI**

MWENYEKITI wa zamani wa Umoja wa Wanawake wa CCM (UWT) Wilaya ya Ilala...


## Kikongwe kortini tuhuma ubakaji

UKURASA 3

**MICHEZO** **YANGA HAITAKI MCHEZO AFRIKA** UK.32 **MAONI, KATUNI** UK.6

# Upimaji afya Sabasaba waibua mazito

**Na Romana Mallya**

ASILIMIA 40 ya watu waliofanyiwa vipimo na Taasisi ya Moyo Jakaya Kikwete (JKCI) kwenye Maonyesho ya 43 ya Biashara ya Kimataifa ya Dar es Salaam, wamekutwa na shinikizo la juu la damu huku asilimia 20 wakiwa na sukari kwenye damu.

Msemaji wa JCKI, Anna Nkinda, aliyasema hayo jana jijini Dar es Salaam na kuongeza kuwa asilimia 60 ya watu waliofanyiwa vipimo walikutwa na uzito mkubwa. Nkinda alisema taasisi hiyo imetoa rufaa ya moja kwa moja kwa watu 73 wakiwemo watoto wawili ambao baada ya kufanyiwa vipimo walikutwa na matatizo ya moyo yanayohitaji kufanyiwa uchunguzi wa kina na matibabu ya kibingwa.

Alisema wananchi 1,776 wamepata huduma za ushauri, vipimo na tiba za magonjwa ya moyo bila malipo zinazotolewa na JKCI kwenye maonyesho hayo yanayofanyika katika Viwanja vya Maonyesho ya Biashara vya Mwalimu Julius Kambarage Nyerere, barabara ya Kilwa, Dar es Salaam.

"Wananchi hawa waliotembelea banda la taasisi hii kwa ajili ya kupima afya zao. Walifanyiwa vipimo vya magonjwa ya moyo na 448 walifanyiwa kipimo cha kuangalia moyo unavyofanya kazi (Echocardiography) na 1,097 walifanyiwa kipimo cha kuangalia umeme wa moyo unavyofanya kazi (Electrocardiogram - ECG)," alisema.

Mkazi wa Shekilango, Rehema Abdallah, aliipongeza taasisi hiyo kwa kutoa huduma ya matibabu ya moyo kwa wananchi bila malipo pamoja na kuwapa kipaumbele wazee waliojitokeza kwenda kupima afya zao.

"Nawashukuru wafanyakazi wa JKCI wanaotoa huduma katika mayonesho haya. Kutokana na umri wangu wamenipa kipaumbele cha kufanyiwa vipimo kwa haraka. Nimekutwa na tatizo la shinikizo la juu la damu na tayari nimepatiwa dawa kwa ajili ya matibabu," alisema.

Maye mkazi wa Mwananyamala, Hatibu Rashid, aliishukuru taasisi hiyo kwa kuwafikiria wananchi wenye uwezo wa chini kupata nafasi ya kufanyiwa vipimo vya magonjwa ya moyo.

"Zamani vipimo kama hivi vilikuwa vinafanyika nje ya nchi tena kwa watu wenye fedha. Lakini leo hii vipimo hivi vinafanyika hapa nchini na tunafanyiwa wananchi wa kawaida kabisa. Ninaishukuru sana serikali kwa kuimarisha huduma ya matibabu ya moyo," alisema.



Kamishna Mhifadhi wa Misitu, Prof. Dos Santos Silayo akikagua baadhi ya maofisa wa Jeshi Usu la Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania, baada ya kuwasili makao makuu ya Ofisi za Wakala huo, katika Jengo la Mpingo, jijini Dar es Salaam jana, kwa mara ya kwanza tokea aapishwe na Rais Dk. John Magufuli kushika wadhifa huo, Julai 9, mwaka huu. **PICHA: TFS**

# Wanafunzi 10 bora sayansi wapata ufadhili chuo kikuu

**Na Mary Geofrey**

CHUO Kikuu cha Mtakatifu Joseph, (SJUIT), kimejitolea kuwafadhili ada ya masomo wanafunzi 10 waliofaulu masomo ya sayansi katika matokeo ya kidato cha sita yaliyotangazwa juzi na Baraza la Mitihani ya Taifa (Necta).

Ufadhili huo ni kwa masomo ya shahada ya kwanza ya sayansi katika uhandisi, tiba na ualimu. Katika chuo hicho, shahada za kwanza za udaktari na mambo ya tiba kwa miaka mitano wa wakati uhandisi na ualimu ni miaka minne.

Kaimu Makamu Mkuu wa Chuo hicho, Prof. Innocent Ngalinda, alitangaza ufadhili huo jana alipozungumza na Nipashe kuwa wameshawishika kufanya hivyo kutokana na juhudi zilizofanywa na wanafunzi hadi kushika nafasi 10 bora kitaifa kwenye masomo ya fani hiyo.

"Tumeamua kutoa ufadhili wa masomo katika chuo chetu kwa miaka minne hadi mitano ya masomo kwa wanafunzi 10 bora wa masomo ya Sayansi. Tutawagharamia ada kwa asilimia 100 isipokuwa chakula na malazi, mahitaji ambayo pia wanaweza kuombea mkopo," alisema Prof. Ngalinda.

Kadhalika, alisema wameamua kutoa ufadhili huo kwa sababu mwasisi wa chuo hicho, Mtakatifu Joseph alikuwa seremala kazi ambayo ina mlengo wa uhandisi na mambo ya sayansi.

Pamoja na ufadhili huo, alisema wanafunzi hao wataendelea kupimwa kwa viwango vya juu vya ufaulu ili waendelee kufanya vizuri katika kipindi chote cha masomo yao katika chuo hicho.

"Chuo kitaendelea kuwapima wanafunzi hawa kila mwaka ili waendelee kufanya vizuri. Tunataka wasibweteke, wahamasike kuendelea kufanya vizuri na endapo watafanya vibaya tutapunguza kumlipia ada ya masomo katika miaka inayofuata," alisema.

Wanafunzi 10 walioongoza katika masomo ya sayansi katika matokeo ya kidato cha sita mwaka huu na shule walizotoka ni Faith Matee (St. Mary's Mzinde Juu, Tanga), Herman Kamugisha (Kisimiri, Arusha), Levina Chami (St. Coreti ya Kilimanjaro), Benius Eustace (Mzumbe ya Morogoro) na Augustino Omari (Ilboru ya Arusha).

Wengine ni Satrumin Shirima (Temeke, Dar es Salaam), Khalid Abdalla, (Feza Boys, Dar es Salaam), Assad Msangi (Feza Boys, Dar es Salaam), Peter Riima (Kibaha, Pwani) na Augustine Kamba (Feza Boys)

Katika matokeo yaliyotangazwa jana na Katibu Mtendaji Necta, Dk. Charles Enock Msonde, yalionyesha ufaulu umepanda kidogo kwa asilimia 0.74 ikilinganishwa na mwaka 2018 ambao ulikuwa 97.58 huku wasichana waking'ara zaidi katika masomo ya sayansi kuliko wavulana.

Aidha, ubora wa ufaulu huo umezidi kuimarika kwa kuwa watahiniwa waliofaulu vizuri katika daraja la kwanza, pili na tatu wameongezeka kwa asilimia 1.09 kutoka asilimia 95.52 mwaka 2018 na kuwa na asilimia 96.61 mwaka huu.

# Jafo ataja siri shule za serikali kung'ara

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi), Selemani Jafo, ametaja siri ya shule za serikali kufanya vizuri katika matokeo ya kidato cha sita mwaka huu.

Akizungumza jana na waandishi wa habari ofisini kwake jijini hapa, Jafo alisema shule hizo zimefanya vizuri ikilinganishwa na awali kutokana na uwekezaji uliofanywa kwenye sekta ya elimu.

"Hapo awali ulikuwa ukiangalia shule 100 bora, za serikali zilikuwa za kutafuta. Siri kubwa ya mafanikio ya shule za serikali kufanya mapinduzi makubwa ni uwekezaji katika elimu," alisema.

Alisema serikali imewekeza katika miundombinu ya elimu ambayo kwa sasa ni rafiki, uwapo wa vifaa vya maabara na mabilioni ya shilingi yameingizwa kwenye ununuzi wa vifaa hivyo.

"Tumewekeza pia katika rasilimali watu, tumeongeza idadi ya walimu. Leo hii shule zina walimu 30 hadi 40 wakati zamani zilikuwa zina walimu watano hadi saba. Kuna shule hadi walimu wengine wanabadilishana vipindi. Tulikuwa na changamoto ya walimu wa sayansi ambayo tunaendelea kuwekeza huko na wanafunzi wameanza kufanya vizuri," alisema.

Waziri Jafo alisema shule za kata hali yake ya awali haiwezi kulingana na sasa kwa kuwa kuna walimu wa kutosha huku akiwataka wazazi kuwaacha watoto kusoma kwenye shule wanazochaguliwa.

"Usione mtoto amepelekwa shule ya kata ukadharau. Kumbuka shule hii inaweza kupiga bao, leo hii tuangalie shule ya Lukole matokeo yake linganisha na Jangwani au Azania. Tusihamishe watoto tuwaache wasome, serikali imeweka uwekezaji mkubwa. Niwatoe hofu Watanzania, tunaenda sasa sehemu nzuri na salama," alisema.

Alifafanua kuwa ufaulu umeendelea kuimarika kutokana na kupanda kutoka asilimia 98.2 hadi 98.93 na kwamba katika shule 10 bora za kwanza, nne ni za serikali.

"Hii ni faraja kubwa sana kwa mwaka wa pili mfululizo tumeona Kibaha ambayo mwaka jana ilikuwa ya kwanza. Shule nyingine Kisimiri ambayo ni shule ya kata kihistoria sasa imekuwa ya kwanza," alisema.

Waziri huyo alitaja shule hizo nne zilizoingia 10 bora kuwa ni Kisimiri, Mwandet, Tabora Wavulana na Kibaha.

INAENDELEA UK. 8

# HABARI KITAIFA



Lundo la takataka zinazozalishwa na Soko la Tandale katika Manispaa ya Kinondoni, zikiwa zimetelekezwa barabarani bila ya kuzolewa, jijini Dar es Salaam jana, kitendo ambacho kinaweza kusababisha magonjwa na milipuko kama vile kipindupindu na usumbufu kwa vyombo vya moto vinavyotumia barabara hiyo. **PICHA: JOHN BADI**

## Waziri ashtushwa mil. 60/- kununua dawa ya mchwa

**Na Mwandishi Wetu,** MOROGORO

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Selemani Jafo, ameshtushwa na matumizi ya Sh. milioni 60 kununua dawa ya mchwa katika ujenzi wa hospitali ya wilaya ya Morogoro, eneo la Mvuha.

Kutokana na kutilia shaka matumizi hayo, Jafo amesema atatuma timu maalum kuchunguza matumizi hayo ambayo amedai kuwa ni makubwa huku yakiwa hajawekwa kwenye taarifa ya matumizi za fedha za ujenzi wa hospitali hiyo.

Jafo alionyesha shaka hiyo katika ziara yake ya kukagua ujenzi wa hospitali ya wilaya ya Morogoro baada ya kupokea taarifa ya ujenzi yenye mchanganuo wa matumizi ya fedha zaidi ya Sh. bilioni moja huku ununuzi wa dawa hiyo ukiwa hauonekani.

"Hivi kweli dawa ya kudhibiti mchwa iliwekwa kwenye majengo haya? Kama kazi ilifanyika kwa gharama ya Sh. milioni 60 unayosema kwa nini matumizi ya fedha hizo hayajawekwa kwenye taarifa?" alihoji.

"Bei ya ununuzi wa dawa hiyo si halisi na sijui kama mlijaribu kujilinganisha na wenzenu wa halmashauri zingine ili mfahamu kuwa walitumia kiasi gani kwenye ununuzi wa dawa kama hiyo au ninyi mmenunua dawa ya aina gani ambayo imegharimu kiasi hiki kikubwa cha fedha," aliongeza.

Kutokana na hali hiyo, alisema ana wasiwasi na matumizi ya fedha hizo za ujenzi kwa ujumla na kwamba atatuma timu maalumu kwa ajili ya kuchunguza matumizi mabaya ya fedha za mradi wa ujenzi wa hospitali.

"Kwa kipindi kirefu Halmashauri ya Wilaya ya Morogoro imekuwa na matumizi yasiyoridhisha ya fedha za miradi mbalimbali ya maendeleo na hali hii inaonyesha dhahiri kuwa kuna changamoto za kiungozi. Hapa kuna tatizo kubwa na lazima tulipatie ufumbuzi," alisema.

Jafo alionyesha kushangazwa na kushindwa kwao kutekeleza miradi kwa wakati kuanzia ujenzi wa jengo la halmashauri Sh. milioni 500 ambazo hazijulikani zilipo na mpaka sasa na jengo halijajengwa.

"Sasa mnataka tena tabia hiyo muilete kwenye mradi wa hospitali? Safari hii mtamaliza ujenzi huu haijalishi fedha mnazo au mmezitumia. Ni lazima mkamilishe ujenzi, mpaka sasa mmekwishatumia Sh. bilioni moja kujenga majengo haya ambayo hayaridhishi na hamjafikia hata kwenye hatua ya kupaua huku mnaniambia mmebakiwa na Sh. milioni 400, sitaki kusikia,"alisema.

Jafo alisema hataki kusikia

INAENDELEA UK. 8

## Uamuzi kesi ya kina Malinzi, Julai 23

**Na Hellen Mwango**

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Kisutu, jijini Dar es Salaam imesema itatoa uamuzi wa kesi ya kutakatisha Dola za Marekani 173,335 inayomkabili Rais wa zamani wa Shirikisho la Mpira wa Miguu Tanzania (TFF), Jamali Malinzi na wenzake kama wana kesi ya kujibu au la Julai 23, mwaka huu.

Uamuzi huo ulitolewa na mahakama hiyo iliyoketi chini ya Hakimu Mkazi, Maira Kasonde baada ya upande wa Jamhuri kufunga ushahidi wake.

Mwendesha Mashtaka wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru), Leonard Swai, alidai kuwa baada ya kuita mashahidi 15 wa Jamhuri hawana nia ya kuita shahidi mwingine.

Alidai kuwa anaiachia mahakama iamue kama washtakiwa wana kesi ya kujibu au la.

Kabla ya uamuzi huo, hakimu aliwahoji mawakili wa pande zote mbili kama wana nia ya kuwasilisha hoja za kama washtakiwa wana kesi ya kujibu au la.

Jopo la utetezi likiongozwa na Wakili Richard Rweyongeza na wenzake kwa nyakati tofauti lilidai kuwa wanaiachia mahakama itoe uamuzi dhidi ya washtakiwa kama wana kesi ya kujibu au la.

Mbali na Malinzi, washtakiwa wengine ni, Katibu Mkuu wa zamani wa shirikisho Selestine Mwesigwa, Mhasibu wa TFF, Mwanga wengine ni, Meneja wa Ofisi TFF, Miriam Zayumba na Karani wa TFF, Flora Rauya, ambao kwa pamoja wanakabiliwa na mashtaka 30 katika kesi ya jinai namba 213 ya mwaka 2017.

Ilidaiwa kuwa washtakiwa walikula njama, kughushi, kujipatia fedha kwa njia ya udanganyifu na kutakatisha Dola za Marekani 173,335.

Malinzi, Mwesigwa na Nsiande wanaendelea kusota rumande kwa sababu wanakabiliwa na mashitaka ya utakatishaji fedha ambayo hayana dhamana kwa mujibu wa sheria.

## Kikongwe kortini tuhuma kumbaka mgonjwa wa akili

**Na Gurian Adolf,** MPANDA

MKAZI wa Kijiji cha Kanoge, Makazi ya Wakimbizi ya Katumba, Mpanda mkoani Katavi, Chubwa Venance, amefikishwa na kusomewa mashtaka katika Mahakama ya Wilaya ya Mpanda kwa tuhuma za kumbaka mwanamke mgonjwa wa akili.

Venance (90) alifikishwa mahakamani hapo jana na kusomewa mashitaka na mwendesha mashtaka kutoka Ofisi ya Mwendesha Mashtaka Mkoa wa Katavi, Hongera Malifimbo, mbele ya Hakimu Mkazi Mfawidhi Gasper Luoga.

Mtuhumiwa huyo alidaiwa kutenda kosa hilo Julai 2, mwaka huu, majira ya mchana katika kijiji cha Kanoge Makazi ya Wakimbizi ya Katumba wilayani Mpanda.

Mwendesha mashtaka huyo aliiambia mahakama kuwa siku ya tukio mtuhumiwa alikutwa akiwa anambaka mwanamke mwenye matatizo ya akili ambaye ni mkazi wa kijiji hicho (jina linahifadhiwa).

Alidai kuwa mtuhumiwa alikamatwa na wanafunzi waliokuwa wakitoka shuleni waliokuwa wanapita jirani na nyumba ambayo ilikuwa pagala, ndipo waliposikia mwanamke akiwa anapiga kelele za kuomba msaada.

Malifimbo aliendelea kudai kuwa baada ya wanafunzi hao kusikia kelele hizo walisogea kwenye eneo hilo walipoingia ndani ya pagala hilo ambalo lilikuwa haliishi mtu, walichungulia na kumwona babu huyo akiwa amemlalia kwa juu mwanamke huyo.

Baada ya kuona tukio hilo, wanafunzi hao wanadaiwa walikimbia na kwenda kutoa taarifa kwa watu kijijini na majirani wa eneo hilo walifika kwenye na kuingia ndani ya pagala na walimkuta babu huyo akiwa bado yuko juu akiwa amemlalia mwanamke huyo.

Mshitakiwa baada ya kusomewa mashtaka hayo, alikana kumbaka mwanamke huyo.

Hata hivyo, baada ya kusomewa mashtaka na kukana, hakimu alisema dhamana kwa mtuhumiwa iko wazi kwa masharti ya kudhaminiwa na mtu mmoja mwenye kuaminika kwa dhamana ya Sh. milioni moja.

Mtuhumiwa alishindwa kutimiza masharti ya dhamana kwa kile alichodai kuwa watoto wake anawategemea wako mkoani Kigoma kwa sasa, hivyo kupelekwa katika gereza la mahabusu la Mpanda mjini hadi Julai 22, kesi itakapoanza kusikilizwa kwa hatua za awali baada ya kukamilika kwa upelelezi.


## TANZIA



*Dr. Peter Matthew Kiangi*

Mama Helen Kiangi, pamoja na watoto wake Aida, Kiangi na Teresia, wanasikitika kutangaza kifo cha mpendwa wao Dr. Peter Matthew Kiangi kilichotokea Jumatano, tarehe 10 Julai 2019, katika hospitali ya Bombo, Tanga.

Habari ziwafikie familia ya Kiangi Kaluse pamoja na ndugu na jamaa wote wanaohusika na msiba huu. Msiba upo nyumbani kwa marehemu, Raskazone nyuma ya uwanja wa michezo wa shule ya secondari ya Popatlal.

Misa ya mazishi itafanyika Jumatatu tarehe 15 Julai nyumbani kwa marehemu, saa 8 mchana, na kufuatiwa na mazishi kwenye makaburi ya Bombo.

**Daima Tutakukumbuka.**

215322202

# Marekani yajitosa mimba za utotoni

**Na George Tarimo,** IRINGA

MAREKANI imesema itaendelea kushirikiana na Tanzania katika kutatua changamoto mbalimbali za wananchi ikiwamo kupunguza mimba kwa wasichana walioko shuleni kwa kusaidia ujenzi wa mabweni.

Kaimu Balozi wa Marekani nchini, Dk. Inmi Patterson, alisema hayo juzi kwenye ziara yake ya kukagua ujenzi wa mradi wa maji katika kijiji cha Mgama wilayani Iringa uliojengwa kwa msaada wa Marekani kupitia shirika lake la misaada ya maendeleo (Usaid) kwa zaidi ya Sh. milioni 260 kutatua changamoto ya huduma hiyo katika kijiji hicho.

"Tuko pamoja kujenga ustawi wa Tanzania lakini bila maji hakutakuwa na ustawi wa Tanzania. Hakutakuwa na nchi ya viwanda, hivyo tuko pamoja kufanya kazi, mimi binafsi ninafanya kazi kila siku kadri ya uwezo wangu kuboresha maisha ya Watanzania wa kawaida," alisema Dk. Patterson.

Awali, wakieleza changamoto za kijiji hicho, baadhi ya kinamama, akiwamo Bertha Ronjino, walisema pamoja na kupata mradi huo ambao umetatua changamoto waliyokuwa nayo, pia wana tatizo la mimba kwa wanafunzi wa kike.

Ronjino alisema kijiji hicho kina Shule ya Sekondari Mgama ambayo wanafunzi wake huwa wanapata mimba kutokana na kukosekana kwa bweni hasa kipindi cha mavuno ya nyanya.

Kaimu balozi huyo, baada ya kusikia changamoto ya mimba, alionyesha kusononeshwa na jambo hilo na kusema atawasiliana na serikali ya Marekani kuona jinsi ya kusaidia suala hilo.

"Mimi ninathamini sana watoto wa kike kwa sababu mimi ni mama wa watoto watatu wote wa kike, hivyo mkimuelimisha watoto wa kike mmeielimisha jamii," alisema.

Mradi wa maji wa mserereko wa Mto Kitamba unaozalisha lita sita kwa sekunde, umejengwa na shirika lisilo la kiserikali la Waridi kwa ufadhili wa Usaid ukiwa na lengo la kuhudumia zaidi ya wananchi 5,000 wa kijiji cha Mgama na vitongoji vyake.

Awali, wananchi wa kijiji hicho walikuwa wakitembea umbali mrefu kutafuta maji kutokana na tangi ambalo limejengwa kwa mbao kwa zaidi ya miaka 40 iliyopita kupoteza maji mengi.

Baada ya shirika hilo kujenga tangi lingine jipya, sasa wananchi hao wataondokana na adha ya kutembea kutafuta maji huku wengi wao wakisema upatikanaji wa tangi hilo utawasaidia wananchi kufanya shughuli zingine za maendeleo.




Kamanda wa Polisi Mkoa wa Pwani, ACP Wankyo Nyigesa, akionyesha vitu mbalimbali zikiwemo silaha, vilivyokamatwa baada ya majambazi kuuawa katika ma jibizano ya risasi katika eneo Kwala, wilaya ya kipolisi Mlandizi , mkoani humo jana. **PICHA: HISANI YA POLISI PWANI**

# Kanyasu awaonya wachimba madini kuhusu misitu

**Na Mwandishi Wetu,** GEITA

NAIBU Waziri wa Maliasili na Utalii, Constantine Kanyasu, amesema Tanzania kwa mwaka mmoja inateketeza takribani hekta 400,000 za misitu na kwamba endapo hali itaachwa hivyo, misitu iliyopo nchini itakwisha baada ya miaka 12.

Kutokana na hali hiyo, Kanyasu amesema wizara yake itaendelea kulinda misitu hiyo kwa nguvu zote ili kuinusuru. Kanyasu aliyasema hayo juzi mkoani hapa alipokuwa akizungumza na wachimbaji wadogo wa madini kwenye mkutano uliolenga kutoa elimu kwa wachimbaji hao kuhusu umuhimu wa kurasimisha mali. Alisema shughuli za uchimbaji madini zimekuwa zikichangia kwa kiasi kikubwa katika uteketezaji wa misitu hiyo na kwamba wachimbaji wengi wamekuwa watu wa kuhama hama na kila mahali wanapohisi kuna madini wamekuwa wakifyeka misitu bila kujali athari zake.

Naibu waziri aliongeza kuwa kwa vile wachimbaji hao wamekuwa wakifyeka misitu hiyo katika maeneo makubwa hata baada ya kumaliza uchimbaji huo, hushindwa kupanda miti mingine.

Aliwaeleza kuwa madhara yake ni makubwa na kama hali hiyo itaendelea kwa vile mara baada ya misitu hiyo kuisha, mvua hazitanyesha na hali ya maisha itakuwa ngumu. Katika hatua nyingine, Kanyasu aliwataka wananchi wanaokata miti iwe yao walioyaipanda, uwe mwembe au mti wa aina yoyote, wafuate taratibu za kupata kibali kwa maofisa misitu au wenyeviti wa maeneo husika. Alisema kwa wale wanaokata miti bila kupata kibali kwa mamlaka husika, serikali haitasita kuwachukulia hatua za kisheria.

## Wafungwa 648 waachiwa kwa Parole

**Na Mwandishi Wetu**

ZAIDI ya wafungwa 640 wameachiwa kupitia mpango wa Parole ndani ya miaka mitatu na hadi sasa hakuna mfungwa aliyevunja masharti na kurudishwa gerezani.

Mwenyekiti wa Bodi ya Taifa ya Parole, Augustine Mrema, alisema hayo jana katika Kikao cha 41 cha Bodi hiyo kilichofanyika katika Ukumbi wa Maofisa Magereza Ukonga, Dare es Salaam.

"Jumla ya wafungwa 666 wamejadiliwa na Bodi ya Taifa ya Parole katika vikao vyake saba vilivyofanyika na kupendekeza kwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi. wafungwa 648 wamenufaika na mpango huo na wengine 18 hawakupendekezwa kutokana na sababu mbalimbali," alisema Mrema.

Alisema utendaji wa bodi yake kwa miaka mitatu, umechangia kuimarika kwa hali ya utulivu na usalama ndani ya magereza kwa wafungwa kwa kuwa wamekuwa na matumaini makubwa ya kuingizwa kwenye mpango huo sambamba na kupokea programu za urekebishaji katika magereza mbalimbali nchini.

Mafanikio mengine, alisema ni wafungwa walioachiwa katika mpango huo, wameshiriki na wanaendelea kushiriki vyema katika shughuli za maendeleo katika jamii zao ikiwamo kuziangalia na kuzihudumia familia zao, hivyo kuipunguzia serikali gharama za kuwahudumia wafungwa kama wangekuwapo magerezani.

Pia Mrema alisema ziko changamoto mbalimbali ambazo zinaikabili bodi hiyo ikiwamo ufinyu wa bajeti katika kufanikisha shughuli zake na maeneo ya kiutawala na kisheria ambazo alisema hatua mbalimbali za utatuzi zinaendelea kufanyiwa kazi na mamlaka husika.

"Bodi hii ya tano imefanikiwa kwa kiasi kikubwa katika kutekeleza majukumu yake katika kipindi cha miaka mitatu. Licha ya changamoto hizo nilizozitaja, kipekee nitoe shukrani za dhati kwa wajumbe wa bodi kwa ushirikiano wao kwangu.

"Pia natoa shukrani za kipekee kwa Rais John Magufuli kwa kuniteua kuwa Mwenyekiti wa Taifa wa Bodi hii katika kutekeleza matakwa ya Sheria ya Bodi za Parole Sura ya 400," alisema.

Bodi ya Taifa ya Parole ya Awamu ya Tano ilizinduliwa na kuanza kufanya kazi zake Machi 21, 2016 inatarajia kumaliza muda wake wa kuwa madarakani kwa miaka mitatu ifikapo Julai 16, mwaka huu.

# HABARI KITAIFA



Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano (Mawasiliano), Dk Maria Sasabo (kulia), akijadiliana jambo na Mkuu wa Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania(TCRA) Kanda ya Kati, Antonio Manyanda (katikati), baada ya kufungua mafunzo ya siku moja kwa Wataalamu wa Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA), kutoka serikalini na taasisi za umma, jijini Dodoma jana. Kushoto ni Mkurungenzi wa Utawala wa wizara hiyo, Kitolina Kippa. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

## Museveni kutua nchini Tanzania leo

**Na Mwandishi Wetu**

RAIS wa Uganda. Yoweri Museveni, leo anatarajiwa kuwasili nchini kwa ziara binafsi ya siku moja.

Rais Museveni atamtembelea Rais John Magufuli kijijini kwake, Mlimani katika Wilaya ya Chato mkoani Geita.

Taarifa iliyotolewa na Kurugenzi ya Mawasiliano ya Rais Ikulu jana, ilisema Rais Museveni atafanya mazungumzo na mwenyeji wake Rais Magufuli.

Wiki iliyopita, Rais wa Kenya Uhuru Kenyatta, naye alifanya ziara ya siku mbili na kufanya mazungumzo na mwenyeji wake Rais Magufuli kijijini kwake Mlimani Wilaya ya Chato mkoani Geita.

# Korti yatoa neno kesi ya Ndama

**Na Hellen Mwango**

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Kisutu, Dar es Salaam, imeuamuru upande wa Jamhuri kutumia busara katika kesi inayomkabili mfanyabiashara , Ndama Hussein, maarufu kama 'Ndama Mtoto ya Ng'ombe' kukamilisha upelelezi au kumwondolea mashtaka mshtakiwa.

Aidha, imesema kesi hiyo ina miaka mitatu mahakamani hapo tangu mwaka 2016 lakini bado upelelezi haujakamilika.

Amri hiyo ilitolewa jana na Hakimu Mkazi Maira Kasonde aliyepangiwa kusijiliza kesi hiyo.

Mapema mahakamani hapo, Wakili wa Serikali Jenifer Masue, alidai kuwa upelelezi wa kesi hiyo haujakamilika na kwamba upande wa Jamhuri unaomba tarehe nyingine ya kitajwa.

Hata hivyo, upande wa utetezi ulidai kuwa kesi hiyo sasa imefikisha miaka mitatu lakini Jamhuri haina dalili ya kukamilisha upelelezi, hivyo kuomba mahakama kutoa ahirisho la mwisho.

Hakimu alisema upande wa Jamhuri utumie busara katika kesi hiyo kwamba ama wakamilishe upelelezi au waiondoe kesi hiyo mahakamani.

"Tangu mwaka 2016 mpaka leo (jana) upelelezi bado haujakamilika Jamhuri. Mtumie busara kukamilisha upelelezi au iondoeni kesi mahakamani dhidi ya mshtakiwa," alisema Hakimu Kasonde.

Katika kesi ya msingi, Ndama anadaiwa kuwa Februari 20, 2014 jijini Dar es Salaam, alighushi nyaraka za kibali cha kusafirisha madini na sampuli za madini kwa kusudi la kuonyesha kuwa kampuni ya Muru Platinum Tanzania Investment Company Limited iliruhusiwa kusafirisha maboksi manne ya dhahabu yenye kilogramu 207 yenye thamani ya Dola za Marekani 8,280,000.00 kwenda Australia kwa kampuni ya Trade TJL DTYL Limited wakati akijua si kweli.

Pia anadaiwa Machi 6, 2014 jijini Dar es Salaam, alighushi kwa kutengeneza hati ya kibali ya Umoja wa Mataifa, Ofisi ya Dar es Salaam, akijaribu kuonyesha kilogramu 207 za dhahabu kutoka Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo zilizotarajiwa kusafirishwa na kampuni ya Muru Platinum kwenda Australia kwa kampuni ya Trade TJL DTYL Limited, zimesafirishwa bila jinai yoyote wakati akijua si kweli.

Ndama pia anadaiwa Februari 20, 2014, alighushi fomu ya forodha yenye namba za usajili R.28092 akionyesha kampuni ya Muru imeilipa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) dola za Marekani 331,200 kama kodi ya uingizaji wa bidhaa ambazo zina uzito wa kilogramu 207 za dhahabu zenye thamani ya Dola za Marekani 8,280,000 kutoka Congo.

Shtaka lingine anadaiwa Februari 20, 2014 alighushi nyaraka za bima kutoka Phoenix of Tanzania Assurance Company Ltd akionyesha kampuni ya Muru imeyawekea bima maboksi manne yaliyokuwa na dhahabu hizo.

Anadaiwa kati ya Februari 26 na Machi 3, 2014, jijini Dar es Salaam kwa njia ya udanganyifu, alijipatia kutoka kampuni ya nchini Australia ya Trade TJL DTYL Limited Dola za Marekani 540,000 baada ya kudanganya atawapa na kusafirisha dhahabu hizo.

## Serikali yatishia kufuta leseni za madini

**Na Mwandishi Wetu,** GEITA

WIZARA ya Madini imesema itaendelea kufuta leseni zote za utafiti ambazo hazifanyiwi kazi na zile ambazo hazilipiwi na kuwapatia wachimbaji wadogo ili wazifanyie kazi na kuwasaidia kuinua uchumi wa nchi na kuzalisha ajira kwa vijana.

Naibu Waziri wa Madini, Stanslaus Nyongo, alisema hayo juzi alipokuwa akifungua Kongamano la siku tatu la Jukwaa la Mitaji na Maendeleo mkoani Geita lililodhaminiwa na Benki ya NMB katika ukumbi wa mikutano wa Halmashauri ya Mji wa Geita.

Alisema wzara imejizatiti kuendelea kutoa maeneo ambayo yataongeza uzalishaji kwa wachimbaji wadogo na kwamba wanataka kuona wanainuka kiuchumi ili kulipa mrabaha wa serikali na kodi.

"Sisi wizara hatutakaa kimya kuona baadhi ya watu ambao wamekuwa wakipatiwa maeneo kwa ajili ya kufanya utafiti wanakaa nayo bila kuyashughulikia. Tutaendelea kuyataifisha maeneo hayo na kuwapa wachimbaji wadogo ili kuinua vipato vyao," alisema Nyongo.

Aidha, Nyongo aliishukuru NMB kwa kuwa mstari wa mbele kuwasaidia wachimbaji wadogo ikiwa ni pamoja na kufadhili kongamano hilo na kwamba anaamini elimu ambayo wameipata itawasaidia kuweka akiba na kujulikana shughuli ambazo wanazifanya ili iwe rahisi kupatiwa mikopo.

Mkuu wa Mkoa wa Geita, Robert Gabriel, alisema Geita bado inakabiliwa na uhaba wa maeneo ya uchimbaji na kwamba ni vyema sasa kwa wizara kutuma wataalamu kuona namna ambavyo watawasaidia kupata maeneo mengine ya uchimbaji.

INAENDELEA UK. 8



# MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

## Makocha wapya Stars wasipangiwe majukumu

**BAADA** ya Timu ya Taifa kuondolewa katika hatua ya makundi kwenye fainali za Kombe la Mataifa ya Afrika (Afcon 2019), uongozi wa Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), iliamua kuvunja mkataba na aliyekuwa Kocha Mkuu, Emmanuel Amunike.

Uamuzi huo ulitokana na kocha huyo raia wa Nigeria kushindwa kupata matokeo mazuri katika mechi zake tatu za Kundi C, ambapo Taifa Stars ilicheza dhidi ya Senegal, Algeria na majirani zao Harambee Stars ya Kenya.

Amunike ambaye aliipeleka Taifa Stars katika fainali hizo, baada ya kuzikosa kwa miaka 39, aliacha kwa kichapo cha mabao 2-0 kutoka kwa Senegal, halafu ikafungwa mabao 3-2 ilipocheza na Harambee Stars na ikamaliza kwa kufungwa mabao 2-0 na Waarabu wa Algeria.

Ukurasa kwa Amunike, mchezaji wa zamani na mwenye mafanikio katika kikosi cha Timu ya Taifa ya Nigeria ( Super Eagles) na Barcelona ya Hispania, umeshafungwa rasmi na TFF tayari imeshatangaza warithi wake.

Makocha hao wapya ni Mrundi, Etienne Ndayiragije ambaye ndio kwanza ametua kwa mabingwa wa Kombe la FA, Azam FC, akiwa na rekodi nzuri ya kuonyesha soka la ushindani alipokuwa anaiongoza Mbao FC ya jijini Mwanza na msimu uliopita alikuwa akiinoa KMC FC.

Ndayiragije, ambaye sasa yuko Rwanda akiiongoza Azam FC kutetea taji la Kombe la Kagame, kwenye majukumu yake mapya kwenye kikosi cha Stars, atakuwa anasaidiana na Wazalendo, Juma Mgunda kutoka Coastal Union na Suleiman Matola "Veron" wa Polisi Tanzania.

TFF ilitangaza kuwa benchi hilo la ufundi ni la muda na jukumu lake kubwa ni kuivusha Taifa Stars ambayo inakabiliwa na mechi za kusaka tiketi ya kushiriki Fainali za Kombe la Mataifa ya Afrika kwa Wachezaji wa Ndani maarufu CHAN.

Taifa Stars itaanza mtihani huo kwa kuwakaribisha Harambee Stars, mchezo utakaochezwa Julai 28 mwaka huu kwenye Uwanja wa Taifa jijini Dar es Salaam.

Nipashe tunasema kuwa, huu ni wakati mwingine wa wadau wa soka kufahamu mipaka yetu. Makocha hao wanatakiwa kupewa uhuru wa kufanya kazi zao vema na kutoingiliwa kwa namna yoyote ile.

Endapo makocha hao wataachwa na kutumia uzoefu na taaluma waliyonayo, tunaamini wanaweza kutimiza malengo ya kazi waliyopewa, kwa sababu ya historia na rekodi ambazo zimewabeba.

Wadau wa michezo tunatakiwa tuendelee kuiamini TFF, ambayo ndio wasimamizi wakuu wa mpira wa miguu hapa nchini, sababu za kuajiri na kutimua makocha wanazifahamu wao.

Hakuna ambaye anapinga kuwa TFF, ndio walimleta Amunike nchini, nao ndio wamefanya uamuzi wa kuvunja mkataba wake, mazuri na mapungufu ya kocha huyo wanayafahamu wao na hivyo, wadau tuendelee kuheshimu kile ambacho kinafanywa na taasisi hiyo.

Tunaamini kuwa hakuna kiongozi wa TFF ambaye atapenda kuona Taifa Stars inafanya vibaya katika mashindano yoyote na uamuzi wao wa kubadilisha benchi la ufundi, unalenga kuipa mafanikio zaidi timu hiyo na si kuirudisha nyuma.

Tuendelee kuipa ushirikiano TFF ili iweze kutekeleza vema majukumu yake ya kila siku, kwa sababu kufanya vizuri kwa Taifa Stars ni sifa ya kila Mtanzania na si viongozi wa shirikisho hilo peke yao.

Kama ambavyo tuko mbele katika kukosoa, Nipashe inawakumbusha wadau kuhakikisha mnajitokeza kuchangia ili kusaidia maandalizi, kwa kuzingatia kiasi cha fedha kinachotolewa na wadhamini ni kidogo, wakati timu nyingine za Taifa za Vijana na Wanawake (Twiga Stars), zenyewe zikiwa hazina wadhamini.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Meneja Matangazo:** Kauthar D'souza, 0767 223311.
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Barnabas Maro

## Tumevuna tulichopanda, tusilalame

**'LALAMA'** au 'lalamika' ni kitendo cha kutoa maelezo yenye hisia ya kutoridhishwa na jambo. Kitendo cha kutoa sauti ya kuumia. Watanzania wanaopenda mchezo wa kandanda wamesononeka mno baada ya Timu ya Taifa (Taifa Stars), kurejea nchini kwa fedheha kutoka Misri ilikoshiriki fainali za Kombe la Mataifa Afrika (Afcon). Taifa Stars ilipoteza mechi zake zote tatu kama ilivyokuwa kwa timu za Burundi na Namibia!

Wahenga walisema "Lisemwalo lipo na kama halipo linakuja." Maana yake jambo linalosemwa huwa tayari limeshatokea au kama sivyo karibuni litatokea. Methali hii hutumiwa kumnasihi mtu mwenye tabia ya kuyapuuza mambo anayoambiwa na watu wengine kwa kuyaona kama upuuzi au uvumi tu. Yafaa kuyazingatia.

Hii ni mara ya tatu nalitahadharisha Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), jinsi ya kupata wachezaji watakaotumiwa na timu zetu za Taifa. Kwamba tujitoe kwenye mashindano ya kimataifa kwa muda wa miaka angalau mitatu ili tuzijenge timu zetu kuanzia za vijana.

Kwamba TFF iwe na chuo maalum cha kandanda kitakachokuwa na mambo muhimu kuhusu mafunzo ya kabumbu. Pia viwanja vya mazoezi na mechi, madarasa ya kufundishia, bwana la kuogelea, ukumbi wa mazoezi ya viungo (gymnasium/gym) na zahanati. Ikiwezekana, atumwe mwalimu mmoja au hata wawili, kutembelea shule za Ulaya ili kujua wanavyofanya wenzetu. Wakati huohuo, kuwe na jopo la walimu wananchi wa kandanda na wengine kutoka nje ya nchi.

Kazi yao iwe kuzunguka nchi nzima ili kupata vijana wadogo na wakubwa wenye mwelekeo mzuri wa mchezo wa kandanda. Wapelekwe kwenye shule maalum ya kandanda itakayojengwa na TFF katika mkoa utakaopendekezwa.

Wakati hayo yakitendeka, vilabu vya kabumbu humu nchini vipigwe marufuku kuwaghilibu vijana hao kwa lengo la kuwasajili. Vilabu vitakavyotaka kuwasajili vijana hao, vijadiliane na TFF na kukiwa na makubaliano, wanunuliwe kama wanavyosajiliwa wachezaji wa kigeni kwa mamilioni ya hela. Vilevile vilabu vyetu visiwazuie wachezaji wetu wanaotakiwa na timu za nnje. Waruhusiwe ili wakachote ufundi zaidi na kuwa tegemeo kwa timu zetu za Taifa.

Wakati hayo yakiendelea, TFF ifanye mipango na nchi kama Brazil, Uingereza, Ufaransa, Ujerumani, Hispania na Ureno ili ikiwezekana ipeleke makocha wetu wa kandanda kwenda kujifunza zaidi mbinu za kisasa. Tofauti na hivyo, tutakuwa watu wa kubadili makocha wa kigeni kama nguo kila msimu baada ya timu zetu kushindwa kwenye mashindano ya kimataifa. Hivyo Tanzania itaendelea kuwa wasindikizaji, watalii na 'kichwa cha mwendawazimu.'

Emmanuel Amunike aliyeajiriwa na TFF msimu uliopita kuwa kocha wa Taifa Stars ameachishwa kazi baada ya Taifa Stars kushindwa mechi zote za AFCON kule Misri na kurejea nyumbani bila hata alama moja kwa mechi tatu ilizocheza!

Ingawa Amunike amekubaliana na TFF kuhusu kuondoshwa kwenye kazi yake, kocha huyo amesema kwa hali ilivyo sasa, ni vigumu kandanda la Tanzania kusonga mbele. Ameshauri kuwa ili Tanzania isonge mbele kwenye mchezo wa kandanda, ni lazima kuwe na misingi mizuri na imara ya kuziandaa timu za Taifa.

Matokeo yake yaweza kuonekana baada ya miaka sita ijayo. Tatizo lingine la TFF ni kuruhusu timu zetu kusajili wachezaji 10 wa kigeni.

Mbali ya upotevu wa fedha za nchi, pia ni kuinyima Tanzania kuwa na wachezaji mahiri ndo maana uchezaji wetu huishia humu humu nchini. Timu zetu zikienda nchi za nje zafanywa kama timu za kuzipa mazoezi timu za huko! Karibu timu zote zilizoshiriki michuano ya AFCON kule Misri zilikuwa na wachezaji wengi wanaocheza ligi za Ulaya. Kuna wakati wachezaji wetu walionekana kama wanafunzi wa kandanda kwa jinsi walivyokuwa wakikimbizwa ovyo na kupigwa chenga za maudhi kiasi cha kutukatisha tamaa tuliokuwa tukiangalia runinga.

Hakuna mkulima anayelima, kupanda mbegu na kuvuna baada ya muda mfupi. Kuna kufanya matayarisho ya shamba kwa kulima kisha kusubiri majira ya mvua za kupanda mbegu. Kinachofuatia ni palizi na mwishowe ni kuvuna kilichopandwa.

Wahenga walitambua hili mapema waliposema "Penye nia pana njia" wakiwa na maana kwamba ikiwa mtu ana dhamira ya kufanya jambo, hawezi kukosa njia. Methali hii hutumiwa kutukumbusha kwamba tunapodhamiria kufanya jambo, lazima tutafanikiwa. Kwa hiyo tusikate tamaa bali twapaswa kuongeza juhudi. Kama wenzetu wanaweza, kwa nini sisi tushindwe?

**marobarnabas@yahoo.com**
**0784 334 096**

# Kigogo CCM kortini madai ya kughushi cheti cha ndoa

**Na Hellen Mwango**

MWENYEKITI wa zamani wa Umoja wa Wanawake wa CCM (UWT) Wilaya ya Ilala, Norah Waziri, maarufu kama Nora Mzeru, amefikishwa katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kinondoni, Dar es Salaam, akikabiliwa na shtaka la kughushi cheti cha ndoa.

Kigogo huyo alisomewa mashtaka yake mbele ya Anifa Mwingira aliyepangiwa kusikiliza kesi hiyo.

Wakili wa Serikali, Benson Mwaitenda, alidai kuwa Februari 4, 1995 jijini Dar, es Salaam, kwa nia ya kudanganya, mshtakiwa alighushi cheti cha ndoa chenye usajili namba 00040078.

Ilidaiwa kuwa alifanya hivyo kwa nia ya kuonyesha kuwa alifunga ndoa na Silvanus Mzeru (sasa marehemu) Februari 4, 1995 katika Kanisa la Katoriki la Parokia ya Mburahati, huku akijua si kweli.

Mshtakiwa alikana shtaka hilo na kusisitiza kuwa Mrezu alikuwa mume wake wa ndoa.

Upande wa Jamhuri ulidai kuwa upelelezi wa kesi hiyo bado haujakamilika.

Mawakili wa utetezi, Mtubika Godfrey na Juma Nyamgaruri, waliiomba mahakama kumpatia dhamana mteja wao kwa sababu shtaka linalomkabili kwa mujibu wa sheria linadhaminika.

Hakimu Mwingira alisema mshtakiwa atakuwa nje kwa dhamana kwa kutimiza masharti ya kuwa na wadhamini wawili, mmoja kati ya wadhamini hao kutoka taasisi inayotambulika na serikali. Mbali na masharti hayo, alimtaka kila mdhamini kutia saini hati ya dhamana ya Sh. milioni moja. Mshtakiwa alitimiza masharti hayo yuko nje kwa dhamana mpaka Julai 17, mwaka huu kesi itakapotajwa.

Awali, Oktoba 24, mwaka jana, mshtakiwa alifikishwa katika Mahakama ya Wilaya ya Ilala na kusomewa shtaka la kughushi mbele ya Hakimu Mkazi Flora Haule.

Hata hivyo, mwaka huu kesi hiyo ilifutwa mahakamani hapo kwa sababu mahakama ile ilikuwa haina mamlaka ya kusikiliza na kufunguliwa upya mahakamani hapo jana




Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Balozi Seif Ali Idd akikabidhi cheti cha kutambua taasisi za kifedha na mshindi wa tatu kwa Meneja Masoko na Uhusiano wa benki ya Maendeleo ya TIB, Saidi Mkabakuri, wakati wa kufunga Maonyesho ya 43 ya Biashara ya Kimataifa jijini Dar es Salaam juzi. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Hospitali yatekeleza agizo la JPM kwa kuzalisha drip

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

HOSPITALI ya Rufani ya Kanda ya Mbeya, imeanzisha kiwanda cha kuzalisha maji tiba (drip) ili kuokoa gharama kubwa ambazo zilikuwa zinatumika kuagiza nchini Uganda.

Hatua hiyo ya hospitali ni utekelezaji wa sera ya uwekezaji wa viwanda vya dawa nchini ambayo imekuwa ikitiliwa mkazo na Rais John Magufuli.

Waziri wa Afya, Maendeleo na Jinsia, Wazee na Watoto, Ummy Mwalimu, alisema hayo jana wakati wa ziara yake ya kukagua hali ya utoaji huduma kwenye hospitali hiyo. Ummy alieleza kufurahishwa na namna hospitali hiyo ilivyoamua kuanzisha kiwanda hicho ili kuokoa serikali kutumia fedha za kigeni kuagiza maji hayo nchini Uganda. Zaidi ya Sh. bilioni 24 hutumika kila mwaka kuagiza maji hayo.

"Nafurahi kuona hospitali ya rufani ya kanda imeamua kuanzisha kiwanda cha kutengeneza maji tiba yaani drip ili kukabiliana na changamoto ya uhaba wa maji hayo pia kuokoa gharama za serikali na kuuza kwa wengine. Hakika mmemfurahisha Rais wetu Dk. Magufuli. Nasisitiza hospitali nyingine kuiga mfano huu," alisema Waziri Ummy. Alisema hospitali hiyo si tu imeanzisha kiwanda hicho kupunguza uhaba na kuokoa fedha bali pia kupitia hatua hiyo, imetengeneza ajira kwa Watanzania na kuwataka wafamasia kutumia taaluma yao kwa kuanzisha viwanda hivyo katika hospitali zote nchini.

Mfamasia wa Hospitali ya Rufani Kanda ya Mbeya, Mkimbili Chalo, alisema kuanzishwa kwa kiwanda hicho kimesaidia kupunguza gharama za kununua malighafi kwa kuwa zinapatikana nchini. Alisema kupatikana kwa bidhaa hiyo kumeiwezesha hospitali kuzalisha maji tiba hayo kwa uhakika na kuokoa gharama za serikali.

Mkurugenzi Mtendaji wa Hospitali hiyo, Goodlove Mbwanji, aliishukuru serikali kwa kuendelea kuboresha sekta ya afya na kuahidi kuendelea kuunga mkono utekelezaji wa sera ya uwekezaji wa viwanda vya dawa nchini.

Alisema kwa sasa wanazalisha maji ya kutumika hospitalini hapo yakiwa yamepita kwenye viwango vya ubora na matarajio yao ni kuendelea kuzalishaji maji hayo zaidi.

Alisema matajario mengine ni kuanza kuzalisha dawa za kutibu magonjwa ya macho ambazo zitasaidia kwa kiasi kikubwa kukabiliana na changamoto ya wagonjwa wa macho.

## St Anne Marie wataja siri ufaulu kidato cha 6

**Na Mwandishi Wetu**

SHULE ya St Anne Marie Academy ya jijini Dar es Salaam, imetaja sababu ya mafanikio kwenye matokeo ya kidato cha sita na mtihani wa majaribio wa darasa la saba kwa Mkoa wa Dar es Salaam.

Mkuu wa Shule hiyo, Gladius Ndyetabura, aliliambia gazeti hili jana kuwa kwa ujumla matokeo ya kidato cha sita na mtihani wa majaribio yamewaweka sehemu nzuri sana

Alisema kwenye matokeo ya kidato cha sita wamefanikiwa kutoa wanafunzi 19 wa daraja la kwanza, wanafunzi 47 daraja la pili, wanafunzi 21 daraja la tatu na hawakupata daraja la nne wala 0.

Kuhusu matokeo ya Mock, Ndyetabura alisema shule yake imeendeleza mafanikio ya kila mwaka ambapo safari hii wanafunzi wengi wamefaulu kwa wastani wa alama A.

Alisema wanafunzi 86 walifanikiwa kupata wastani wa alama A na wanafunzi 13 tu ndiyo walipata alama B na kwamba hakuna mwanafunzi hata mmoja aliyepata alama C,D wala E.

"Tunawashukuru walimu kwa kazi kubwa wanayofanya kuhakikisha tunapata matokeo mazuri kama haya na tunaushukuru uongozi wa shule hususan Mkurugenzi Jasson Rweikiza kwa ushirikiano uliosababisha kupatikana kwa matokeo haya tunaahidi makubwa zaidi," alisema Ndyetabura

Alisema hii si mara ya kwanza kwa shule yake kufanya vizuri kwenye mitihani ya kitaifa kwani hivi karibuni Mkoa wa Dar es Salaam uliipatia Ngao Maalum shule hiyo kama sehemu ya kutambua mchango wake katika kuinua elimu hapa nchini na kuwa miongoni mwa shule zinazofanya vizuri kitaaluma.

Alisema shule yake ilipewa ngao inayoonyesha kuwa ni miongoni mwa shule zilizofanya vizuri zaidi kwenye matokeo ya darasa la saba Best Performing Primary School in Tanzania.

Alisema shule yake pia ilifanikiwa kuingia kumi bora kwenye matokeo ya darasa la saba mwaka jana na kwamba nia yake ni kuwa namba moja kitaifa kwenye matokeo yanayokuja.

"Kwenye matokeo ya darasa la saba mwaka jana tumefanikiwa kuwa wa kwanza Wilaya ya Ubungo, tumekuwa wa pili Mkoa wa Dar es Salaam na tulikuwa wanane kitaifa sasa hii haitufanyi tubweteke tutapambana kupata nafasi za juu zaidi," alisema.

# Lugha ya alama yapewa vyombo vya haki

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

SERIKALI imesema iko haja ya kuwapo mitaala ya mafunzo ya lugha za alama katika vyuo vya polisi, mahakama na magereza ili kuwawezesha maofisa wa taasisi hizo kuwasiliana na kutoa uamuzi wa haki katika kesi na mashauri yanayowahusisha viziwi.

Katibu Mkuu wa Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, Meja Jenerali Jacob Kingu, alisema hayo jana katika kongamano la kitaifa la lugha za alama kwa vyombo vya ulinzi na usalama lililofanyika katika ukumbi wa Bunge, jijini hapa.

Alisema vyombo vya ulinzi na usalama vinatakiwa kujua lugha za alama kwa sababu vinakutana na mashauri mengi ikiwamo kesi zinazohusu jamii ya viziwi ambazo ni ngumu kuamua kama hujui lugha ya alama.

"Ni muhimu mitaala hiyo iwapo katika vyuo hivyo kwa sababu itasaidia kuepusha migongano baina ya pande hizo mbili pale zinapokutana katika mashauri," alisema.

Alisema kuna kila sababu ya watoa huduma kwa umma kujua mahitaji ya lugha za alama ambayo yanapaswa kuzingatiwa katika kutoa huduma muhimu kwa jamii kama vile haki, ulinzi, usalama, afya, elimu na uwezekano wa ushiriki kikamilifu wa viziwi katika shughuli zote za maendeleo ya taifa.

Kutokana na hilo, aliushukuru mfuko wa asasi za kiraia kwa kutoa ushirikiano kwa watu wenye ulemavu, huku akizitaka taasisi zingine ziige mfano wa asasi hiyo, ikiwamo kujenga mazoea ya kushirikiana pamoja na kundi hilo.

Naye Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Katiba na Sheria, Amon Mpanju, alisema lugha ya alama za mawasiliano kwa watu wenye ulemavu kwa vyombo vya ulinzi na usalama ni muhimu kwa sababu zinawasaidia kuwatambua wanapokutana nao katika matukio mbalimbali ya kiutendaji.

Alisema kutokana na hilo, serikali inapaswa kuhimiza taasisi mbalimbali kutoa elimu hiyo kwa jamii hasa ikizingatiwa kuwa taifa linaelekea katika uchaguzi wa serikali za mitaa ili makundi hayo yashiriki kikamilifu.

Mpanju alisema lugha za alama kwa vyombo vya ulinzi na usalama ni muhimu kutokana na ukweli kwamba zitawasaidia kuwatambua ikiwamo kuwaepushia hatari pale wanapokuwa wamekutwa na matatizo na kushindwa kujieleza.

"Ni muhimu vyombo vya ulinzi na usalama kujua lugha hiyo kwa sababu ukiwa unamhoji kiziwi itakusaidia kumjua ikiwamo kuondoa adha ya kumpiga ilihali anakuwa na haki," alisema Mpanju.

Alisema kutokana na hilo, kuna kila sababu ya vyombo hivyo kuanza kutoa elimu hiyo ya muda mfupi na baadaye kipindi kirefu, jambo ambalo litasaidia jamii kulitambua kundi hilo.

Alisisitiza serikali itaendelea kuhimiza taasisi mbalimbali kutoa elimu ya alama hizo hususani katika kipindi cha uchaguzi wa serikali za mitaa kwa sababu kundi hilo linahitaji kushiriki kikamilifu katika mchakato huo.

"Lugha hii ni muhimu kwa kila mmoja na si viziwi pekee kwa sababu jamii ya watu hawa tunakutana nao kila mahali," alisema Mpanju.

## Serikali yatishia kufuta leseni

INATOKA UK. 5

Ofisa Mkuu wa Wateja Wadogo na wa Kati wa NMB, Filbert Mponzi, alisema benki hiyo inatambua mchango wake mkubwa kwa jamii wakiwamo wachimbaji wadogo na ndiyo sababu ambayo imewafanya kufadhili kongamano hilo.

"Imani yetu ni kwamba maelekezo na elimu ambayo tumeitoa naamini wachimbaji wadogo wakiifanyia kazi sisi tuko tayari kuwakopesha. Tulikuwa tunashindwa kutokana na namna ambavyo walikuwa wakihama hama lakini naamini maelekezo tuliyowapa watayatekeleza," alisema.

Baadhi ya wachimbaji wadogo mkoani hapa, waliishukuru NMB kuwa tayari kuwakopesha na kwamba kupitia mikopo watakayopatiwa, itawasaidia kwa kiasi kikubwa kuboresha shughuli zao za uchimbaji ambazo wamekuwa wakizifanya kila siku.




Wakazi wa Jiji la Dar es Salaam wakichagua nguo za mtumba katika eneo la Kariakoo sokoni jana. Wananchi hupendelea nguo hizo kutokana na kuuzwa bei nafuu. **PICHA: GETRUDE MPEZYA**

## Jafo ataja siri shule za serikali kung'ara

INATOKA UK. 2

"Haya ni mafanikio makubwa ambayo tumedhamiria kuyafanya. Tumeona shule hizi mbili zina asili ya kata, niwapongeze walimu na wanafunzi kwa ufanya vizuri," alisema.

Aidha, alisema nafasi ya 11 hadi 20, shule sita za serikali ambazo ni Ilboru, Nachingwea, Mzumbe, Mwanamwema, Tabora Wasichana na Dareda zimeingia katika kundi hilo.

"Shule hizi zinafanya vizuri ikilinganishwa na kule tulikotoka mwanzo. Pia katika shule 100 bora mwaka huu, 64 ni za serikali ambazo 52 ni za kata na 12 ni shule kongwe na vipaji maalum," alisema.

Alisisitiza kuwa shule za kata kwa sasa zinatimua mbio licha ya wengine walikuwa wakizibeza.

"Wazazi acheni watoto wasome kwenye hizo shule serikali imeweka mazingira rafiki kupeleka vifaa na walimu na haya ndo matunda makubwa ya serikali,"alisema.

Kadhalika, alisema katika wanafunzi 10 bora watano wametoka shule za serikali na watano bora wa masomo ya sayansi ni wa shule za serikali.

Alipongeza mikoa ya Arusha, Tabora na Pwani ambayo shule za serikali zimefanya vizuri kwa kuingia 10 bora.

"Nimpongeze Mkuu wa Mkoa wa Pwani (Evarist Ndikilo) anajitahidi sana. Kuna shule pale inaitwa Maneromango ndiyo imetoa kwa mara ya kwanza wanafunzi wa kidato cha sita. Imekuwa shule ya 59 kitaifa kati ya shule 594 na ni shule ya pili kwa mkoa wa Pwani ukiacha Kibaha," alisema.

Alisema ataandaa vyeti maalum kwa wakuu wa mikoa hiyo mitatu huku akiagiza tathmini ifanyike kwa mikoa iliyofanya vibaya ili kutafutia ufumbuzi changamoto zinazokwamisha ufaulu.

## Waziri ashtushwa mil. 60/- kununua dawa ya mchwa

INATOKA UK. 3

sababu yeyote na anataka ifikapo Julai 30 Hospitali hiyo iwe imekamilika.

Akitolea ufafanuzi changamoto zilizojitokeza katika ujenzi wa hospitali hiyo, Mkuu wa Wilaya ya Morogoro, Regina Chonjo, alisema Kamati ya Ulinzi na Usalama imekuwa ikishauri kila wakati namna bora na ya haraka ya kukamilisha mradi huo lakini kumekuwa na mwitikio mdogo wa wataalamu wa halmashauri katika kutekeleza yale yanayoshauriwa.

**DED AJITETEA**

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Morogoro, Masoud Rioba, alisema ununuzi wa dawa za kuua mchwa kuwa yalijumuishwa kwenye taarifa ya mradi katika kipengele cha vifaa vya ujenzi na si kwenye kipengele kinachojitegemea ndiyo maana si rahisi kuiona kwa uharaka.

"Manunuzi (ununuzi) ya (wa) dawa yamejumuishwa (umejumuishwa) kwenye vifaa vya ujenzi, haionekani kwa haraka kwa sababu hatukuiweka peke yake na gharama yake ni Sh. milioni 60. Hii ni baada ya kununua lita 1500 ambazo ndizo zilizokuwa zinahitajika na kila lita moja ilikuwa na gharama ya Sh. 55,000 hivyo kuleta gharama ya zaidi ya Sh. milioni 60,"alisema.

Akifafanua kuhusu fedha zilizobaki kama zinaweza kukamilisha ujenzi wa hospitali hiyo, alisema mpaka sasa vifaa vingi vimekwishanunuliwa hivyo fedha hiyo itafanya kazi za ukamilishaji wa majengo hayo na kumhakikishia Jafo kuwa kazi hiyo itakamilika kwa fedha zilizobakia.

Hata hivyo, Mmoja wa mafundi wanaojenga, alimlalamikia Waziri kuwa kukosekana kwa vifaa vya ujenzi kwa muda mrefu katika hospitali hiyo na kusuasua kwa malipo ya mafundi hao kumewakatisha tamaa.

# Serikali yawapoza wajasiriamali, wafanyabiashara

**Na Cynthia Mwilolezi,**
ARUSHA

SERIKALI imewataka wajasiriamali na wafanyabiashara kufanya biashara zao bila hofu na kuboresha bidhaa zao kwa kuwa imefuta tozo 49 zilizokuwa zinalalamikiwa.

Naibu Waziri wa Viwanda na Biashara, Stella Manyanya, aliyasema hayo alipokuwa akizungumza na wamiliki wa viwanda na wajasiriamali waliopatiwa mafunzo ya kibiashara kutoka Shirika la Maendeleo yua Viwanda Vidogo (SIDO) pamoja na mkopo.

Alisema serikali ilifuta utitiri wa tozo zilizokuwa zinalalamikiwa, baada ya

kufanya kikao na wafanyabiashara Ikulu jijini Dar es Salaam hivi karibuni, hivyo kuwapunguzia mzigo wafanyabiashara na wajasiriamali.

"Sasa fanyenyi kazi zenu kwa kujiamini na kufuata misingi iliyopo.

Lakini kama mtu anatakiwa kulipa kodi lipeni na mziboreshe bidhaa ili zipate masoko ndani na nje ya nchi maana hakuna kikwazo kwa sasa sababu serikali tumewasikiliza na tumetekeleza kwa kufuta tozo mlizokuwa mkizilalamikiwa," alisema.

Manyanya pia alisema kwa sasa serikali iko katika ujenzi wa viwanda na hivi karibuni alikutana na Waziri wa Uholanzi kwa lengo la kuwajengea mazingira ya uwezeshaji wafanyabiashara ili kuuza bidhaa zao nje ya nchi.

Alisema Sido imepiga hatua katika teknolojia na jukumu lililopo sasa ni kuendelea kuhamasisha na kuwaomba wajasriamali wazidishe ubunifu, wazalishe bidhaa zenye ubora zaidi, watumie mitandao kutafuta masoko.

Aidha aliwasisitiza wajasiriamali na wafanyabiashara kutumia lugha zinazoeleweka za Kiswahili kwa ajili ya soko la ndani na Kiingereza kwa ajili ya soko la nje, ili kumwezesha mtumiaji kuelewa aina ya bidhaa anazotumia.

Alisema wizara imejipanga katika kanda saba kwa ajili ya kuwasikiliza wadau na anatembelea nchi nzima ili kuzungumza nao na kwa kuanza ameanzia Arusha na Manyara.

Awali, Meneja wa Sido Mkoa wa Arusha, Nina Nchimbi, alisema kwa sasa shirika hilo linaanza kuwafundisha wajasiriamali elimu ya haki miliki kwa ajili ya kulinda biashara zao kwa kuwa wengi wao hawana elimu hiyo.

Aliongeza kuwa Sido katika kazi zake imekuwa ikishirikiana na taasisi zingine za serikali ikiwamo Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) katika kutoa elimu, ili kuwaondolea wananchi usumbufu lakini kuna baadhi ya watumishi wa taasisi hizo wanalalamikiwa .

Wakichangia kwenye kikao hicho wadau hao ambao hawakutaka majina yao yatajwe, waliilalamikia ofisi ya Mkemia Mkuu wa Serikali kuwa ina urasimu, hivyo kuwa ni kikwazo katika shughuli zao.

Taasisi nyingine iliyolalamikiwa ni TRA Mkoa wa Arusha kuwa kuna baadhi ya watendaji wake ni kikwazo na kuna kulindana, hivyo kusababisha wajasiriamali 67 waliopatiwa mafunzo na Sido kushindwa kuanzisha viwanda.



Katibu Mkuu wa CCM, Dk. Bashiru Ally, akisaini kitabu cha wageni kwenye uzinduzi wa Shina la Wakereketwa G8 la Mji mdogo wa Mirerani, wilayani Simanjiro juzi. Kushoto ni Mwenyekiti wa shina hilo, Omary Mandari na Katibu Jafari Matimbwa. **PICHA: GIFT THADEY**

## Apongeza wananchi kumaliza mgogoro

**Na Cynthia Mwilolezi,** SIMANJIRO

MBUNGE wa Simanjiro mkoani Manyara, James Ole Millya, amewashukuru wananchi wa Vijiji vya Sukuro na Kitiangare, waliomaliza mgogoro wao uliodumu zaidi ya miaka 20 wakigombea Kitongoji cha Katikati.

Mgogoro huo ulishasababisha mtafaruku mkubwa baina ya aliyekuwa Mkuu wa Mkoa huo, Henry Shekifu na aliyekuwa Mbunge wa Jimbo hilo, Christopher Ole Sendeka mwaka 2010.

Akizungumza jana na wananchi wa Kijiji cha Sukuro, aliwapongeza wananchi wa vijiji hivyo viwili, kwa kuridhia kwa pamoja na kuachana na malumbano na mgogoro usio na tija kwao.

Alisema katika mgogoro huo, binafsi alikaa pembeni bila kupendelea kijiji chochote, kwa kuwa vyote viwili ni vyake, hivyo hakupaswa kupendelea kimoja na aliwaachia wataalamu wagawe vitongoji kama sheria inavyoelekeza.

"Nawapongeza sana wananchi wa vijiji vya Kitiangare na Sukuro, kwani hali ya amani haikuwapo lakini sasa mmemaliza mgogoro wenu na kuridhia kwa pamoja kuishi kama ndugu kwani mlikuwa kijiji kimoja kabla ya kugawanywa," alisema.

Alisema hivi sasa hali ya amani na upendo imerejea baina ya vijiji hivyo viwili kama awali na wananchi wanasalimiana kwa furaha, wanaoleana na kunywa maji pamoja.

Ole Millya alisema kupitia mfuko wa jimbo, anatoa Sh. milioni sita kwa vikundi vya wanawake wa vijiji vyote viwili na Sh. milioni nne kwa mradi wa maji kijiji cha Sukuro na darasa la shule ya kijiji cha Kitiangare.

Mkazi wa Kijiji cha Sukuro, Lengai ole Makoo, alipongeza hatua ya kumalizika kwa mgogoro huo, usiokuwa na tija uliosababishwa na baadhi ya wanasiasa wa wilaya hiyo.

# Watishia kuchoma moto ngozi za mifugo

**Na Woinde Shizza**,
ARUSHA

ZAIDI ya wafanyabiashara 130 wa nyama katika Jiji la Arusha, wametishia kuteketeza ngozi za mifugo wanazozalisha baada ya kuchinja mifugo kwa sababu wameshindwa kupata masoko ya uhakika ya zao hilo.

Hatua hiyo inatokana na kampuni zinazojihusisha na biashara hiyo kutowalipa kwa zaidi ya miaka minne sasa.

Mwenyekiti wa wafanyabiashara hao, Alex Lasike, alisema jana katika kikao cha pamoja kuwa wamefikia uamuzi huo baada ya kukata tamaa na zao hilo, kutokana na kukosekana kwa masoko ya uhakika huku bei ya zao hilo ikiendelea kuporomoka.

Alisema hali hiyo imewafanya wafanyabiashara hao kutishia kuachana na biashara ya ngozi, badala yake watakuwa wakiziteketeza kwa moto au kuwapa mbwa kama chakula baada ya kampuni za Salex Limited na Ngozi Center za jijini Arusha kushindwa kuwalipa mamilioni ya fedha wanazozidai katika kipindi hicho. "Ni mwaka wa nne tunauza ngozi tena kwa bei ndogo ya Sh. 100 kwa kilo moja katika kampuni hizo binafsi lakini hatujawahi kulipwa kwa muda mrefu na watu wanazidi kuumia," alisema Lasike.

Alisema kila siku wafanyabiashara hao wanachinja ng'ombe, mbuzi na kondoo zaidi ya 150 lakini ngozi zinazopatikana zinakusanywa na kampuni hizo kwa ajili ya malipo, lakini hadi sasa wanasotea zaidi ya miaka minne.

Lasike aliiomba serikali kuwatafutia soko la uhakika ili waachane na kampuni hizo zinazonunua kwa mkopo na kushindwa kuwalipa kwa wakati.

Baadhi ya wafanyabiashara wa nyama, katika Jiji la Arusha, Hopson Minja na Elius

Lazaro, walisema wamesikitishwa na kampuni hizo zinazonunua ngozi, kushindwa kuwalipa fedha zao na kuiomba serikali iingilie kati ili wapate haki zao.

"Kwa mfano mimi nadai zaidi ya Sh. milioni nne sijalipwa kwa zaidi ya miaka minne sasa. Naiomba serikali itusaidie kupata haki zetu, pamoja na kututafutia soko la uhakika la ngozi," alisema Minja.

Mmoja ya wamikili wa kampuni ya Salex Limited, Mahsin Ghalib, alisema biashara ya ngozi katika soko la dunia imeporomoka kwa kiasi kikubwa, kutokana na nchi zilizokuwa zikinunua kutokununua kwa wingi, jambo linalosababisha biashara hiyo kudorora.

"Kiwandani kwangu kuna shehena ya ngozi zaidi ya kilo milioni 2.8 sina mahala pa kuuzia. Masoko hakuna, nchi zilizokuwa zikinunua siku hizi hawataki ngozi za chumvi," alisema Ghalib

# Wafanyabiashara waiasa Tantrade urasimu

**Na Godfrey Mushi,** MOSHI

BAADHI ya wafanyabiashara wa viwanda mkoani Kilimanjaro, wameitaka Mamlaka ya Maendeleo ya Biashara nchini (Tantrade), kutoruhusu malalamiko ya kuwapo urasimu, wakati wa zoezi la kuipeleka kliniki ya biashara katika kila mkoa kwa ajili ya kutatua changamoto za biashara.

Mfanyabiashara na mmiliki wa kiwanda cha kutengeneza vifaa vya ujenzi, Amran Kangesa, mkazi wa Moshi, alisema uamuzi wa mamlaka hiyo kuanzisha kliniki kwa lengo la kuwasaidia wafanyabiashara kupata mafaniko yatakayowawezesha kuwa wafanyabiashara wakubwa na kuinua uchumi, ni jambo ambalo linahitaji umakini katika utekelezaji wake.

"Tuna imani na Tantrade katika hili la kuanzisha kliniki, lakini ushauri wetu ni kwamba wasikubali urasimu ukatikisa tena mfumo huo kwa sababu shida kubwa wanayoiona wafanyabiashara ni ujanja wa baadhi ya watumishi wanapokutana na wafanyabiashara kusikiliza kero zao," alisema Kangesa.Aidha, mfanyabiashara Kennedy Olottu, alisema ili kuvutia wafanyabiashara wa viwandani, maduka makubwa, sekta mtambuka kama bidhaa za kilimo mifugo na maeneo mengine kama ujenzi ni vyema serikali ikaweka mazingira rafiki ya wafanyabiashara na kuondoa urasimu ili kufanikisha kaulimbiu ya Tanzania ya viwanda.Kwa upande wake, mfanyabiashara Goodluck Sareiyo, ambaye anamiliki maduka ya pembejeo alisema mambo ambayo Tantrade inapaswa kuyaangalia wakati itakapoanza kuitembeza mikoani kliniki hiyo ni pamoja na njia wanayoitumia kudai kodi Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), kwa vile inaonekana kuwakimbiza nchini baadhi ya wafanyabiashara.

Juzi, Mkurugenzi Mkuu wa Tantrade, Edwin Rutageruka, alikaririwa akisema kuwa wameanzisha kliniki ya biashara katika viwanja vya maonyesho ya Sabasaba ili kutatua changamoto za biashara, kwa lengo la kuwasaidia wafanyabiashara kupata mafaniko yatakayowawezesha kuwa wafanyabiashara wakubwa na kuinua uchumi.

Kwa mujibu wa Rutageruka, uanzishwaji wa kliniki hiyo umetokana na agizo la serikali la kutaka kuboresha mazingira ya biashara nchini.



Meneja wa shamba la miti la Lunguza, wilayani Muheza, Mkoa wa Tanga, Elyneema Mwasalanga (kushoto), akikabidhi msaada wa mbao 184 kwa Mbunge wa jimbo la Muheza, Balozi Adadi Rajabu, kwa ajili ya kusaidia utengenezaji wa madawati ya shule za wilaya hiyo, juzi. **PICHA: STEVEN WILLIAM**

# Latra yaombwa kuingilia kati upandaji nauli

**Na Mwandishi Wetu,** SIHA

MAMLAKA ya Udhibiti wa Usafiri wa Ardhini (Latra), imeombwa kuingilia kati, tatizo la upandishaji wa nauli kiholela ambalo linaendelea kuwaumiza abiria wanaosafiri kwa mabasi madogo yanayofanya safari zake katika Barabara Kuu ya Sanya Juu-West Kilimanjaro.

Mabasi yanayodaiwa kupandisha nauli bila kuthibitishwa na Latra ni yale yanayotumia barabara hiyo inayoendelea na ujenzi wa kilomita 32.2 za kiwango cha lami zinazojengwa na serikali kwa gharama ya Sh. bilioni 52.19.

Jana, wananchi hao wakiongozwa na Diwani wa Kata ya Ndumeti iliyopo Wilaya ya Siha, mkoani Kilimanjaro, Jackson Rabo, waliiomba mamlaka ya hiyo kuchukua hatua dhidi ya madereva wa mabasi hayo ya abiria kupandisha nauli kiholela kutoka Sh. 1,000 hadi Sh. 3,000 kwa mzunguko mmoja.

"Hatuwezi kukubali hali hii iendelee kutuumiza wananchi, Latra waje wafanye uchunguzi hata kwa kujificha na kutojitambulisha na wakibaini kuna ongezeko hilo la nauli mara mbili ya bei elekezi, wachukue hatua dhidi ya madereva na makondakta wa mabasi hayo," alisema Rabo.

Alisema inasikitisha kuona kwamba baada ya barabara hiyo kukaribia kukamilika na kukabidhiwa serikalini, wenye mabasi hayo wamepandisha nauli, badala ya kupunguza kutokana na kuboreshwa kwa miundombinu ya barabara hiyo. Madereva hao wanadaiwa kupandisha nauli hiyo kutokana na ubovu wa barabara.

Baadhi ya wananchi walipaza sauti zao wakilaani upandishaji huo wa nauli, wakiwamo Jonh Mbwambo na Aisia Kombe, walisema kuwa wamekuwa wakinyanyaswa na madereva na makodkta wa magari hao ya abiria kwa kulipishwa fedha hizo kwa nguvu bila hata ya kupewa tiketi.

Alipotafutwa kutoa ufafanuzi kuhusu malalamiko hayo, Ofisa Mfawidhi wa Latra, Mkoa wa Kilimanjaro, Johns Makwale, alisema taarifa kuhusu malalamiko hayo wameshazipokea na kwamba muda sio mrefu atakwenda kufanya uchunguzi ili kujiridhisha, lakini pia wataalam wake watalazimika kwenda kupima umbali wa barabara hiyo ili kufanya hesabu na kujua nauli inapaswa kuwa kiasi gani.

"Hata madiwani wa Wilaya ya Siha, walishaleta kwangu malalamiko haya na tulishaongea nao. Kwa sasa nipo likizo, lakini muda sio mrefu atakuja mtu kupima umbali huo ili nauli iweze kupangwa na kusafiri bila wasiwasi," alieleza Makwale kwa njia ya simu.

# Makada wa CCM wapishana majimboni

**Na Mwandishi Wetu,** HAI

VIGOGO wa juu wa Chama cha Mapinduzi (CCM), akiwamo Katibu Mkuu, Dk. Bashiru Ally na viongozi wengine wa juu wa jumuiya za chama hicho, wameanza kupishana kwa kuingia na kutoka katika majimbo matano yanayoongozwa na wabunge sita wa vyama vya upinzani mkoani Kilimanjaro.

Watendaji hao ambao ni wajumbe wa vikao muhimu vya maamuzi kitaifa ndani ya CCM, kwa wiki ya pili sasa, wanafanya vikao vya ndani kuhamasisha uungwaji mkono katika uchaguzi ujao wa serikali za mitaa utakaofanyika Oktoba mwaka huu pamoja na kuweka mikakati ya kuhamasisha wananchi kujitokeza kwa wingi kushiriki uboreshaji wa daftari la kudumu la wapiga kura.

Viongozi hao ni Katibu Mkuu Dk. Bashiru Ally, ambaye amemaliza ziara yake juzi na baadaye kupishana njiani na Katibu Mkuu wa Jumuiya ya Umoja wa Vijana wa chama hicho taifa (UVCCM), Raymond Magwala, aliyekwenda moja kwa moja Jimbo la Hai kuanza kazi hiyo katika Wilaya ya Hai.

Majimbo ambayo CCM imeweka nguvu zaidi ni Jimbo la Hai, linaloongozwa na Mwenyekiti wa Taifa wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema) na Kiongozi wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, Freeman Mbowe na Jimbo la Moshi Mjini ambalo linashikiliwa na Japhari Michael (Chadema).


Mengine ni Jimbo la Vunjo ambalo Mbunge wake ni James Mbatia (NCCR-Mageuzi) ambaye pia ni Mwenyekiti wa Kituo cha Demokrasia Tanzania (TCD), Jimbo la Same Mashariki lililopo chini ya Mbunge Nangenjwa Kaboyoka (Chadema), ambaye pia ni Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali (PAC).

Vile vile, limo Jimbo la Moshi Vijijini linaloshikiliwa kwa sasa na Mbunge wa Chadema, Athony Komu.

Jana, Mwangala wakati anazungumza na viongozi mbalimbali wa chama hicho wilayani Hai, aliwataka wanachama wa CCM kushirikiana ili kupata ushindi, huku wakiweka lengo la namna ya kushinda uchaguzi ujao wa serikali za mitaa na uchaguzi mkuu utakaofanyika mwakani.

Alisema ushirikiano ni jambo muhimu, kwa kuwa hata timu ili kupata ushindi inahitaji kuwa na ushirikiano baina ya wachezaji na viongozi na kwamba amekuja ili kujiimarisha na kuhakikisha wanafanya vizuri kwenye uchaguzi wa serikali za mitaa.

"Ushirikiano ni muhimu na mnaposhindwa kufanya hivyo, matokeo yake ni kuumiza chama na kuwapa nguvu wapinzani," alisema Mwangala.







Bibi Zena Khamisi (89), mkazi wa Mtaa wa Karume Mji mdogo wa Kibaigwa, Wilaya ya Kongwa. mkoani Dodoma, akiandaa chakula cha mifugo nyumbani kwake jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Mimba za utotoni janga la taifa

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WAKATI Tanzania ikiungana na mataifa mengine duniani kuadhimisha siku ya Idadi ya watu, imeelezwa kuwa tatizo la mimba za utotoni bado ni kubwa nchini.

Kauli hiyo aliitoa juzi na Naibu Waziri Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi), Mwita Waitara, katika maadhimisho ya siku hiyo yaliyoenda sambamba na uzinduzi wa Ripoti ya Idadi ya watu Duniani, jijini hapa.

Alisema tatizo hilo ni kubwa kwa shule za msingi na sekondari kwa asilimia 29 na linachangiwa kwa kiasi kikubwa na mila na desturi, uendeshaji wa kesi kumtia mtu hatiani aliyempa mimba.

"Kuna mila na desturi ambazo watoto wa kike wakifikia umri fulani wanapewa chumba hivyo huko mtaani usiku kucha huwezi jua kinachoendelea, mazingira magumu ya usomaji.

"Namna ya uendeshaji kesi hizi mpaka kumtia mtu hatiani bado ni changamoto sana kwa kuwa wanaofanya vitendo hivyo wengine ni watu wa karibu na familia na wengine wanarubuni ndugu na kumalizana kimya kimya," alisema.

Pamoja na hayo alisema uelewa wa watoto bado ni mdogo huku mimba nyingi zinaripotiwa, lakini zinaishia hewani.

"Sisi kama serikali tutafanya vikao na wazazi mara kwa mara ili kuondokana na tatizo hili," alisema.

Kadhalika, alisema bado kuna changamoto ya vifo vitokanavyo na uzazi na kati ya vizazi hai 100,000 watu 556 huripotiwa kufariki dunia kwa sababu mbalimbali ikiwamo mimba za utotoni.

"Tanzania ni moja ya mataifa 179 yaliyokutana nchini Cairo na tulikubaliana kutekeleza mpango kazi tuliopanga katika mkutano huo wa idadi ya watu na maendeleo, Serikali ya Tanzania imetekeleza mambo mengi, ni wajibu wetu kushirikiana kumaliza vifo vinavyotokana na uzazi na mimba za utotoni ili kila kijana atimize ndoto zake," alisema.

Vile vile, alisema serikali imekuwa ikitekeleza mipango mbalimbali ya maendeleo na inalenga kufikia uchumi wa kati ifikapo mwaka 2025.

"Serikali itaendelea kushirikiana na Unfpa ili kuongeza upatikanaji wa huduma za afya ya uzazi ikiwamo uzazi wa mpango," alisema.

Awali, akisoma taarifa ya idadi ya watu duniani iliyotolewa na shirika hilo, Ofisa kutoka Unfpa, Samwel Msokwa, alisema kadiri watu wanavyoongezeka changamoto zinaongezeka na katika ripoti hiyo inaonyesha tatizo la mimba za utotoni duniani ambalo linaathiri mipango mbalimbali, vijana wengi wanahitaji kupata fursa, vifo vya wajawazito.

"Ripoti inaeleza kinaga ubaga kuwa kuna tatizo la ukatili wa kijinsia licha ya taasisi mbalimbali kufanyiwa kazi, tuelekeze nguvu kukabiliana na tatizo hili," alisema.

Naye, Mwakilishi wa Mkazi wa Umoja wa Mataifa (UN), Alvaro Rodriguez, alisema vifo vinavyotokana na uzazi bado ni changamoto hasa kwa wasichana wenye umri kati ya miaka 15-19.

# SNV yakutana na wadau wa maziwa kuboresha sera

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

SHIRIKA la Maendeleo la Uholanzi (SNV), limekutana na wadau wa tasnia ya maziwa, ili kupitia ripoti ya utafiti iliofanywa na shirika hilo kwa nchi mbalimbali, kwa lengo la kuboresha sera ya upatikanaji wa huduma muhimu kwa wafugaji na wasindikaji.

Pia SNV imekutana na wadau wa sekta hiyo ili kuhakikisha jitihada za serikali za utumiaji wa sheria ya blue print ambayo inalenga mfumo wa udhibiti wa utitiri wa tozo inatumika ipasavyo.

Akizungunza jijini Dodoma, Meneja mradi wa kuboresha sera na kuongeza uwajibikaji katika tasnia ya maziwa, Tom Ole Sikar, alisema wameamua kukutana na wadau hao ili kujadili changamoto zinazoikabili sekta hiyo hususani utitiri wa tozo ambazo nyingi zinajirudia na kusababisha sekta hiyo kushindwa kuhimili soko la ushindani.

Alisema pamoja na kuwa serikali imefikia hatua nzuri katika sheria ya blue print ambayo imeanza kutumika, wanahitaji kutilia mkazo ili watu wajue na kuielewa ikiwamo kuifanyia kazi.

"Tunahitaji kuona wadau wa sekta ya maziwa wanaelewa sheria ya blue print, wataalamu wa tasnia ya maziwa tumekutana tukawe mabalozi wa kuielewesha jamii," alisema Ole Sikar.

Alisema kwa mujibu wa utafiti waliofanya, kati ya tozo 31 zilizopo tozo 18 zinajirudia na kuongeza kupitia warsha hiyo itasaidia kwa kiasi kikubwa kukutana na serikali kuangalia jinsi gani ya kukabiliana na changamoto hiyo ikiwamo kutatua jambo ambalo litasaidia tasnia hiyo iweze kuhimili soko la ushindani la maziwa. Alisema wanaimani baada ya kujadili watakuwa na vigezo vizuri ambavyo watakavyowasilisha serikalini ili viweze kufanyiwa kazi kwa haraka na kuisaidia sekta hiyo kuinuka kiuchumi kama zilivyo nchi nyingine. Naye profesa Lusato Kurwijila, alisema imefika wakati sasa wadau wa maziwa na wasindikaji kubadilika ili waweze kuinuka kiuchumi kupitia sekta ya maziwa, ikiwamo kuinua uchumi wa taifa.

Prof. Kurwijila alisema majadiliano kupitia ripoti hiyo wakayafanyie kazi ili kusaidia wafugaji na wasindikaji kupata huduma muhimu katika suala zima la usindikaji wa maziwa.

"Tunatakiwa kusonga mbele katika uzalishaji wa maziwa baada ya kikao hiki, mikakati tulioiweka ifanyiwe kazi ili kuwasaidia wafugaji na wasindikaji," alisema Profesa Kurwijila.

Mkurugenzi Msaidizi wa Mazingira na Biashara kutoka Ofisi ya Waziri Mkuu, Christopher Mramba, alisema SNV na wadau wa maziwa wanapaswa kukaa pamoja kupanga nini kinachowakwamisha na kukiwasilisha serikalini kiweze kupatiwa ufumbuzi.

"Serikali inategemea majibu kutoka kwenu angalieni nini kinachotakiwa kuongezwa au kupunguzwa katika ripoti ya utafiti iliyofanywa na kuwaletea faida nyie na taifa kwa ujumla," alisema Mramba.

# Serikali yaipa kazi Tume ya Umwagiliaji

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

SERIKALI imeiagiza Tume ya Umwagiliaji nchini kuhakikisha inatumia weledi na utaalamu walio nao kuwasaidia wakulima katika umoja na vyama vya skimu za umwagiliaji zilizopo nchini ili kuwainua katika kilimo.

Pia, serikali imetoa wito kwa wakulima walio katika skimu za vyama vya umwagiliaji kuhakikisha wanakuwa na usimamizi madhubuti wa skimu hizo ili zilete tija kwa taifa.

Hayo yalisemwa jijini hapa na Mkurugenzi wa Mafunzo na Huduma za Ugani na Utafiti, Dk. Wilhelm Mafuru, kwa niaba ya Katibu Mkuu wa wizara hiyo wakati wa mkutano wa ushirikiano wa kiufundi wa kuwezesha uboreshaji maendeleo ya skimu za umwagiliaji chini ya Mpango wa Maendeleo ya Wilaya, awamu ya pili.

Alisema, lengo la mkutano huo ambao umezihusisha skimu nane kati ya 36 zilizoshindanishwa katika mashindano yaliyoandaliwa na wizara hiyo, ni kuhakikisha wakulima ambao ni wanachama wanashirikishana uzoefu na uendeshaji.

Alisema jambo kubwa lililopo ni kuwawezesha wakulima hao kupata ushauri kutoka kwa wataalam ambao wameandaliwa kwa ajili ya kutoa mada kwenye mkutano huo ikiwamo kuwajengea uzoefu katika uendeshaji wa kilimo.

Alifafanua kuwa wakati taifa linakumbana na mabadiliko ya tabia ya nchi ni lazima wao wajikite katika kilimo hicho cha umwagiliaji ili waweze kuwa na kilimo endelevu ambacho kitaleta uhakika wa mavuno, tija na kuongeza uzalishaji kwa wakulima hapa nchini.

"Kufanikisha hilo lazima Tume ya umwagiliaji ihakikishe inatekeleza kikamilifu usimamizi wa masuala ya umwagiliaji nchini, kwa kuwa hali ya umwagiliaji kwa sasa nchini iko vizuri," alisema Mafuru.

Kwa upande wa Katibu Mkuu mstaafu, wa wizara hiyo, Mbogo Mfutakamba, alisema hali ya uzalishaji nchini bado iko chini na inakabiliwa na changamoto ya uwekezaji katika miundombinu hususani ya uvunaji wa maji ya mvua, wataalam pamoja na utoaji wa mafunzo ya utumiaji wa teknolojia.

Alisema nchi ina miundombinu ambayo imejengwa, lakini bila kuwapo kwa mafunzo ya kina kwa watumiaji haitakuwa na tija yoyote kwa jamii na taifa kwa ujumla.

Alisema mafunzo hayo ya kujengeana uzoefu yakitolewa na wataalamu mara kwa mara yatasaidia kuongeza uzalishaji wa chakula hasa katika kipindi hicho cha mabadiliko ya tabia nchi.

"Kutokana na mvua nyingi zinazonyesha, kwa hiyo yakivunwa maji ya mvua na kuyahifadhi kipindi cha ukame wakulima hawawezi kupata shida kwasababu watatumia kilimo cha umwagiliaji," alisema.

Naye Mratibu wa mkutano huo, Anthony Nyarubamba, alisema awali walikutanisha skimu 36 za umwagiliaji nchini na baada ya mashindano hayo ni skimu nane pekee kutoka kanda nane ndio zilifuzu na kuibuka washindi na ndizo zimeitwa kwa ajili ya kupatiwa mafunzo.





# Ataka ushiriki jamii mapambano ya rushwa

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Haroun Ali Suleiman, amewataka viongozi wa serikali, taasisi binafsi na jamii kushirikiana katika mapambano dhidi ya rushwa na uhujumu uchumi.

Aliyasema hayo jana wakati akizungumza na waandishi wa habari kuhusu Maadhimisho ya Siku ya Mapambano dhidi ya Rushwa Afrika, ofisini kwake Mazizini, Unguja.

Alisema iwapo mapambano hayo yatashirikisha wadau wote, kuna matumaini makubwa ya mafanikio kupatikana.

"Wajibu wa kupambana na rushwa si wa serikali pekee bali ni jukumu la kila mmoja wetu wakiwamo wananchi," alisema.

Alisema licha ya Umoja wa Afrika kuamua kuadhimisha siku hiyo kila mwaka, bado kuna changamoto mbalimbali zinazokabili jitihada za mapambano dhidi ya rushwa na uhujumu uchumi Afrika ikiwamo Zanzibar.

Waziri Suleiman aliwatahadharisha viongozi wa ngazi mbalimbali ambao wanagombea nafasi za uongozi, kujiepusha kutoa rushwa na wananchi waache kupokea rushwa. Alisema uongozi haununuliwi wala haurubuniwi kwa kutoa hongo na kiongozi anaefanya hivyo hafai.

Alisema serikali inafanya jitihada kutoa elimu mjini, vijini, taasisi za serikali na maeneo ya shule za msingi na sekondari kupiga vita rushwa na uhujumu uchumi.

Kwa mujibu wa Waziri, kuanzia Januari hadi Juni, mwaka huu, Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi Zanzibar (Zaeca), imepokea malalamiko 110 na tuhuma zinaendelea kufanyiwa uchunguzi. Waziri huyo alisema tuhuma mbili zilifungwa baada ya kukosekana ushahidi na zingine ziko kwa ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka. Alisema Zanzibar inaungana na mataifa mengine ya Afrika kuadhimisha siku hiyo ambayo itasaidia kuongeza mwamko wa kupambana na changamoto katika vita dhidi ya rushwa.

Naye Mkurugenzi Mkuu wa zaeca, Mussa Haji Ali, aliizitaka taasisi za serikali na binafsi kuendeleza mapambano hayo.

Alisema mamlaka inafanya jitihada mbali mbali kusimamia sheria hiyo na kuhakikisha wananchi wanakuwa na uelewa juu ya rushwa.

Alisema Tanzania imeridhia mikataba wa Umoja wa Afrika ya kupambana na rushwa kupitia kanuni mbalimbali zinazotaka nchi wanachama kuimarisha utawala bora.



Wanafunzi wa kidato cha tano na sita wa shule ya St Anne Marie Academy, wakifurahia matokeo ya kidato cha sita na Mwalimu Mkuu wa shule hiyo, Gladius Ndyetabura, shuleni kwao, jijini Dar es Salaam juzi, baada ya shule hiyo, kufaulisha wanafunzi 19 kwa daraja la kwanza, 47 daraja la pili na 21 daraja la tatu. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wanaswa wakisajili simu bila kibali

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

MAMLAKA ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) ofisi ya Zanzibar kwa kushirikiana na Jeshi la Polisi imeendesha ukaguzi na kuwakamata mawakala wa mitandao ya simu za mkononi wanaoendesha shughuli hizo kinyume cha sheria za TCRA.

Msako huo uliofanyika eneo la darajani Mjini Unguja, lilisababisha zaidi ya mawakala 50 kukamatwa kwa kuendelea na shughuli zao kinyume cha sheria.

Mkuu wa TCRA Ofisi ya Zanzibar, Esuvatie Masinga, alisema lengo la msako huo ni kuwakagua mawakala na 'freelancer' wanaosajili laini kwa kufata sheria za TCRA.

Alisema mawakala wengi ni wa kujitolea na hawana vibali zikiwamo leseni, barua ya idhini kutoka mitandao husika, namba ya utambulisho wa mlipakodi (TIN) na ofisi jambo ambalo ni kinyume cha sheria za mamlaka hiyo.

"Utakuta mawakala hawana ofisi maalum badala yake wapo chini ya miavuli. Hawana hata barua za vibali kutoka mitandao husika ambayo wanasajili hizo laini, hili ni kosa wa mujibu wa sheria." alisema Alitoa onyo kwa mawakala wanaosajili laini kwa alama ya vidole kuacha kuwatoza wananchi pesa kwa kuwa kazi hiyo inafanywa bila malipo yoyote.

Naye Mhandisi wa TCRA Ofisi ya Zanzibar, Mtende Shirazi Hassan, alisema mawakala wengi wamekutwa na vitambulisho vya kampuni ya simu badala ya barua ya idhini kutoka kila kampuni anazosajili laini hizo .

Alisema mawakala wengi wanafanya kazi bila ya kuwa na leseni ya ofisi inayowataka kuendesha shughuli hizo kisheria.

Hata hivyo, alisema agizo la ukaguzi huo kwa 'freelancer' na mawakala limefanyika kwa utulivu licha ya baadhi ya wasajili laini na mawakala kufunga vibanda vyao na kukimbia.

Kwa upande wao, mawakala hao waliwashauri TCRA kutoa taarifa mapema juu ya mabadiliko yoyote yanayotokea ili wafuate sheria na kuepuka usumbufu.

# Wanawake na vijana kushirikishwa ajira

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MAKAMU wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Balozi Seif Ali Iddi, amesema katika kuhakikisha mazingira bora ya biashara yanaimarika, serikali itashirikiana kikamilifu na vijana, wanawake na makundi maalum ili kutengeneza ajira.

Balozi Iddi alisema hayo jana wakati akifunga Maonyesho ya 43 ya Biashara ya kimataifa katika ukumbi wa Rashid Mfaume Kawawa ndani ya Uwanja wa Maonyesho wa Mwalimu Julius. K. Nyerere.

Alisema matengenezo hayo ya fursa za ajira yanaweza kusaidia kupunguza kwa kiasi kikubwa umaskini wa kipato, hususan kwa watu wenye mazingira magumu hasa sehemu za vijijini.

Alisema ushirikiano huo unathibitishwa na hatua zinazoendelea kuchukuliwa na serikali katika kuandaa mpango wa kuimarisha mazingira ya biashara kupitia andiko la 'blue print' ambalo utekelezaji wake umeshaanza rasmi kutumika.

Balozi Seif alisema kabla ya kuanza kwa utaratibu huo serikali ya Muungano imeshaanza utekelezaji wa mpango kazi huo kwa kuondoa tozo nyingi katika sekta za kilimo, madini na viwanda.

Alisema hatua zinazochukuliwa za kuendeleza mazao ya ndani yanayoshughulikiwa na wakulima wenyewe kupitia wataalamu wazalendo yamepelekea kuhamasisha wananchi kujenga tabia ya kupenda kutumia bidhaa zinazozalishwa na viwanda nchini.

Alisema mfumo huo una nia na lengo la kutumia vyema soko la ndani ambalo ni kubwa lakini wakati huo huo kuongeza ajira kutokana na uzalishaji wa bidhaa ambazo nyingi huzalishwa na viwanda vidogo na vya kati na kupunguza tatizo la ajira.

Balozi Iddi aliwahakikishia washirika wa sekta ya biashara ndani na nje ya nchi kwamba serikali daima iko pamoja nao katika kuhakikisha sekta ya biashara na viwanda nchini inakuwa kwa kasi na kuwa kichocheo kikubwa cha kuchangia ukuaji wa uchumi, ajira na kupanua wigo wa kodi.

Aliushukuru uongozi wa Mamlaka ya Maendeleo ya Biashara Tanzania (Tantrade) kwa jitihada za kuziendeleza bidhaa za viungo, chumvi, mwani na dagaa zinazozalishwa Zanzibar kwa kuongeza thamani ya mazao hayo, hivyo kuyawezesha kushindana katika masoko ya ndani na nje ya Zanzibar.

Naye Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi ya Tantrade, Dk. Ng'wanza Kamata, aliwapongeza washiriki wote kwa uthubutu wao uliofanikisha maonyesho ya mwaka huu kuwa bora zaidi ikilinganishwa na yale ya mwaka uliopita.

Aliwahakikishia kuwa bodi na serikali iko pamoja nao katika kuweka mazingira bora na rafiki ya ufanyaji biashara nchini ili kuwezesha sekta ya biashara na viwanda kukua, kuvutia wawekezaji na hatimae kuchangia katika uchumi wa taifa.



**KISWAHILI CHA BEYONCE CHAWA LULU** Soma UK.20

Nipashe
MWANGA WA JAMII
BT

JUMAMOSI JULAI 13, 2019



# KWELI KAACHIKA Shilole amwambia Shamsa asing'ang'ane

## BASI SAWA



## Bad Key kutambulisha 'Mvuvi' hivi karibuni

MSANII anayechipukia katika muziki wa Bongofleva kupitia lebo ya PMM, Bad Key, amesema kuwa yupo katika maandalizi ya kuachia ngoma yake mpya hivi karibuni.

Akizungumza na BT, Bad Key amesema ngoma hiyo inayoitwa 'Mvuvi' itatambulishwa siku chache zijazo baada uongozi wake kukamilisha kazi ya kuupitia.

"Nimepania kufikia levo zingine katika ujio wangu, nimejipanga kuja kivingine kabisa kwa kuwa soko la muziki linazidi kupanuka kimataifa,"alisema Bad Key .



## Jack anapoipa tano tamthilia ya Huba

MWIGIZAJI wa filamu, Jackson Kabirigi 'Jack', amesema tamthilia ya Huba imemfanya kutambulika zaidi ndani na nje ya nchi.

Kabirigi ambaye amecheza sehemu tufauti katika tamthilia hiyo, amesema michezo ya aina hiyo inalipa zaidi na kumfanya msanii kujulikana na watu wengi.

"Nimeanza kushiriki tamthilia hiyo baada ya kukaa kimywa kwa muda mrefu, ninachoshukuru kuwa jina langu limekua zaidi baada ya kuigiza katika tamthilia hii," amefunguka Jack.



# Shilole amwambia Shamsa asing'ang'ane

MWIGIZAJI na mwimbaji wa Bogofleva, Shilole amethibitisha kwamba msanii mwenzake Shamsa Ford na mume wake Chid Mapenzi wameachana.

Kauli ya wanandoa hao wameachana ameitoa wakati wasanii hao wawili walipokutana juzi usiku.

Shilole alikaririwa akisema Shamsa alikuwa wifi yake kwa Chid, lakini pia ni rafiki yake wa siku nyingi.

"Shamsa alikuwa wifi yangu kwa Chid, siwezi kusema ang'ang;ane hata kama ameshindwa. Mimi namuheshimu kutokana na urafiki wetu wa siku nyingi ambaye alinishawishi kuingia katika muziki," amesema Shilole.

## INSTA-TWITTER





Mtoto anatamani baba afe ili arithi nyumba. Baba atamani mtoto afe ili apangishe chumba -**Roma Mkatoliki.**



**Mpambanaji** hafi bali anazimia tu.Tusichoke kupambana -**Shamsa Ford.**



# Tundaman kumbe hakai meza moja na Matonya

MKONGWE wa muziki wa Bongo Fleva Tundaman, amesema majisifu ya Matonya yamemfanya kuwa mbali naye.

Akihojiwa katika kipindi cha Planet Bongo ya East Africa Radio, Tundaman amesema kitendo cha matonya kujisifu anamuiga sauti yake kimemfedhehesha na ndio maana hana ukaribu naye.

"Wakati nakutana na Matonya alikuwa na ngoma mbili tu, baada ya kukutana na mimi ndio nikampa madini ya tone ya sauti yangu, yeye ndio ananiiga mimi sauti. Nakumbuka kipindi kile alikuwa anakaa Kariakoo akawa mshikaji wangu sana, tulitaka kuanzisha kundi na nilimmezesha ngoma nyingi na nilimuandikia ngoma, ana material yangu mengi". Amesema Tundamna.

>>> **Usikose Jarida hili la Burudani Tele (BT) ndani ya Gazeti lako la Nipashe kila Jumamosi, pia lipo kwenye mtandao wa kijamii Twitter, tu' follow**

**@burudanitele**

## UNASEMAAA...

# Adam umekuna upele, wacha wahangaike nalo

MUANDAAJI na muongozaji mkongwe wa video za muziki na filamu hapa Tanzania, Adam Juma, amefunguka sababu hasa za tasnia ya filamu kudumaa kwa muda mrefu.

Akizungumza hivi karibuni, Adam amesema licha ya wasanii wengi wachanga kufanya kazi nzuri kuliko wale wakongwe, bado wanashindwa kufika mbali kutokana na Watanzania kuchoshwa na maudhui kuwa ni yaleyale.

Amesema kuwa Watanzania wengi wana tabia ya kunyanyapaa kazi za wasanii ambao hawana ubunifu.



## BODA 2 BODA

# Fresh Jumbe ainogesha 'Nanawa Mikono' ya Phantom



KUNDI la 'Zing Zong' la Phantom Musica International wameibuka tena na wimbo wao wa tatu unaoitwa 'Nanawa Mikono' ambapo katika safu ya waimbaji kuna sauti ya mwimbaji nguri Freshi Jumbe Mkuu.

Jumbe ambaye kwasasa anaishi nchini Japan katika jiji la Tokyo, ameshiriki katika wimbo huo na ndiye aliyeinogesha kiufundi kufanya kibao hicho kuwa na ubora wa kimataifa.

Wimbo huu 'Nana Mikono ni kazi ya tatu kwa kundi hilo la Phantom Musica International, ambao awali walikuja na 'Sononeko la Huba' na kisha 'Sekidobwa' ambazo zote zimeacha gumzo katika anga la muziki wa dansi ndani na nje ya Tanzania.

Mkurugenzi Mtendaji wa bendi ya Phantom Musica International, Abdulfareed Hussein, amesema kuwa, Fresh Jumbe ameshiriki katika wimbo huo mpya ambao umeanza kusikika katika vituo mbalimbali vya radio nchini na kupitia mitandao ya kijamii.

## INSTA-TWITTER

Tuffolow/ Tu-tag **@burudanitele**



**Maisha** hayahitaji mashaka wala woga, zaidi ya kupambana. Tunaishi na tunapita **- Ibrahim Ajibu.**



**Mwanamke** jikwamue. Usikubali kupitwa na mambo mazuri jamani! Kina mama tujipange mapema. Mbinu pekee ya wewe kujikwamua ni hii hapa. Ujasiriamani. Unachokitamani maishani unakijua wewe. Hamu ya mafanikio unaijua wewe. Kumbuka mbuyu ulianza kama mchicha, unachohitaji ni maarifa tu **- Aunt Ezekiel.**



**Eti** Mimi si nilikukataza usimsikilize Mbosso mrongo yule. Wanawake wa Mombasa bwana **- Mbosso.**

# Kuumbe!



## VICHUPI STOP! Nick Minaj agoma kutumbuiza

SI mara ya kwanza wasanii wa Marekani na Ulaya kushindwa kutumbuiza katika matamasha ya burudani yanayoandaliwa nchini Saudia Arabia.

Pamoja na nchi hiyo kulegeza baadhi ya sheria, bado imekuwa vigumu kwa wasanii kutoa burudani kutokana na kushindwa kutimiza masharti ya sheria za nchi hiyo inayoegemea sheria za Kiislam.

Hivi karibuni, rapa maarufu Nicki Minaj, amekumbana na hali hiyo  na amelazimika kuvunja tamasha lake nchini humo  huku akitoa sababu ya anaunga mkono haki za wanawake na wapenzi wa jinsia moja.

Taarifa za nyota huyo wa miondoko ya rap kutumbuiza Saudia ziliwashtua wengi na kusababisha kelele kali kutoka kwa wanaharakati wanaokosoa rekodi ya haki za binadamu ya nchi hiyo.

Wengine walijiuliza msanii huyo atavaaje kwenye tamasha hilo kwa kuwa nchi hiyo inafuata mfumo wa kihafidhina wa Kiislamu, na Minaj ni maarufu kwa kuvaa nguo za nusu uchi.

Kwa mujibu wa shirika la habari la BBC, ukoselewaji wa Saudia kwenye eneo la haki za binadamu uliongezeka zaidi baada ya mauaji ya mwanahabari Jamal Khashoggi katika ubalozi mdogo wa Saudia jijini Istanbul, Uturuki mwezi Oktoba mwaka jana.

Mwezi Machi mwaka huu, nchi hiyo ikaingia lawamani zaidi baada ya kuwafungulia mashtaka wanawake 10 ambao ni wanaharakati wa haki za binaadamu.

"Baada ya kufikiria kwa kina, nimeamua kutoendelea na tamasha langu jijini Jeddah," mwanamuziki huyo amesema kwenye taarifa yake.

"Japo ninapenda kwelikweli kutumbuiza mbele ya mashabiki zangu nchini Saudia, lakini baada ya kujipatia elimu zaidi kwa masuala kadhaa, naamini ni muhimu kwangu kuweka wazi kuwa naunga mkono haki za wanawake, wapenzi wa jinsia moja na uhuru wa kujieleza."

Ijumaa iliyopita, Taasisi ya Haki za Binadamu yenye maskani yake nchini Marekani ilimuandikia barua ya wazi Minaj ikimtaka aachane na tamasha hilo la Julai 18.

Walimuomba nyota huyo "akatae pesa za utawala (wa nchi hiyo)" na kutumia ushawishi wake kushinikiza kuachiliwa huru kwa wanaharakati wanawake waliokamatwa.

Mapema mwaka huu, mwanamuziki Mariah Carey aliyapa kisogo maombi ya wanaharakati kuacha kutumbuiza nchini humo huku Disemba mwaka jana mwanamuziki Nelly alikosolewa vikali kwa kutumbuiza kwenye tamasha la wanaume pekee nchini humo.





## Wakikusuta lazima utoe chozi

ASHA BOKO

Na Adam Fungamwango

KWENYE filamu za Kibongo kuna wasanii wa aina tofauti na vipaji mbalimbali. Si kila msanii ana kipaji cha kuigiza sehemu ile ile, ingawa inapaswa msanii kuwa na uwezo wa kuigiza sehemu zote unazopangiwa.

Lakini baadhi ya wasanii  wana umahiri wa wa kipekee kuigiza sehemu fulani kiasi cha watazamaji kudhani ndiyo tabia yake halisi. Kwenye ukali akikaa mwigizaji kama Mohamed Fungafunga, maarufu kama Mzee Jengua basi utapenda.

Kwa siku za karibuni kuna aina fulani za filamu hasa za maisha ya uswahilini zikionekana kutamba, huku  mashabiki wengi ambao ndiko wanapoishi wamekuwa wakizifuatilia kwa karibu.

Baadhi ya wasanii wake wanaigiza kama kinadada au kinamama ambao wana maneno ya shombo, nyodo na kuwa na tabia ya kwenda kuwazodoa au kuwasuta wenzao kwa sababu mbalimbali zinazohusu maisha ya uswazi.

Kwenye filamu za Kibongo ikishafika sehemu kama hiyo ya kuzodoana, kusutana wapo wasanii wenye uwezo mkubwa wa kazi hiyo.



RIYAMA

### RIYAMA ALLY

Ni msanii wa kike mwenye kipaji cha hali ya juu ya uigizaji. Ana uwezo wa kuigiza sehemu nyingi zinazotakiwa. Lakini kwa miaka ya hivi karibuni ameonekana kuwa ni mahiri sana kuigiza sehemu za kuzodoana, kusutana kutokana na kuwa na maneno mengi ya shombo, kejeli, nyodo, mizaha, akizipangilia kwenye nahau, misemo, methali na kila aina ya neno ambalo ataona litamuudhi au kumkera mgomvi wake.

Mtu kama huyu akija nyumbani kwako akiwa amekodishwa na mtu uliyegombana naye ni lazima utimue mbio kwa sababu hata ukijifungia mlango, akibaki nje na kukupa vipande vyako, unaweza kulia.

### CHUMA SULEINAM 'BI HINDU'

Bibi huyu siyo kama anaigiza. Ni kweli ana uwezo mkubwa ya kuongea. Ukiachilia mbali kuigiza amekuwa akionekana akihojiwa na wanahabari kwenye mambo mengine ya kijamii, ikiwamo kuhusu klabu yake ya Simba. Hata huko ameonekana yuko vile vile. Akiongea kawaida ni kama anaigiza na akiigiza anaonekana kama anaongea kawaida. Ni mama aliyejaaliwa maneno mengi, hasa ya Kipwani, kutokana na kuwa ni mzaliwa na jiji la Dar es Salaaam. Unaweza kusema kuwa ni mama wa mjini.  Sina haja ya kumueleza sana kwani watazamaji wa filamu wanalifahamu timbwili lake. Ukimchokoza huyu ujue umelikoroga. Hutopigwa makofi, lakini maneno yake yanaweza kukufanya uwe kama umepigwa.

Kama umemchokoza akija nyumbani kwako, ondoka kabisa na kwa bahati mbaya awe ameongozana na Riyama, mjomba shughuli unayo.



SHAMSA FORD

### TAUSI MDEGELA

Awali alionekana kama msanii wa kawaida tu, lakini kadri siku zilivyozidi kusonga mbele ameonekana kuwa ni mmoja kati ya wasanii wenye uwezo mkubwa ya kuongea na kuwapa makavu laivu wenzake kwenye filamu.

Mbishi na mwenye uwezo mkubwa wa kuzungumza na maneno ya shombo juu. Huyu ni Tausi Mdegela, msanii mwenye muonekano wa kipekee, lakini pia ni kipenzi cha watoto mitaani.

Naye anawekwa kwenye orodha ya wasanii kwenye uwezo mkubwa wa maneno ya shombo.

Huyu naye akiamua kuja nyumbani kwako kama umemchokoza, anakudai, au amekodishwa anaweza kukufungia mtaa, kimbia.

### ASHA BOKO

Ni maarufu sana kwenye filamu za ucheshi. Ni mwoga wa kupigwa, lakini mdomoni yuko vizuri.

Ni mmoja wa waigizaji mwenye uwezo wa hali ya juu wa kike nchini na hasa zile za kusemana, kucharurana na kusutana.

Naye yumo kwenye orodha hii, na kama akija nyumbani kwako kukusuta, dawa yake ni moja, tishia kumpiga, ila kama akija na Tausi, Riyama, na Bi Hindu, funga mlango timua mbio ndugu yangu, hutowaweza.

### SHAMSA FORD

Sikutegemea kama naye yumo. Ni mmoja wa wasanii maarufu wa kike nchini Tanzania mwenye uwezo mkubwa wa kuigiza. Lakini hakuna aliyejua kuwa naye ana uwezo wa kuigiza kama mwanadada wa uswahilini. Filamu chache alizoigiza mambo ya uswazi, zimesababisha wengi kugundua kipaji chake kingine cha kuweza kuongea na kuwa na tabia zile zile za huko.

Sasa fikiria, kama wote hawa, Riyama, Bi. Hindu, Boko, Tausi na Riyama wanakuja nyumbani kwako kwa kazi moja tu ya kukusuta. Siku hiyo hapatoshi. Upo nyonyo?

# Vijimambo

PICHA ILIYOPITA



1. Wanasema eti mimi chizi. Watanzania bwana kwa figisu! - Majuto Magazeti, Miyomboni Iringa.
2. Duuh! Jamani kazi kwanza, kuselifika baadae - Bahati, Kiwalani DSM.
3. Hii mitandao ya kijamii inatutesa. Kwa hii selfii kila mtu atakomenti 'nice' - Agatha Mbale, Moro Town.
4. Natafuta picha ya kutupia 'whatsap' - Dullah Dimoso, Tabata DSM.
5. Kijana hiyo simu imepitwa na wakati, ipeleke makumbusho - Oiso, Nyaishozi Tegeta DSM.
6. Ukisikia uchizi taslimu, basi ndio huo. Simu ya mezani na selfii! - Mama Nah, Manzese DSM.
7. Watu watajua najipiga selfii, watati mie namtoa mende kwenye simu - Dully, Kiembesamaki Zenji.
8. Yes, hapa sasa pozi limekubali, ngoja nijifotoe sasa - Samwel Sungi, Utemini Singida.
9. Hii simu vipi, mbona sioni sehemu ya kujiselfisha? - Msabaha J. Msabaha, Mikindani Mtwara.
10. Lazima baby wangu aikubali hii picha, si selfii ya kitoto - Beneali Moussa Beneali, Migombani Zenji.
11. Hii inaitwa 'ekotite', muulizeni Kofi Olomide anaifahamu sana - Rehema Jumbe, Kwanjeka Tanga.
12. Kweli ushamba mzigo. Wewe, sio kila simu unaweza kujiselfisha nayo - Mariam Beneali, Migombani Zenji.
13. Ha ha haaa, usitake ncheke mie! Hebu rudisha simu ya watu ofisini - Moussa Beneali, Migombani Zenji.
14. Hapo 'chacha'! Disco limeingia watu wa kabila lileee! Mtajuta kuijua selfii - Rehema Jumbe, Kwanjeka Tanga.
15. Mnashangaa nini? Mie sijiselfishi kama nyie, mie fundi simu jamani - Dully, Kiembesamaki Zenji.
16. Ukitaka kugombana naye, mwambie kuwa hiyo simu haiselfishi - Antar, Makumbusho Kijitonyama DSM.
17. Hapa sasa mademu wote wa 'bush stars' wangu - Nahoja Mazengo, Mbande Chamazi DSM.
18. Wewe! Hebu acha ushamba wako bwana, unawaabisha Wairinga wenzip - Jimmy Mwaipiana, Keko Bora DSM.
19. Hiyo selfii yako inanitia homa kwa kicheko - Bimkubwa Ausi Juma, Michenzani Unguja.
20. Hilo ndio tatizo la Wahehe wakishaingia mjini - Jimmy Mwaipiana, Keko Bora DSM.
21. Kaa hivyo hivyo, baada ya 'masaa' kadhaa utaona sehemu ya kupigia picha inajionyesha - Judi, Mbezi Mwisho DSM.
22. Watu wa kizazi hiki, kweli wamedata. Haya bhana na selfii yako bandia - Mama Nah, Manzese DSM.
23. Kweli ushamba zigo la miba. Tangulini simu hiyo ikatumika kwa selifii? - Judi, Mbezi Mwisho DSM.
24. Hiyo ni sawa na kuosha mchele kwenye mto wa maji mengi. Utapata taabu sana - Semeni Mpanjira, Kilwa.

**SMS Bomba ya Leo:**
**Watu watajua najipiga selfii, watati mie namtoa mende kwenye simu - Dully, Kiembesamaki Zenji.**

PICHA MPYA



TUMA MESEJI - 0773 477 311




# Siri ya Usia: Warithi wasio na urithi

**Na Adam Fungamwango**

FILAMU hii inaitwa 'Siri ya Usia'. Mtunzi alitaka kuonyesha jinsi baadhi ya familia kwenye jamii zilivyobeba siri kubwa zilizojificha.

Pia tamaa na ujuaji mwingi unaweza kumletea mtu matatizo na kujikuta akikosa hata kile kidogo ambacho alikuwa akipate.

Imechezwa na wasanii maarufu kama Esha Buheti, Eddy Ally, Said Majumba, Mzee Chillo, Mzee Jengua, Flora Mvungi, Nasra Said, Mohamed Mtei, Ahmed Julius, Furaha Rashid na wengineo.

Inaanza kwa kuwaonyesha watoto wa marehemu mzee Chillo. Hao ni Eddy, Esha na Majumba.

Wanaanza maisha mapya baada ya wazazi wao kufariki. Hawana shida kwani wazazi wao wamewaachia mali, ambavyo ni majumba na mashamba.

Kati ya watoto hao, Eddy ambaye ni mtoto wa mwisho anaonekana kuwa ni mtukutu na mkorofi kuliko wenzake.

Akaanza kulazimisha mali za baba yao ziuzwe wagawane ili kila mmoja afe na chake. Ndugu zake walipinga hilo na kila mbinu na hila ya ndugu yao kutaka kufanya hivyo ziligonga mwamba.

Baada ya mbinu zake kushindikana, Eddy alibadili mbinu na sasa akatishia kuchoma nyumba moto.

Mbinu hii ilisaidia kwani ndugu zake walilegeza masharti kwa kumkubalia kuuza shamba moja.

Pesa aliyeipata aliitumia kwenye starehe. Kujirusha kwenye mabaa, akitumia na mrembo mmoja matata, Flora Mvungi. Kama kawaida ya warembo wengi wa mjini, lengo la si mapenzi, bali wapo kimaslahi zaidi.

Hivyo anafanya mipango na kumuibia pesa zake zote, na hilo linafanikiwa.

Baada ya kuibiwa, Eddy anaishi maisha ya kubangaiza na kuona aibu kurudi nyumbani kwa ndugu zake.

Hilo linamfanya akamatwe na polisi na kuunganishwa kwenye kesi ya wizi.

Kaka yake Majumba anasikia taarifa hiyo, anaamua kwenda kumuwekea dhamana.

Anamrudisha nyumbani ili waishi kama zamani na yale yote yaliyopita zamani wayasamehe.

Siri inakuja kufichuka baada ya miaka mingi kuwa kumbe Majumba aliyehesabiwa kama mtoto wa kwanza wa mzee Chillo hakuwa mtoto wa kumzaa, bali mke wa mzee Chillo alimuokota porini kabla watoto wao halisi Esha na Eddy hawajazaliwa.

Kusikia hivyo, Eddy kwa sababu alitawaliwa na roho mbaya, tamaa ya mali, akili zikamruka na kuamua kumfukuza nyumbani kwao.

Kibaya zaidi akamwambia aondoke kwani hahusiki na chochote mle ndani kwa sababu kumbe aliokotwa tu. Majumba yeye akakataa na kusema yeye hana kwao, zaidi ya hapo.

Ugomvi unakuwa mkubwa, Eddy anaamua kuchukua kisu na kumchoma Majumba. Kumbe Majumba anajua kila kitu kuhusu ile mali kwa sababu mze Chillo alimwambia kabla hajafa.

Akiwa kwenye hali mbaya, Majumba aliwaambia ndugu zake Esha na Eddy kuwa vyote alivyofanya ni upendo tu kwa ndugu zake, vinginevyo yeye ndiye ambaye angewatimua na kila kitu angerithi peke yake.

Alikuwa na ushahidi wa hati ya mali zote. Majumba akawaambia kuwa ni kweli aliokotwa porini, hata hivyo kwenye nguo alizokuwa amefunikwa kulikuwa na vipande vya dhahabu vilivyowekwa na mtu aliyemtupa.



FEDHA CHEKWAA

# Mastaa hawa usiwaguse kwa noti

WIKI hii Dunia imezidi kushangazwa baada ya jarida maarufu la Forbes kutangaza majina 20 ya mastaa walioingiza mkwanja mrefu kupitia kazi zao wanazozifanya.

Swift ameonekana kuwapiku mastaa hao kutokana na juhudi zake za kutafuta pesa na kufanikiwa kuingiza kiasi cha dola milioni 185.

Swift ambaye ni mwanamuziki na mjasiriamali, ameonekana kushindana na mtoto wa familia maarufu nchini Marekani ya Kardashian, Kylie Jenner ambaye amejikusanyia dola milioni 170.

Rapa mkali na aliyeoa katika familia hiyo, Kanye West yeye ameshika nafasi ya tatu kwa kuwa na ukwasi wa doma milioni $150. Kanye amemuoa dada wa Kyle, Kim Kardashian na kufanikiwa kupata naye watoto wanne.

Kwenye orodha hiyo, Rapper P. Diddy na Jay- Z hawapo kwenye Top 10 badala yake wameshika nafasi ya 28 na 20 kwenye Top 30.

Kwa upande wa michezo, Lionel Messi anayekipiga kunako klabu ya Barcelona ndiye mchezaji wa kwanza duniani, aliyeingiza mkwanja mrefu kwa mwaka 2019 ameingiza USD $127 na kushika namba 4 kwenye orodha hiyo ya Forbes.

Orodha hiyo imeangalia vigezo vya mishahara, Dili za matangazo na biashara wanazofanya mastaa hao.

# Card B kwani Dupri kasema uongo?



RAPA Cardi B ameonekana kukerwa na kauli aliyoitoa mkongwe wa muziki wa Hip Hop Jermaine Dupri baada ya kusema kuwa kwa sasa hakuna rapa bora wa kike kutokana na wao kuimba kitu kimoja.

Dupri aliendа mbali na kusema hata kwenye masuala ya video wote wanakuja na stori moja ya wao kuonekana wakiwa club wanachotakiwa kufanya ni kuimba kuhusu vitu tofauti na mtu mmoja ajitoe ili kuleta ladha tofauti kwenye muziki wa Hip Hop nchini Marekani.

Cardi B alimjibu Dupri kwa kusema kwamnba yeye binafsi huwa ana-rap kuhusu vitu ambavyo havina maana kwa sababu jamii ndio inapenda vitu visivyo na maana. Pia alizidi kumchana Dupri akisema wakongwe hao hawatoi ushirikiano kwa wasanii wachanga.



## Kiswahili cha Beyonce chawa lulu

KIBAO cha mwanamuziki wa Marekani, Beyonce, ambacho kina vionjo vya lugha ya Kiswahili, kimeonekana kuwapagawisha mashabiki wengi wa muziki wa Afrika Mashariki.

Beyonce alitambulisha wimbo huo 'Spirit' ukiwa na baadhi ya maneno ya Kiswahili.

Wimbo huo unaanza kwa sauti nyororo "Uishi kwa muda mrefu mfalme," na kisha kufuatiwa na sauti nzito inaitika "uishi kwa", kabla ya mwanamuziki huyo kuanza kumwaga mashahiri yake kwa Kingereza.

Kibao hicho kiitwacho Spirit ni sehemu ya albamu inayosindikiza filamu mpya ya Lion King inayotengenezwa na kampuni kubwa ya Disney ya nchini Marekani.

## We 9ice unataka kuwatoa roho wenzio?

MWANAMUZIKI wa Nigeria. 9ice, ameingia katika utata baada ya kutamka kwamba akimuona mbakaji anamuua kwa mikono yake.

Akitumia ukurasa wake wa Instagram, 9ice aliandika ujumbe ambao unaeleza kama akimuona mwanaume mbakaji basi atamuulia mbali na kwamba hajali kushtakiwa kwa mauaji.

Kulingana na maoni yake kwamba mwanaume wa aina hiyo hafai kuishi kwani kuna njia mbalimbali za kukabiliana na mihemuko na si kwenda kumbaka mwanamke.





## Wendy kweli umenogewa na 'serengeti boy'

MSANII anayetamba kwenye mitandao ya kijamii, Wendy Williams, ameamua kuweka wazi mahusiano yake ya kimapenzi na kijana wa miaka 27, akisema ana nguvu ya kimahaba bila kujali miaka umri wake.

Akizungumza wakati akiendesha kipinndi chake cha TV,

Wendy alimwambia msichana mmoja aliyeshiriki kipindi hicho kwamba ni kweli vijana wanapendeza lakini linapokuja suala la mahusiano anaweza kumpenda mtu fulani, hata akiwa na umri wa miaka 50.

## Makofi kwa jaji... Franklin, Lilian nyie rudini tu

JAJI anayesikiliza kesi ya talaka kati ya mwanamuziki Ubi Franklin na mkewe Lilian Esoro, amewataka wenza hao kurudi nyumbani kwa ajili ya mashauriano kufikiria upya hatma ya ndoa yao.

Kumekuwa na mabadiliko ya kuvutia katika kesi hiyo jambo ambalo Jaji ameamua kuondoa kesi hiyo na kuwataka wanandoa hao kuwalea kwa pamoja watoto wao wachanga

Kulingana na blogger, SDK, jaji huyo wa Mahakama Kuu ya Ikeja, aliamua kwamba talaka yao ni batili tangu Lilian alipothibitisha kuwa Ubi hutoa matunzo kwa toto wao na bado ni marafiki mzuri sana.





Na John Juma
0716217615

## Mionzi ya Sheria

# Miongozo kisheria ukopaji wa rehani -1

MASUALA ya kuweka mali rehani ili kupata mkopo, nchini Tanzania, yanaongozwa na sheria kuu mbili nazo ni Sheria namba 4 ya Ardhi ya mwaka 1999 sura ya 113,pamoja na sheria namba 17 ya rehani ya mwaka 2008.

Sheria hizo zimetajwa haki nyingi za mtoa mkopo; sambamba na zile za mchukua mkopo huo, la msingi shuruti (wajibu) kwa upande wa mtoaji mkopo huo.

Kwa mujibu wa maelekezo ya Sheria ya Rehani Tanzania ya mwaka 2008, baadhi ya wajibu na masuala muhimu walionao watoa mkopo ni pamoja na kuhakikisha kuwa anafanya utafiti na kujua iwapo mtu anayechukua mkopo ana mke au ana mume, kulingana na jinsia ya mkopaji.

Hii ni kwa sababu kwa mujibu wa sheria elekezi ikiwa nyumba au kiwanja kilichowekwa au kitakachowekwa rehani ili kupata mkopo ni cha familia kwa maana hiyo hao ni wanandoa.

Hivyo basi ni lazima wote wawili (mume na mke) kwa pamoja wawe wameridhia na kusaini waraka maalum unaothibitisha au utakaothibitisha ridhaa zao.

Mathalani, endapo basi taasisi ya mkopo haikufanya utafiti na kujiridhisha kwanza; itakuwa ni uzembe kwa upande wao. Katu, hairuhusiwi kwa mwanandoa mmoja kutumia mali ya familia (nyumba, shamba na kiwanja na hata gari kama dhamana bila pasipokuwa na ridhaa ya mwanandoa mwenzake; mke au mume.

Ni wajibu kwa mtoa mkopo ni kuhakikisha mali inayowekwa kwake kama rehani haijawekwa rehani sehemu nyingine yoyote, haina mgogoro wowote katika mahakama na katika vyombo vya sheria, haina au haijawekewa zuio lolote lile (caveat), na wala siyo ardhi ambayo iko katika mpango fulani wa serikali ambao, kwa njia moja au nyingine, utatekelezwa muda mfupi kabla ya deni kuisha au hapo baadaye kidogo.

Hii yenyewe, husaidia , kumuepusha mtoa mkopo kutoingia katika mgogoro au kadhia na mamlaka nyingine hasa za serikali au watu binafsi ambao wanaweza kuwa na maslahi, moja kwa moja, katika ile ardhi kabla yake.

Halikadhalika, wajibu mwingine muhimu, kwa upande wa mtoa mkopo, ni kuhakikisha wanamfahamu mwenye shamba na kumweleza bayana ukweli mteja wao kuhusu huo mkopo; ikiwa ni pamoja na athari zake atakaposhindwa kulipa deni.

Afahamishwe taratibu za marejesho, uhuru wa kuongeza mkopo na ukomo, na kila kitu ambacho ni sehemu ya muamala wa mkopo.

**ULINZI WA MKOPAJI**

Endapo kutakuwa au kutatokea badiliko lolote kufuatia taratibu za ulipaji deni la mkopo, riba yake au mabadiliko yoyote katika tarehe ya marejesho ni haki ya mchukua mkopo kujulishwa kwa maandishi na taarifa rasmi zifikishwe kwake.

Taasisi kubwa za fedha (mabenki) zimekuwa zikilifanya jambo hili hili tofauti kabisa na baadhi ya taasisi ndogo hasa za kuweka na kukopa (Saccos na vikoba) ambazo siku hizi, zenyewe, ndiyo zinazohudumia wateja wengi wa kipato cha chini na kati na hata cha wastani. Kwenda kinyume ni ukiukwaji mkubwa wa haki za wateja wao.

Muhimu, tena, kufahamu kuwa mali iliyowekwa au kutolewa kama rehani ni ardhi. Itaendelea kuwa haki ya mchukua mkopo; na ikiwa tayari mnada ulikwisha fanyika, mhusika aliyenunua/atakayenunua ardhi tajwa endapo hakumaliza au hajakamilisha fedha ya ununuzi yote kwa mujibu wa makubaliano. Umiliki bado, utaendelea kuwa wa mchukua mkopo mteja.

Na tena, kama haitoshi, muda au wakati wowote katika kipindi ambacho mnunuzi bado hajamaliza manunuzi ya ardhi hiyo nafasi ya yeye kukomboa mali yake itaendelea kuwa wazi.

Mfano amelipa au atalipa asilimia 25 na kubakia asilimia 75 na kushindwa kumalizia pesa iliyobakia, kuanzia hapo sheria ni rafiki kwa mchukua mkopo.

Haki ya kupatiwa taarifa ya siku 60 kabla ya mauzo kufuatia nia ya kufanya mauzo kufidia deni la mkopo. Hii haki, mara nyingi au kadhaa, imekuwa ikipuuzwa sana, hasa na wanaofanya minada (court brokers).

Mkopaji ana haki ya kulipa rejesho na riba kwa viwango vya fedha vinavyotambulika au kukubaliwa kwa mujibu wa sheria elekezi.

Katika hili, baadhi ya taasisi fedha hususan zile ndogo mfano na saccos na vikoba zimekuwa tabia au utamaduni wa kujipangia viwango vya marejesho na riba ambazo ni kubwa kupita kiasi huku na moja kwa moja kukiuka taratibu nzima za viwango vya fedha elekezi vilivyopo.

Kwa lengo au kusudi kuu la kujipatia faida kubwa na kujinufaisha zaidi, bila ya kumjali mteja.

**ITAENDELEA**



Reubeni Lumbagala

## Kalamu ya Mwalimu

# Chimba: Waziri Mkuu aliyeacha alama isiyofutika

KAMA ilivyo serikali ya kitaifa , hata ya wanafunzi vioni nayo ina uongozi,, mojawapo ni Waziri Mkuu.

Miongoni mwa viongozi hao ni Hussein Chimba. Ni Waziri Mkuu wa Serikali ya Wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Dodoma (Udoso-Udom). Katika makali hii, anazungumza kuhusu utekelezaji wa majukumu yake ya kiuongozi chuoni hapo.

Akizungumza na Nipashe anajivunia mengi kuwa yeye aliyasimamia kwa manufaa ya wanajumuiya ya Udom.

Baadhi ya mambo hayo ni kama vile, kuandaa utaratibu bora wa kuwapokea wanafunzi wa mwaka wa kwanza. Serikali ya wanafunzi, imeweka utaratibu wa kudumu na maalum kwa wanafunzi wanaoanza masomo kupokelewa katika Stendi ya Nane Nane kwa kutumia mabasi ya chuo na mabasi mengine ya benki za NMB na CRDB.

Anasema hilo limesaidia kuondoa usumbufu kwani mwanzoni wanafunzi wa mwaka wa kwanza ambao ni wageni walikuwa wakitumia gharama kubwa kufika chuoni kupitia ulaghai wa madereva wa boda boda wanaowasafirisha.

Wasafirishaji hao waliutumia ugeni wao kuwaumiza kwa kuwatoza fedha nyingi.

Jingine, anasema ni kutenga mfuko maalum wa kusaidia wasiojiweza. Huu ni mfuko maalum ambao unatengewa fedha kwa ajili ya kuwasaidia wanafunzi wenye shida mbalimbali. Kwa mfano, misiba, wagonjwa na hata kulipia nauli walemavu kwenda sehemu mbalimbali kama vile darasani.

Jambo la tatu, kuimarisha na kudumisha ulinzi na usalama. Hili limekuwa na mafanikio makubwa kutokana na ushirikiano mzuri kati ya wanafunzi, serikali ya wanafunzi na walinzi chuoni hapo.

Chuo Kikuu cha Dodoma ni chuo kikubwa ambacho suala la ulinzi na usalama ni lazima lipewe kipaumbele ili wanafunzi waweze kusoma katika mazingira mazuri bora na salama bila kuwa na hofu ya usalama wao wa maisha yao.

Aidha, kutokana na wingi wa wanafunzi wanaosoma chuoni hapo ni lazima kuwa na ulinzi wa kutosha ili kuwabaini wale wanaoingia chuoni hapo kwa nia ovu. Vitendo vya wizi vimedhibitiwa kwa ushirikiano mkubwa na vijana wa skauti

Nne, kuwasaidia wanafunzi kupata vitambulisho vya utaifa. Ofisi ya Waziri Mkuu wa serikali ya wanafunzi kwa kushirikiana na wizara nyingine walijitoa kwa hali na mali kushughulikia wanachuo ambao hawakuwa na vitambulisho vya utaifa wawewze kupata. Kutokana na ushirikiano huo, Ofisi ya Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (Nida) waliweza kuwapatia wanafunzi vitambulisho hivyo ambavyo ni muhimu sana.

Wanafunzi zaidi ya 12,000, wamenufaika na kupata vitambulisho vya utaifa.

Jambo jingine ni kutunza mazingira ya chuo. Katika kumuunga mkono Makamu wa Rais Samia Suluhu Hassan, katika kampeni ya kutunza mazingira na kulifanya jiji la Dodoma kuwa la kijani; miti zaidi ya 2,100 imepandwa chuoni kwa msaada wa Jiji la Dodoma. Pia kutokana na ushirikiano mzuri na vyuo vingine, Chuo Kikuu cha Mwenge kimetoa miche ya miti zaidi ya 100 katika kutunza mazingira ya Chuo Kikuu cha Dodoma.

Wengine ni kuwasaidia wanafunzi yatima, wanaotoka katika mazingira magumu na waliokosa mikopo kula chakula kwenye mesi za chuo (cafeteria) bure bila malipo yeyote.

Waziri Mkuu aliwashawishi watoa huduma ya chakula katika cafeteria zilizopo chuoni kuona namna ambayo watawasaidia wanafunzi wenye changamoto mbalimbali ili waweze kula bure kama sehemu ya kuwasaidia wahitaji hao kupata elimu bora huku wakiwa na uhakika wa kupata chakula. Cafeteria kama za Mwafrika, Kano, Mwarabu na nyingine zimekubali ombi la kutoa huduma ya chakula bure kwa baadhi ya wanafunzi wanaotoka katika mazingira magumu.

Jitihada hizi zimefanikiwa kutokana na ushirikiano wa Waziri wa Afya na cafeteria katika serikali ya wanafunzi Udom, Kulwa Boniface, wamiliki wa cafeteria, Dk. Ombeni Msuya na Mlezi wa wanafunzi Abubakar Hafidhi.

Hawa wote wamekuwa nguzo muhimu kufanikisha wanafunzi kula chakula bure kwenye cafeteria.

Anazungumzia kuchangishana fedha kwa ajili ya kuwalipia ada wanafunzi wanaotoka kwenye familia zisizo na kipato na waliokosa mikopo.

Kutokana na wingi wa wanafunzi wanaohitaji mikopo ya elimu ya juu, wengine hukosa mikopo hiyo.

Viongozi wa serikali ya wanafunzi wamekuwa wabunifu kwa kuwaomba wahisani na wanafunzi kuchangishana wenyewe ili kupata fedha za kuwasaidia wanafunzi wanaotoka mazingira magumu na wale waliokosa mikopo. Zoezi hili limerejesha matumaini ya wanafunzi waliokata tamaa kuwa na matumaini mapya ya kusonga mbele kielimu na kutimiza ndoto zao za maisha.

Nane, kutatua changamoto za kadi za bima ya afya kwa wanafunzi na kupata huduma bora na kwa wakati. Changamoto ya wanafunzi kupata kadi za bima ya afya kwa wakati imebaki historia kwani sasa wanafunzi wanapata kadi hizo kwa wakati na hata wanapoenda hospitali hupata huduma bora.

Waziri Mkuu Hussein Chimba anakiri kuwa mafanikio haya ni zao la ushirikiano wa viongozi wote wa serikali ya wanafunzi wa Udom pamoja wahadhiri.

# Unyanyasaji ulivyo kilio kwa watoto wa Zanzibar

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

LICHA ya Zanzibar kuwa na Sheria ya Mtoto namba 6 ya mwaka 2011 ambayo mwaka 2015 ilishinda tuzo ya sera za mustakabali yaani (Future Policy Award) pamoja na mafanikio hayo bado watoto wa Zanzibar wanaendelea kufanyiwa vitendo vya ukatili na udhalilishaji wa kijinsia.

Tuzo hiyo ilitolewa mjini Geneva, Uswisi na Shirika la World Future Council pamoja na Umoja wa Mabunge Duniani IPU na Shirika la Umoja wa Mataifa la Kuhudumia Watoto (UNICEF).

Adha, sheria hiyo imetajwa kuwa inasaidia kubadilisha mtazamo wa jamii kuhusu watoto na kuchangia katika kupambana na ukatili dhidi yao.

Hivi karibuni yalifanyika maadhimisho ya Siku ya Mtoto wa Afrika, Zanzibar kama sehemu ya Afrika iliadhimisha siku hiyo ili kuona watoto wanapewa haki zao za msingi kama wengine wa bara hilo.




Wadau wa kutetea haki za watoto visiwani Zanzibar katika moja ya mikutano ya kuhamasisha kumaliza ukatili. **PICHA:MTANDAO.**

Katika maadhimisho hayo wadau wa masuala ya watoto, wanasema kuwa Zanzibar bado inashuhudia vitendo mbalimbali vya kinyama ikiwa ni pamoja na kulawitiwa na kubakwa kwa watoto katika maeneo mbalimbali ya Unguja na Pemba ambapo jumla ya matukio 486 ya udhalilishaji wa kijinsia ya watoto yamefikishwa mahakamani kwa mwaka 2018.

Asha Salim Ali, Mkurugenzi wa kijiji cha kulelea watoto yatima na wanaoishi katika mazingira magumu (SOS) , anasema Zanzibar inakabiliwa na kiwango cha juu cha udhalilishaji wa watoto na wanawake ikiwemo utelekezwaji, ndoa za ututoni, ukatili wa kingono na wa kimwili licha ya kuwapo juhudi mbalimbali za kupinga vitendo hivyo.

"Licha ya nchi yetu kuwa na sheria mbalimbali, sera na mipango mizuri ya kuwalinda watoto dhidi ya aina zote za udhalilishaji, bado tumekuwa tukishuhudia vitendo hivi vikiibuka kila uchao maeneo mbalimbali ya visiwa vyetu", alisema Mkurugenzi huyo wa SOS.

Hata hivyo, anaeleza kuwa ni wajibu wa wazazi kutambua familia ndiyo taasisi ya mwanzo kuweka msingi wa maendeleo ya watoto kwa mujibu wa makubaliano ya kimataifa ikiwamo Zanzibar na Tanzania kwa ujumla.

Asha anawataka wazazi na walezi kutimiza wajibu huo kwa kuwalinda na kuwatengenezea watoto mustakbali bora wa maisha yao ya baadae ikiwa ni pamoja na kuwapatia haki zao za msingi kama elimu, matibabu na haki ya kusikilizwa.

Anaitaka serikali kuhakikisha sheria zinasimamiwa vizuri bila ya muhali (aibu) ili watoto waweze kulindwa na kutunzwa.

Anaonya kuwa bado jamii nayo haijawa tayari katika mapambano ya udhalilishaji hivyo serikali ibuni mbinu na njia bora za kuwashajihisha ili kutoa ushirikiano watoto wanapofanyiwa ukatili huo.

Mwakilishi wa taasisi ya kuhudumia watoto ya Save the Children Zanzibar, Amanda Procters, anasema ukatili dhidi ya watoto sio kwa Zanzibar pekee bali ni suala la dunia nzima, hivyo ni wajibu wa serikali kubuni mikakati mipya ya kukabiliana na udhalilishaji wa watoto Zanzibar.

"Save the Children, itashirikiana na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kuona ustawi wa watoto unalindwa na kupatiwa haki zote za msingi hasa ikizingatiwa kuwa watoto ni taifa la sasa", anasema Amanda.

Anaeleza kuwa mtoto wa kike anakabiliwa na changamoto nyingi zaidi ikilinganishwa na wa kiume, hivyo, ipo haja kwa serikali na wazazi kuwaongezea fursa watoto wa kike.

Fatma Ahmad, Meneja mradi wa huduma za simu kwa watoto, anasema vitendo vya udhalilishaji na ukatili wa kijinsia kwa watoto unatisha katika mkoa wa Kaskazini Unguja ukilinganisha na mikoa mingine ya Zanzibar.

"Kwa kweli watoto katika maeneo haya wanachangamoto kubwa ikiwa ni pamoja na kubakwa, kutelekezwa, kulawitiwa na kufanyiwa matendo mengine ya kikatili, hivyo, kama wadau ni lazima tuchukue juhudi za makusudi kuwalinda watoto weu, "anasema Fatuma.

Meneja wa sera na utetezi wa Chama cha Wanahabari Wanawake (Tamwa), Ofisi ya Zanzibar, Hawra Shamte, anasema kuwa iwapo watuhumiwa wanatiwa hatiani na kupewa adhabu kali vitendo vya ukatili na udhalilishaji wa watoto vingepungua au kuondoka. Anaeleza kuwa Zanzibar bila ya ukatili na udhalilishaji inawezekana iwapo kila mmoja atakuwa tayari kutoa ushirikiano kukomesha vitendo hivyo.

"Bado muhali umetawala katika jamii ambayo kila mmoja anaona aibu kumficha mtuhumiwa wa udhalilishaji kwa kuhofia kutengwa, hebu, tuachane na hali hii ili kuwanusuru watoto na janga hili"anasema.

Aidha, anasema kuwa Tamwa inashirikiana na wadau mbalimbali wa kutetea haki za watoto katika kuhakikisha mtoto analindwa na anapatiwa haki zake zinazostahiki.

### WAZAZI NA WALEZI

Sabra Ali ni mzazi anayesema kuwa vitendo vya udhalilishaji vinaleta athari katika jamii pamoja na kwenye familia hivyo serikali izidishe nguvu ili kutokomeza kabisa ukatili kwa watoto.

Aidha, anasema endapo serikali itashindwa kudhibiti tatizo hilo taifa, litakosa vijana bora na wenye nguvu za kufanya kazi.

Anaeleza kuwa jamii imekua ikivunjika moyo kutokana na wahusika wa matukio hayo kutochukuliwa hatua za kisheria au kupewa adhabu kali.

"Hata ukisema unampeleka mtuhumiwa katika vyombo vya sheria muda mfupi tu unamkuta yupo mitaani hivyo tunavunjika moyo"anasema.

Anaeleza kuwapo wimbi kubwa la baba wa kambo kuwabaka watoto wa kuwalea lakini mama wa mtoto anakataa kwenda katika vyombo vya sheria kutoa taarifa kwa kuhofia kupewa talaka au kukosa huduma kutoka kwa mume.

Ali Haji anasema kuwa hivi sasa kuna wimbi kubwa la watoto wanaobakwa na kupewa ujauzito, kuozeshwa kwa kukimbia kutoa ushahidi.

Anasema kitendo hicho hufanywa kwa makubaliano kati ya upande wa muhanga na upande wa mdhalilishaji kwa lengo la kesi hiyo kutosikilizwa mahakamani na kutolewa hukumu inayostahili.

"Haya hufanyika baada ya kuwapo kwa makubaliano na huwa hayafanywi bure fedha inatumika ili kuua kesi ya aina hiyo"anasema Haji mzazi na mlezi wa watoto.

### MAHAKAMA

Hakimu wa Mahakama ya Watoto Vuga Zanzibar, Naila Abdulbaswit, anasema kesi nyingi za ubakaji zinashindwa kupatiwa hukumu kutokana na mashahidi kukataa kutoa ushahidi.

Anasema kuwa kitendo cha mashahidi kukataa kutoa ushahidi mahakamani, inawalazimisha kufuta kesi baada ya kukaa muda mrefu mahakamani bila kusikilizwa.

"Niiombe jamii inapofikisha kesi hizi za udhalilishaji katika vyombo vya sheria kutokuwa wagumu kutoa ushahidi pale wanapohitajika ili kuweza kukomesha hivi vitendo,"anasema Hakimu huyo.

Anaeleza kuwa kuendelea kutopatikana kwa hukumu kwa watuhumiwa wa kesi hizo watoto wataendelea kudhalilishwa na kuwakosesha haki zao za msingi.

### WATOTO

Mwenyekiti wa baraza la watoto shehia ya Mahonda, Thureiya Hassan Mohammed, anasema mtoto ana haki ya kulindwa, kupewa elimu na kukingwa na majanga yote yanayoweza kumuathiri.

Anasema iwapo kama mtoto atajengewa mustakbali bora wa baadae sambamba na kupewa haki zake za msingi ni wazi kuwa anaweza kuwa kiongozi bora wa familia, jamii na taifa.

"Watoto wengi wanakoseshwa haki zao na kufanyiwa ukatili wa kutisha, ipo haja ya vyombo vya sheria kuwachukulia hatua za kisheria wafanyaji wa matendo hayo", anasema Thureiya.

### WAZIRI

Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Wanawake na Watoto Moudline Castico, anasema kuwa licha ya kuendelea kwa matendo ya udhalilishaji na ukatili wa kijinsia katika jamii, bado haijakata tamaa juu ya kupambana na maovu hayo.

Anasema serikali haijakaa kimya katika kufuatilia vitendo vya ukatili na udhalilishaji kwa watoto vinavyoendelea katika jamii, na kuutaka umma kushirikiana kuwafichua watu wa aina hiyo na sio kuwaonea muhali.

Anaeleza kuwa Zanzibar imekuwa ikitekeleza mpango wa kitaifa wa miaka mitano wa kutokomeza ukatili dhidi ya wanawake na watoto wenye lengo la kuzuia udhalilishaji wa aina zote.

"Juhudi mbalimbali zinachukuliwa na serikali kuhakikisha watoto wanalindwa bila ya kuvunjiwa haki zao kisheria ili kuweza kufikia malengo yao katika maisha" anasema Waziri Castico.

### MTOTO WA AFRIKA

Maadhimisho hayo ya siku ya Mtoto wa Afrika ni sehemu ya kumbukumbu ya kuwakumbuka watoto waliouawa kikatili huko Soweto Afrika kusini mwaka 1979.

Watoto hao walikumbwa na mkasa huo wa kudhalilishwa kufuatia kudai uhuru wao kwa maendeleo yao kwani walikuwa wakipinga kupewa elimu duni iliyokuwa ikitolewa kwa Waafrika na utawala wa kibaguzi.

Walipinga ukandamizwaji huo kwa watoto kwa kuandamana kwa amani kupinga utawala wa kibaguzi uliokuwa ukiendeshwa na makaburu wakati huo.

Wakiwa kwenye maandamano hayo watoto wengi wa shule waliuawa na wengine kujeruhiwa kwa kupigwa risasi na askari wa makaburu.

Kutokana na mauaji na mashambulio hayo kwa makusudi Afrika iliamua nchi zote za Afrika tangu mwaka 1991 kuadhimisha siku hiyo na Zanzibar ikiwa ni sehemu ya

Afrika nayo iliadhimisha siku hiyo huku watoto wakiwa na ujumbe mbalimbali wa kupinga ukatili na udhalilishaji dhidi yao.

MAKALA

# Tanzania inavyokaribia kuitokomeza Trachoma

Na Yasmine Protace

MARADHI ya vikope yajulikanao kitaalamu kama trachoma ni ugonjwa wa maambukizi ya macho macho yatokanayo na vimelea viitwavyo Chlamydia Trachomatis.

Vimelea vya ugonjwa huo, husambazwa na inzi wa majumbani kutoka kwa mtu mmoja hadi mwingine.

Ni ugonjwa unaoanzia utotoni na madhara ya kupata vikope kutokea ukubwani ikiwa mtoto hata pata tiba sahihi na kuimarishwa kwa usafi wake na mazingira yanayomzunguka.

**DALILI ZA MARADHI**

Vikope ni hali ya kope jichoni kuota na kukua zikielekea ndani ya jicho badala ya kutoka nje, hivyo kuanza kukwaruza kioo cha mbele ya jicho kinachojulikana kitaalamu kama Cornea.

Hali hiyo husababisha jeraha kwenye kioo cha jicho na liapopona huacha kovu, nalo huzuia mwanga wa kutosha kuingia ndani ya jicho na hivyo kusababisha uoni hafifu au hata kufika upofu kulingana na ukubwa wa tatizo.

Ugonjwa huo hupatikana zaidi katika nchi za hari au ukanda wa joto na zenye hali ya hewa ya kitropiki na maradhi haya huwashambulia watu wanaoishi kwenye jamii ambazo maisha yake ni duni.

Huwapata watu ambao hawana usafi , makazi yao yamejaa vumbi, hakuna usafi wa kuridhisha , watu hawana maji ya kutosha kuoga na kanawa na pia wapo inzi wanaosambaza magonjwa ikiwamo trakoma na mengineyo.

Magonjwa yanayosababisha makovu au cornea scars kwenye kioo cha mbele ya jicho ni kama vile ugonjwa wa usubi, surua ya utotoni na ajali za macho.

Matatizo hayo kwa pamoja yanaingia katika orodha ya magonjwa yanayosababisha upofu unaoweza kuepukika.

**DALILI YA VIKOPE**

Mojawapo kubwa ni macho kuwa mekundu, yanayotoa machozi muda wote, yenye kuuma na kuwasha.

Dalili hii zinapatikana zaidi kwa watoto wakati vimelea vya trachoma vinashambulia nyama lakini ya ndani ya vifuniko vya macho. Hatua hii ya ugonjwa kitaalamu inaitwa Chlamydia Conjunctivitis. Mashambulizi haya ya mara kwa mara yasipopatiwa tiba kusababisha vifuniko vya jicho kujikunja na kope kuingia ndani ya jicho na ndiyo mwanzo wa vikope. Hatua ya kupatikana vikope na madhara yake ni pamoja na kusababisha makovu kwenye kilo cha mbele cha jicho huonekana zaidi kwa watu wazima.

**HALI YA UGONJWA**

Tanzania imepunguza maambukizi ya ugonjwa wa trakoma kutoka wilaya 71 hadi sita ambazo zitaendelea na kumeza kingatiba, anasema Mratibu wa Taifa wa Magonjwa Yaliyokuwa hayapewi Kipaumbele kutoka Wizara ya Afya Dk.Upendo Mwingira.

Dokta Mwingira (pichani) , anayasema hayo wakati wa mafunzo ya kimataifa ya uchukuaji wa takwimu za ugonjwa wa vikope yaliyofanyika mkoani Arusha. Dokta Mwingira anasema kuwa kama nchi , Tanzania inajivunia kwa mafanikio makubwa kwani hivi sasa wilaya 65 hazihitaji tena kingatiba kulingana na vigezo vilivyowekwa na Shirika la Afya Duniani (WHO).

"Lengo la WHO ni kwamba hadi ifikapo mwaka 2020 tuwe tumetokomeza ugonjwa wa trakoma kama tatizo la kijamii, kwamba hatutaki maambukizi mapya, anasema Dokta Mwingira.

Aidha, anasema mwaka 2010 katika tathimini Tanzania kulikuwa na makadirio ya wagonjwa wa vikope takribani 160,000, lakini kutokana na jitihada za Wizara ya Afya hadi Julai 2018, inakadiriwa wagonjwa hao wamepungua mpaka kufikia 17,000.

Hata hivyo Dk. Mwingira anasema kazi ya kusawazisha vikope hapa nchini linaendelea zaidi ya mikoa 10 sasa hivi katika halmashauri zenye maambukizi.


Mafunzo haya yanahusisha wataalam wa macho kutoka mataifa mbalimbali duniani na kwa nchi za Afrika yanahudhuriwa na wataalamu wa nchi za Afrika Masharíki, Magharibi na Kati.

**MIKOA YENYE VIKOPE**

Mikoa yenye vikope ni pamoja na ya Kanda ya Kaskazini yenye jamii za wafugaji ambazo huishi kwenye sehemu kame lakini pia zisizo na maji ya kutosha na mazingira ya makazi si ya kudumu bali ya kuhama hama.



## CHEMSHABONGO NA NIPASHE NAMBA (00 7 00)




Dondoo: Kulia

1. Nchi yenye miji mikuu mitatu
8. Mzazi wa kiume 9. Upesi
10.Mfalme wa pili wa Israeli
11.tia hatiani
12.Jina la zamani la Malawi
15.Chanzo 16.Dalili ya kitu
18.Taka kwa unyenyekevu
20.Mji mkuu wa Somalia
22.Uvunjaji ungo
24.Ndege asiyeruka
25.Sema hapana
27.kaka wa mama
28.kitu au jambo linaloashiria

Dondoo: Chini

1. Watu wa Ghana
2. Chana vipande
3. Kuongezeka kimo
4. Ukweli wa jambo 5. fichua
6. toa tangazo kwa sauti kubwa 7. Shetani
13.Furaha
14.Bandari kubwa Angola
15.Mzungu wa Afrika ya kusini
17.Mpiganaji wa Kijapani
18.Safisha kwa maji na sabuni
19.mtu wa asili ya Bara Hindi
21.Starehe 23. dumu
26.Kagua

## Jibu Na: 6

| | | | | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| M | A | R | E | K | A | N | I | | S | | M | |
| O | | I | | I | | | M | N | I | N | G | A |
| M | W | A | N | Z | A | | A | | N | | U | |
| B | | L | | A | | M | M | E | A | | M | |
| A | S | I | | Z | A | B | U | N | I | | B | |
| S | | | K | I | T | U | | D | | | A | |
| A | G | U | A | | A | N | G | E | L | A | | |
| | H | | S | | M | I | A | L | E | | K | |
| | A | | H | | I | | M | E | N | Y | W | A |
| | R | I | A | K | A | | B | A | G | U | A | |
| F | A | N | T | A | | | I | | O | M | A | N |
| | M | K | A | T | A | B | A | | | B | | T |
| B | A | A | | A | | | | N | Y | A | M | A |

MAKALA

# Viongozi wa dini wahandisi wakuu uchumi wa viwanda




**Na Gaudensia Mngumi**

WAKATI Tanzania inajizatiti kujenga viwanda, kukuza uchumi na kuongeza jitihada za kufanya biashara, mojawapo ya jambo ambalo linapewa umuhimu wa kipekee ni uwapo wa amani ndani ya nchi kuanzia kwenye familia, mitaani na popote shughuli za uwekezaji na uzalishaji zinapofanyika.

Kwa kuliona hili viongozi wa dini kutoka madhehebu mbalimbali mkoani Dar es Salaam, wanasema mafanikio ya sera ya viwanda ni lazima yaende pamoja na kulinda amani, kudumisha uzalendo , uwajibikaji na kufanyakazi kwa bidii.

Viongozi wa dini wanaokutana kwenye Siku ya Amani, ndani ya Maonyesho ya Biashara ya Kimataifa (Sabasaba), jijini Dar es Salaam, wanafanya mdahalo kuhusu umuhimu na thamani ya amani katika uchumi wa viwanda.

Anapozungumza kwenye kusanyiko hilo, Mwenyekiti wa Kamati ya Amani Mkoa wa Dar es Salaam, Sheikh Alhaji Musa Salum, anasema amani ni muhimu kwa maendeleo ya uchumi, na kwamba amani ni utimilifu na haimaanishi kutokuwepo kwa vita.

"Amani ni watu kuwa na upendo baina yao, kuvumiliana, kuchukuliana, kuwa na mshikamano, uadilifu, kutenda haki na kuhurumiana." Anasema Sheikh Salum.

Anaongeza kuwa kwenye ujenzi wa uchumi wa viwanda, viongozi wa dini ni wa kwanza wakiwa na jukumu la kujenga nguzo kuu ya uchumi rasilimali watu ili iwe na maadili.

"Kuna nguzo sita za uchumi nazo ni watu, kazi, vifaa na teknolojia, soko la mali zinazozalishwa... Lakini sisi tunashughulika na mwili na roho ya mfanyakazi," anasema Sheikh Salum.

Anaongeza kuwa ni jukumu lao ni kuitengeneza nguvu kazi kuwa na uzalendo, kujiamini, uwajibikaji na kufanyakazi kwa weledi ili kufikia azma inayokusudiwa.

Hata hivyo, anaeleza kuwa ni lazima uchumi huo unaojengwa uwe na uzalishaji mkubwa na mapato mengi, lakini wenye matumizi madogo na ya muhimu ili kuwa na ziada kwa ajili ya uwekezaji mwingi zaidi ili kuleta maendeleo na hilo linafanikiwa ikiwa watu ni waadilifu na wazalendo.

"Ili kuwe na amani ni lazima shughuli za uchumi zinazofanyika zijenge taifa na zilete maendeleo kwa kuwapa wananchi huduma za maji, elimu bora, nishati, kulea na kusaidia wahitaji kama yatima na wajane ili wawe na maisha yenye Amani na ustawi,"anasema Sheikh Salum.

**KUKUMBUSHA AMANI**

Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Viwanda na Biashara, Ludovick Muhede, anawapa viongozi wa dini angalizo kuwakumbusha waamini wao kuhusu ulinzi na kuendeleza Amani.

"Amani ni tunu ni lazima tuilinde ndiyo inayohasisha kuweka vitega uchumi, viwanda, kuongoza ajira ili kubadili maisha duni ya Watanzania".

**UVUNJIFU.**

Naibu Katibu Mkuu Muhede anasema viongozi wa dini wana wajibu wa kukemea viashiria vya uvunjifu wa amani, ambavyo ni pamoja na ufisadi, fujo zisizo na sababu, kuendeleza tamaa binafsi, uonevu na kudhulumu wananchi.

Anasisitiza kuwa viwanda, biashara, uwekezaji hauwezi kufanikiwa iwapo taifa halina Amani. Aidha, akifungua kongamano hilo, Naibu Spika, Dk. Tulia Ackson(pichani ), anasema viongozi wa dini wana umuhimu kwa sababu wanasikilizwa na wananchi wote bila kujali itikadi na vyama vya siasa. Anawaambia viongozi wa dini kuwa wana umuhimu wa kipekee kwani wanasikilizwa na Watanzania wote. Kwa vile ndani ya dini kuna wanachama wa vyama vyote na wapo pia wasio na ufuasi wa vyama vya siasa , lakini ni waamini na wanawasikiliza viongozi wao wa dini.

Kadhalika Dk. Ackson anawataka wazazi na walezi kuwafunza watoto wao umuhimu wa kuthamini na kulinda amani ya taifa kwa vile kinachowapa watu wote furaha ni uwepo wa amani.

Anasema katika Biblia maandiko yanasema wana amani nyingi waishikao sheria ya bwana, vivyo wana amani nyingi wanaoheshimu sheria za nchi. Akiwasilisha mada kuhusu Wosia wa Mwalimu Nyerere kuhusu umuhimu wa Amani kwenye uwekezaji na kufikia maendeleo ya viwanda, Mkurugenzi wa Taasisi ya Mwalimu Nyerere (MNF) Joseph Butiku, anasema msingi mkuu wa Amani ni haki.

Anasisitiza kuwa haki kubwa kuliko zote ni ya kuishi na kuthamini utu wa mtu, ndiyo maana msingi wa katiba ni haki na usawa wa binadamu wote.

Anasema Tanzania ina maandiko na vitabu vinavyozungumzia haki na amani, ambavyo Mwalimu Nyerere aliandaa ikiwa ni pamoja na Katiba, Azimio la Arusha, Katiba ya chama na kwa ujumla amani inatajwa kuwa msingi wa maendeleo.

Anasema maendeleo ni haki ya kila Mtanzania na kwamba msingi mkuu wa maendeleo na haki ya kila raia wa taifa hili ni rasilimali za nchi.

"Rasilimali zote za taifa ni mali ya Watanzania iwe almasi, dhahabu, bahari, mbuga za wanyama ni mali ya wote. Uvunjifu wa amani unatokea endapo kutakuwa na wachache wanaojimilikisha mali za umma, kuvunja katiba na kunapokuwa na uongozi usiowajibika kwa Watanzania,"anaonya Butiku.

Butiku ambaye amewahi kuwa Katibu wa Rais, wakati wa awamu ya kwanza anasisitiza kuwa kila mtu ana haki ya kuwa mwanachama wa chama anachokipenda, kuabudu kwa imani ya dini anayoiamini na kwamba yote hayo yanasimamiwa na katiba na sheria.

Anaonya kuhusu kuvunja katiba na kupindisha sheria kwa vile hayo ndiyo yanayoleta kuvunjika kwa amani. Anaonya kuwa kukosa uzalendo na kutofanya kazi kwa bidii ni mambo yanayotishia amani akisema, uvuvi ni tatizo la Watanzania na iwapo raia hawatapenda kufanyakazi kikamilifu kufikia maendeleo ni dhahiri wanakosa haki ya maendeleo na hata kusababisha kukosekana amani.

# Jeshi lazima jaribio la mapinduzi

**KHARTOUM,** Sudan

WANAJESHI kadhaa wa ngazi ya juu nchini Sudan wanahusishwa na jaribio la mapinduzi dhidi ya baraza la kijeshi Sudan,kwa nia ya kuzuia utekelezaji wa makubaliano ya kisiasa yaliyofikiwa na yatakayosainiwa leo Jumamosi.

Maofisa takriban 16 wa kijeshi wamekamatwa kufuatia jaribio la mapinduzi ya kijeshi dhidi ya utawala wa muda unaoshikiliwa na baraza la kijeshi nchini Sudan.

Luteni Jenerali Gamal Omar ambaye ni mjumbe wa baraza kuu la kijeshi linaloshikilia madaraka katika nchi hiyo amesema hivi sasa kuwasaka maofisa wengine zaidi walioshiriki kwenye njama hiyo ya kutaka kufanya mapinduzi ya kijeshi jana alhamisi.

**Maofisa takriban 16 wa kijeshi wamekamatwa kufuatia jaribio la mapinduzi ya kijeshi dhidi ya utawala wa muda unaoshikiliwa na baraza la kijeshi nchini Sudan.**

"Uhuru na kutangazwa mageuzi ni mambo yanayoleta matumaini ni malengo ya watu wa Sudan kuondokana na utawala uliopita na kuangalia mbele katika kupatikana uthabiti na usalama na kuwapatia Wasudan walioanzisha vuguvugu takatifu la mapinduzi, maisha ya staha wanayostahili.

" Kutokana hali hii tunayoishi, vikosi vyetu vya usalama vimefanikiwa kuzima jaribio la mapinduzi yaliyoshindwa yaliyoandaliwa na kupangwa na kundi la maofisa wa juu jeshini, vikosi vya usalama na idara za kitaifa za usalama, kwa nia ya kufanya mapinduzi ya kijeshi kutatiza utekelezaji wa makubaliano ya kisiasa yaliyoingoza nchi hii kuelekea kwenye mabadiliko ya kisiasa na kuyafikia mahitaji ya wananchi wetu."

Baraza la kijeshi lilisema waliokamatwa katika njama hiyo wanne miongoni mwao ni maofisa wastaafu jeshini. Sakata hili limetokea katika wakati ambao unasubiriwa mchakato wa kutia saini makubaliano ya kisiasa.

Wiki iliyopita jeshi na muungano wa wanaopigania demokrasia nchini humo walikubaliana kuhusu baraza huru la pamoja la kusimamia uongozi wa nchi hiyo kwa miaka mitatu wakati nchi hiyo ikiandaa uchaguzi mkuu wa kidemokrasia.



Umoja wa Afrika kupitia mjumbe wake wa ngazi ya juu Mohammed el Hassan Labat, umeshathibitisha kwamba mchakato huo wa kusainiwa makubaliano ya kisiasa utafanyika leo Jumamosi, tangazo ambalo limetolewa saa chache tu baada ya jeshi la Sudan kudai limezima jaribio la mapinduzi jana usiku.Kadhalika msuluhishi kutoka Ethiopia Mohamoud Dirir akitoa ufafanuzi zaidi juu ya makubaliano kwa kueleza"

"Waraka wa kisiasa umeshakubalika kwa sauti moja kilichobaki ni tangazo litakalochanganua kipindi cha mpito au kipindi cha mpito kuelekea serikali ya kiraia.Hili litajadiliwa na kuzungumzwa na kutiwa saini wakati mmoja", alisema Dirir.

Makubaliano ya kisiasa yanayosubiri kusainiwa ni njia inayodhamiriwa kuuvunja mkwamo wa kisiasa ulioikumba nchi hii tangu alipoangushwa madarakani rais aliyeiongoza kwa mkono wa chuma Omar al Bashir mwezi Aprili mwaka huu. **DW**



Wasudani wakiwa mitaani kwenye maandamano ya muda mrefu kupinga utawala wa Bashir (Picha ndogo juu) aliyeongoza taifa hilo kiimla kwa miongo kadhaa na kusababisha mauaji, uhasama na kudorora uchumi. **PICHA: MTANDAO**

## Vijana Afrika 'vijogoo' kuhonga

**BERLIN,** Ujerumani

VIJANA wa Afrika wana uwezekano mkubwa zaidi wa kutoa hongo kuliko watu wazima au wenye umri mkubwa zaidi.

Shirika la kukabiliana na ufisadi la kimataifa la Transparency International linasema vijana wa Afrika wenye umri wa kati ya miaka 18 hadi 34, wana uwezekano mkubwa wa kutoa rushwa kuliko watu wenye umri mkubwa wa zaidi ya miaka 55.

Katika kipimo chake cha kiwango cha ufisadi duniani cha mwaka 2019, shirika hilo limesema kuwa utafiti wake pia umefichua kwamba watu maskini zaidi wana uwezekano mara mbili zaidi wa kutoa rushwa na wanauwezekano mkubwa pia wa kuwa waathiriwa wa hongo inayosababishwa na tabia ya urasimu kuliko matajiri.

Utafiti huo wa kila mwaka ambao ni wa mwaka wa 10, unasema kuwa barani Afrika ni wa kiwango cha juu zaidi katika Jamhuri ya Kidemokrasi ya Kongo, ambapo asilimia "75 ya wale ambao wanakabiliwa na ufisadi walilipa polisi hongo".

Shirika lilisema mataifa yanayoongoza kwa hongo ni Congo yenye alama za juu za asilimia 80, Liberia 53 wakati Sierra Leone ina alama 52.

Mataifa yenye kiwango cha chini ulaji mlungula ni Mauritius asilimia tano, Botswana nane na CaboVerde asilimia 8. Ripoti hiyo pia ilisema kuwa raia wa kigeni pia huchangia kwa kiasi kikubwa katika kuchochea na kushiriki ufisadi katika bara la Afrika , "na hivyo kuhujumu maendeleo ya kudumu ya kikanda".

Transparency International ilisema kuwa kampuni hutoa hongo ili kupata mikataba kama vile ya haki ya uchimbaji wa madini, mikataba ya ujenzi wa miradi mikubwa na mikataba mingine.

Transparency International ilisema pia kwamba matokeo ya utafiti wake yametokana na mahojiano ya ana kwa ana kati ya Septemba 2016 na Septemba 2018, yaliyofanyika kwa ushirikiano na taasisi ya utafiti wa kimaendeleo barani Afrika-Afrobarometer. **BBC**

## Akamatwa kuishi na maiti inayoharibika

**TEXAS,** Marekani

POLISI nchini Marekani anamshikilia mwanamke mmoja jimboni Texas, Marekani kwa madai ya kukutwa na masalia ya mwili wa mama yake .

Masalia ya maiti ya mama yake inayooza yaligunduliwa nyumbani wanakoishi pamoja na familia.

Polisi wanaamini mwanamke huyo mwenye umri wa miaka 71 alifariki mwaka 2016 baada ya kuanguka au kudondoka na kuumia.

Wanamtuhumu binti yake mwenye umri wa miaka 47kuwa alishindwa kumhudumia vizuri mamake aliyefariki "siku chache baadaye" kutokana na athari ya kuanguka huko.

Masalio ya mwili wa marehemu huyo yalipatikana kwenye sakafu ya chumba kimoja. Binti yake na mjukuu wake marehemu walilala katika chumba cha pili katika nyumba hiyo.

Mjukuu wa marehemu alikuwa na miaka 15 wakati akiishi na maiti ya bibi yake. Na kutokana na hilo, mamake ameshtakiwa kwa 'kumdhuru mtoto' wa chini ya miaka 15.

Mjukuu huyo sasa anatazamwa na jamaa zao na anapokea msaada kutoka kitengo cha kuwalinda watoto.

Huenda mwanamke huyo akakabiliwa na kifungo cha hadi miaka 20 gerezani na faini ya hadi Dola 10,000.

Polisi walisema marehemu bibi huyo aliheshimika katika jamii kwenye eneo hilo, na alifanya kazi kama karani na mwalimu msaidizi katika mojawapo wa shule katika eneo hilo kwa miaka 35.

Alipostaafu, alikuwa akifanya kazi ya kukusanya tiketi katika sherehe za michezo huko Seguin. **BBC**

# HADITHI

WASWAHILI wana msemo wao unaosema kuwa ufukara ni jereha la ulimwengu. Wakiwa na maana, mtu fukara mara nyingi hukutana na mitihani mikubwa duniani, ambayo mingi husababishwa na baadhi ya binadamu wengine wenye vipato kwa kuwaona hawana thamani na hawatajiki kuwa na kitu chochote cha thamani.

# JUMBA JEKUNDU- 9

Mtunzi anapatikana (0716 350534)

**Na Adam Fungamwango**




KIJANA anayetoka kwenye familia duni Kadili, anatokea kupendwa na msichana mrembo anayetoka kwenye familia ya kitajiri, Edina.

Lakini kitendo hicho kinamsababishia kijana huyo matatizo makubwa ambayo hajawahi kuyapata katika maisha yake, kiasi cha maisha yake kuwa hatarini. Fuatilia mkasa huu wa aina yake.

==============================================

Kwa mbali alimuona Edina akiingia kwa kunyata na si kwa bashasha kama ambavyo huwa anafanya. Hakuonekana kutaka kucheza.

Aliingia kwenye kundi la watu waliokuwa wanacheza, akinesanesa mithili ya mtu anayecheza, lakini ni kama vile alikuwa anatafuta kitu.

Kama kawaida, mabausa watatu walikaa kando wakimuangalia binti huyo akionekana kujipindapinda kufuatisha mdundo wa muziki.

Ni kama vile alikuwa akizunguka, lakini alijua walipo. Alipofika karibu na Kadili aliinua jicho na kuangalia tena chini. Akatingisha kichwa taratibu kama ishara ya kukataa kitu. Ishara hizi zote zilimchanganya Kadili. Wakati akidhani atafika pale alipo, aligeuka na kurejea alipotoka. Kadili na Meze walishuhudia akiangusha kitu kama karatasi iliyokuwa imekunjwakunjwa kama vile kitu kisicho na thamani, takataka, au karatasi iliyofungiwa kitu cha kula na mlaji akawa amemaliza.

Kwa sababu kawaida yao huwa hawamfuati msichana yule wala kumsalimia mpaka yeye aanze kufanya hivyo, hawakufanya chochote bali kumsimama tu na kushangaa. Mwili wa Kadili ndiyo uliokuwa umekufa ganzi zaidi. Kwa akili ya haraka, Meze aliifuata karatasi ile iliyoangushwa kwa bahati mbaya au makusudi kwa mrembo Edina.

Kadili yeye macho yake yalikuwa yakimsindikiza mrembo Edina ambaye alionekana hakuwa kwenye hali ya kawaida, akitoka moja kwa moja kwenye ukumbi huo huku mabausa wakimfauta kwa nyuma.

Meze alirejea na kikaratasi kile akiwa amekishika mkononi, lakini hakutaka kukikunjua na kujua kuna nini.

Alichofanya ni kumkabidhi Kadili. Wakiwa kama wamechanganyikiwa, walishikana mikono kama vile wanakwenda msalani.

Nje ya maliwato kulikuwa na taa zilizomulika kwa ajili ya usalama wa watumiaji.

Hakuwa na wasiwasi sana kwa sababu walijua Edina na mabaunsa wake wameshaondoka.

Kadili alikunjia karatasi hiyo kuona kama kuna kitu chochote ndani au nini ambacho mrembo yule alikusudia.

Karatasi ilikuwa na maandishi yaliyoandikwa kwa mkono na wino wa rangi ya bluu.

Kila mmoja aliusoma na kuurudia mara tatu. Waliangaliana. Kadili miguu ilizidi kutetemeka kuliko mwenzake.

Hakuna aliyekuwana hamu tena ya kuendelea kukaa pale, zaidi ya kuondoka.

********************************

> **Na kama ni bwana'ake, mchumba wake, mpenzi wake au mumewe kwa nini awe anamruhusu kwenda disco, halafu anawaambia mabaunsa wamlinde asicheze na mtu badala ya kumpiga marufuku kwenda?**

Hakupata usingizi. Kila akiwaza haelewi ni nini kinaendelea. Alirudisha kumbukumbu yake nyuma.

Alikutana na msichana malkia ya urembo kwenye hoteli ya Blue Star maeneo ya Sinza.

Kutokana na umahiri wa kucheza, demu akamuomba kucheza naye. Aliondoka bila kumuaga.

Mara ya pili alipokwenda tena yeye na rafiki yake Meze walikutana na msichana huyo aliyekuwa na furaha zaidi kuliko siku ya kwanza. Akacheza naye na kuongea maneno japo machache ya kujitambulisha.

Mara zote hizo alitokea kumpenda, lakini hakuna hata siku moja aliyowahi kumwambia neno 'nakupenda.'

Badala yake alimpenda na neno hilo kubaki moyoni. Mtu pekee aliyemtamkia kuwa anampenda yule mwanadada ni rafiki yake Meze. Kadili alikuwa hana uhakika kama siku zote hizo ambazo demu anamfuata kucheza naye ni kwa sababu anampenda au ni kwa sababu anapenda kucheza naye kutokana na kuonekana fundi wa kucheza.

Hii mara ya tatu ndiyo imemchanganya zaidi. Msichana amekuja amenuna. Akaangusha kikaratasi ambacho Meze alikiokota na wakaenda kukisoma. Kilikuwa kimeandikwa maneno haya.

'Leo sitawafuata. Sikucheza na wewe swahiba yangu Kadili. Na pia msijaribu kunifuata. Nimewekewa ulinzi leo na hawa mabaunsa sitakiwi kucheza na mtu yoyote, natakiwa kucheza peke yangu tu. Na simu yangu wameichukua na sitakiwi kuitumia tena. Kinachofanyika ni kufuata taratibu ya kujisajili upya kwa namba nyingine. Ni kwa sababu nisiwasiliane na watu ambao nawasiliana nao. Vinginevyo ningekuandikia hata namba humu ili unipigie. Nashukuru sana kwa siku ambazo tulikuwa tunacheza wote. Nilifarijika sana. Lakini sasa sivyo. Nasema hivi kwa sababu hata kwenda disco kwa sasa nitakuwa napangiwa sehemu ya kwenda kucheza, tena sehemu tofauti kila wiki kwa hiyo hata hamuwezi kujua wapi nipo.

Kwa heri ya kuonana. Milima haikutani, lakini binadamu wanakutana. Mungu akipenda na tukaonana nitakueleza kila kitu kilichotokea hadi ikawa hivi, kama haikuwezekana basi Mungu hakupenda na kazi yake haina makosa.'

Maandishi ya barua ile yalikuwa yakijirudia mara kwa mara kwenye mawazo yake, usiku wa manane, wakati watu wote wamelala. Sauti za nje zikihanikiza kwa sauti ya kuogofya. Ni Kadili pekee ndiye aliyekuwa macho.

Alikuwa na maumivu makali moyoni. Alikuwa anaugua. Bora angekuwa anaumwa jino, au tumbo la kuhara.

Alikuwa anamwa mapenzi. Mapenzi ya mwanamke ambaye hata siku moja hajawahi kumwambia kuwa 'nakupenda'. Hata huyo mwanamke mwenyewe hawajawahi kumwambia Kadili kuwa 'nakupenda'.

Hata kwenye karatasi aliyoandika bado hakukuwa na dalili kuwa anampenda, zaidi ya kuonekana kama kukosa kampani tu.

"Ni nani aliyemkataza kucheza na mtu yoyote kwenye disco?"

"Na inavyoonekana ni kwamba amepigwa marufuku kwa sababu ya kucheza mimi kila anapokuja disco." Kadili alikuwa akijiuliza na kujiambia mwenyewe.

"Ni nani aliyemwambia huyo mtu aliyemkataza kuwa Edina kila anapokwenda disco kuna kijana anacheza naye? Nadhani ni wale mabausa." Alijiuliza na kujijibu mwenyewe.

"Na kama ni bwana'ake, mchumba wake, mpenzi wake au mumewe kwa nini awe anamruhusu kwenda disco, halafu anawaambia mabaunsa wamlinde asicheze na mtu badala ya kumpiga marufuku kwenda?"

"Kwa nini mara zote hizo tatu ambazo amekutana naye disco hajawahi kuja na huyo mumewe?"

"Na kwa nini ameendelea kumruhusu kwenda disco, lakini kwa kumbadilishia maeneo ya kwenda badala ya Blue Stars sasa atakuwa akipangiwa kumbi ya kwenda, tena tofauti kila wiki, badala ya kumpiga tu marufuku au kwenda wote?"

"Na kwa nini Edina aandike yote haya kwenye karatasi ili mimi nifahamu suala hilo?"

"Kulikuwa na ulazima gani wa mimi kufahamu maswala yake na mumewe au hawara yake?"

Haya ni maswali ambayo alikuwa anajiuliza Kadili bila majibu yoyote usiku wa manane.

Pole pole, hatimaye usingizi mzito ukampitia.

**Itaendelelea Jumamosi**

## TANGAZO

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

### ELIMU/ MASOMO

**NAFASI ZA MASOMO,** Chuo cha Uuguzi na Ukunga MASSANA kilichopo dar es Salaam, Mbezi Beach Goba Road. Kinatangaza nafasi za masomo kwa ngazi ya Diploma na cheti yatakayoanza mwezi wa September 2019. Njoo tukujazie Form Kupitia Mtandao wa Nacte: 0713 321260/0769 666880

### MCHANGANYIKO

**VIWANJA VINAUZWA,** Viwanja Vinauzwa Kibaha Visiga, ukubwa ni mita 20 kwa 20 bei ni millioni moja tuu(1,000,000/=) unaweza kulipa kwa awamu ndani ya miezi mitatu. Huduma zote zipo. Mawasiliano: 0714 090008 au 0767 090008

**PROJECTS GENERATE INCOMES AND CREATE EMPLOYMENT**
*Learn DESIGNING projects *Find DONORS *Establish NGO 0784505108 /0769505108

**NIPASHE NI JIBU LAKO**

NJOO UTANGAZE NASI BIDHAA YAKO KWA BEI NAFUU SANA


### KUPOTEA KWA PASSPORT/HATI YA KUSAFIRIA



**Liberatha Mbasha Mosses** anatangaza kupotea kwa Passport yake yenye **TAE 103515** iliyotolewa Na Idara ya Uhamiaji Dar es Salaam mwaka 2019. Yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi. Polisi Taarifa: **DAR/KIJ/RB/25736/2019**

115321302


### KUPOTEA KWA CERTIFICATE



**DENICE F. MINJA** anatangaza kupotelewa na Certificate of degree in bachelor of science in health Information Systems, **B.SC (HIS) 00000018,** Iliyotolewa –UDOM. mwaka 2015. Taarifa ya polisi: **AR/RB 4849/2019.**

115321102

### VYETI VIMEPOTEA



**CELESTINE MSIMBU SHIJA** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye **index namba S.800/0040** kilichotolewa na LOYOLA HIGH SCHOOL mwaka 1999. Cheti cha Chuo – CBE chenye namba **TFC.03DBA/ACC/193** kilichotolewa na **COLLEGE OF BUSINESS EDUCATION** mwaka 2005. Yeyote atakayeviona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi cheti cha kidato cha nne: **KJN/RB/8228/2018.** Taarifa ya polisi cheti cha chuo: **DAR/OST/RB/33597/2019.**

115320802

### CHETI KIMEPOTEA



**LINA COLBERT MUSHI** anatangaza kupotelewa na Form Four Leaving Certificate yenye **index namba S.0284/0045** iliyotolewa na RoNeCa Girls Secondary School mwaka 2016. Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **DAR/STA/RB/106066/2019.**

115321802

### KUPOTELEWA NA KADI YA PIKIPIKI

**MSITA VERONICA MKWAZI** Anatangaza kupotelewa na kadi ya Pikipiki yenye namba ya usajili **MC 814 BCU,** aina ya HONDA. Yenye rangi Nyekundu Chassis namba **LALPCJ0D4C3006193** Yeyote atakayeiona atoe taarifa Kituo cha Polisi. Taarifa ya Polisi: **MW/TR/RB/898/2019**

215321702

### KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

**GLADNESS NDEKERO MGHAMBA** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari aina ya **TOYOTA IST** yenye namba za usajili **T 582 DLN.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **DAR/KIJ/RB/124924/2019.**

115317902

### KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

**GRACE KOKUUMBYA MUTAYOBA** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari aina ya TOYOTA CARINA yenye namba za usajili **T 879 CAX.** Chassis namba **AT2116012948.** Engine namba **7AG593799.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **DAR/MSI/RB/95586/2019.**

115320702

### KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**Kituo cha Afya cha Baraki** kinatangaza kupotea kwa kadi Ya Gari yenye namba **T 750 AFA** Aina ya **TOYOTA LAND CRUISER** Kwa atakae iona atoe taarifa kituo chochote cha polisi kilichopo Karibu kwa Kumb, **MUS/RB/9454/2018.**

115320702

### KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**EMMANUEL RICHARD MALEKO** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari aina ya TOYOTA NOAH yenye namba za usajili **T 817 CPL** rangi ya BLACK. Chassis namba **SR400108070.** Engine namba. **3S0070800.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **DOD/DOD/RB/12440/2019**

115321002

KWA MATANGAZO MADOGO MADOGO TUPIGIE

***0767 223311***

**Kwa Habari Motomoto usikose Gazeti lako la Nipashe kila siku**

**NJOO UTANGAZE BIDHAA YAKO KWA BEI NAFUU SANA**

**OFISI ZA MATANGAZO**
**MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,**
**PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 745 700 710.**
**E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com**

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.



# BENIN WAPOKELEWA KISHUJAA

**PORTO**-NOVO

LICHA ya Benin kutolewa kwenye michuano ya Kombe la Mataifa Afrika (Afcon) Jumatano wiki hii kwa kufungwa na Senegal, lakini wamekaribishwa kishujaa.

Walionyesha kiwango cha kuvutia walipowatoa Morocco kwenye hatua ya 16 Bora, kabla ya wao kufungwa bao 1-0 na Senegal kwenye robo fainali.

Hata kwenye mchezo dhidi ya Senegal waliwabana vizuri na bao hilo pekee kwenye mchezo huo walifungwa dakika ya 70 na Idrissa Gueye.

"Tulikuwa na uhakika wa kufika nusu fainali, lakini kwa sasa tumeridhika na matokeo haya," alisema mshambuliaji wa Benin, Steve Mounie. "Tunajisikia fahari kwa nafasi tuliyofika, lakini kwa upande mwingine tunaamini tulikuwa na uwezo wa kufika mbali zaidi."

Benin walishiriki michuano ya mwaka huu kwa mara ya nne, na wamefungwa jumla ya mechi tisa katika michuano ya mwaka 2004, 2006 na 2010.

## Nigeria vs Algeria, nusu fainali ya kibabe

**CAIRO,** Misri

NIGERIA na Algeria zitapambana kuwania kucheza fainali ya Kombe la Mataifa ya Afrika mwaka 2019, wakati zitakapokutana Jumapili katika mchezo wa hatua ya nusu fainali ya michuano hiyo.

Nigeria ilifuzu nusu fainali baada ya kuibuka na ushindi wa mabao 2-1 dhidi ya Afrika Kusini (Bafana Bafana) mapema wiki hii. Super Eagles wenyewe walipata ushindi huo dhidi ya Bafana Bafana, shukrani kwa mabao ya Samuel Chukwueze na William Troost-Ekong.

Mbinu za Kocha Gernot Rohr zilionekana kuwa na manufaa makubwa kwao na kuweza kupata ushindi huo dhidi ya Afrika Kusini ambayo iliwatoa wenyeji wa mashindano hayo, Misri (Mafarao).

Huku wao Algeria walifuzu kwa nafasi hiyo, baada ya kuwafunga Ivory Coast kwenye robo fainali Alhamisi usiku.

Algeria waliongoza mchezo huo na walipata bao la mapema kupitia Sofiane Feghouli, lakini wakakosa penalti iliyopigwa na Baghdad Bounedjah na Ivory Coast wakasawazisha kupitia Jonathan Kodjia na kuufanya mchezo huo kumalizika kwa sare ya 1-1 na kwenda muda wa ziada.

Kwenye changamoto ya mikwaju ya penalti wakaibuka na ushindi wa mabao 4-3 na licha ya Youcef Belaili kukosa penalti ya mwisho. Ivory Coast walikosa penalti kupitia kwa Wilfried Bony na Serey Die.

Algeria wameingia kwenye nusu fainali ya michuano hii kwa mara ya kwanza tangu mwaka 2010 na wanajipanga kutinga fainali hiyo kwa mara ya kwanza tangu walipofika mwaka 1990 na kulitwaa kombe hilo kwa mara yao ya kwanza.

Nigeria kwa mara ya mwisho kufuzu nusu fainali ya Afcon ilikuwa ni mwaka 2013 nchini Afrika Kusini wakati waliposhinda kombe hilo.

Takwimu zinaonyesha Nigeria na Algeria zimekutana mara 19, huku Super Eagles wakishinda mara tisa na Algeria mara saba, na mechi tatu wakimaliza kwa sare.



## Kocha Madagascar ajivunia mafanikio yao



**CAIRO,** Misri

KOCHA wa Timu ya Taifa ya Madagascar, Nicolas Dupuis amebainisha kwamba itakuwa ngumu kwenye michuano ya Kombe la Mataifa ya Afrika (Afcon), kwa timu ndogo kuweza kung'ara na kufika robo fainali kama walivyofanya wao.

Madagascar ambao wameshiriki michuano hiyo kwa mara ya kwanza, ndoto zao zilizimwa Alhamisi walipofungwa mabao 3-0 na Tunisia.

"Najisikia fahari kubwa kwa kile ambacho wachezaji wangu wamefanya tangu mwanzo wa mashindano haya. Nimewavulia kofia," alisema Dupuis, ambaye mkataba wake umemalizika baada ya mashindano hayo nchini Misri.


"Leo (juzi) ilikuwa hatua kubwa kwetu. Kwa sasa sifikiri kuhusu majaliwa yangu ya baadae, kwangu sio kitu muhimu. Mimi ni mtu ambaye naiweka kwanza mbele Madagascar."

Dupuis alichukua mikoba ya kuinoa Madagascar mwaka 2017 na ameitengeneza timu hiyo kuweza kucheza soka la ushindani na sasa wanashika nafasi ya 190 kwenye viwango vya ubora duniani.

"Sijui kama kipaumbele cha Madagascar ni kuniacha niendelee kuwa kocha," aliendelea akisema Dupuis.

## HABARI MICHEZO

# Lukaku akosa mazoezi ya Man United




**PERTH,** Australia

ROMELU Lukaku hakuwapo kwenye siku ya kwanza ya mazoezi ya Manchester United hapa Perth juzi Alhamisi, huku uvumi ukizidi kuenea juu ya majaliwa yake klabuni hapo.

Mshambuliaji huyo wa kimataifa wa Ubelgiji alikosa mazoezi hayo pamoja na Anthony Martial kwenye Uwanja wa WACA ambapo mashabiki 12,000 walihudhuria.

Lukaku anatakiwa na Inter Milan na mazungumzo kati ya maofisa wa klabu hizo yakiwa yamefanyika wiki hii jijini London.

Mshambuliaji huyo anataka kuondoka Old Trafford kipindi hiki cha majira ya joto, kwani kwa sasa namba yake imechukuliwa na Marcus Rashford.

Kwa mujibu wa ESPN FC, Inter inataka kumsajili Lukaku kwa mkataba wa awali wa mkopo, huku United wanataka kulipwa pauni milioni 80 ili kumwachia.

Lukaku alikuwa kwenye rada za Antonio Conte wakati akiwa Chelsea kabla ya kuhamia United mwaka 2017 na mchezaji huyo wa zamani wa Everton anamchukulia kocha huyo wa Italia kama kocha bora duniani.

Wakati alipojiunga kwa mara ya kwanza pale United, Lukaku alikuwa chaguo la kwanza, lakini alipoteza namba kwa Rashford mara tu Ole Gunnar Solskjaer alipochukua mikoba ya Jose Mourinho.

Kiungo, Paul Pogba ni mchezaji mwingine wa United ambaye anaweza kuondoka kipindi hiki cha majira ya joto, huku wakala wake, Mino Raiola, akisema hivi karibuni kwamba mipango inaendelea.

Hata hivyo, Solskjaer amesema United hawana mpango wa kumuuuza mchezaji yoyote.

# KOSCIELNY AIGOMEA ARSENAL




**NEW YORK,** Marekani

NAHODHA Laurent Koscielny amekataa kwenda Marekani na kikosi cha Arsenal katika maandalizi ya msimu mpya wa Ligi Kuu England, klabu hiyo imesema.

Majaliwa ya Koscielny ndani ya Arsenal yameripotiwa kuwa shakani baada ya kuingia kwenye mwaka wake wa mwisho wa mkataba wake, na kukiwa hakuna ishara ya kusaini mkataba mpya.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 33 amekuwa akihusishwa na mpango wa kutaka kurudi nchini Ufaransa katika Klabu ya Bordeaux.

Arsenal imethibitisha taarifa hizo kwa taarifa yake iliyosema: "Tumesikitishwa na uamuzi wa Laurent, kitu ambacho ni kinyume na sheria zetu.

"Tunatumaini tutalimaliza hili na hatutatoa tena taarifa kwa sasa."

Koscielny, ambaye alijiunga na Arsenal akitoka kwa miamba wa Ufaransa, Lorient mwaka 2010, amecheza mechi 350 kwa klabu hiyo.

Mkataba wake aliosaini mwaka 2017, unamalizika msimu wa 2019/20.

Beki huyo wa kati aliumia goti wakati wa mchezo dhidi ya Atletico Madrid Mei mwaka jana, na kumfanya ashindwe kucheza Kombe la Dunia nchini Urusi ambapo Ufaransa waliibuka kuwa mabingwa.

Arsenal itacheza mechi za kirafiki dhidi ya Colorado Rapids Julai 16 kabla ya kuwavaa Bayern Munich, Fiorentina na Real Madrid kwenye mashindano ya kimataifa.

Arsenal itaanza kampeni ya kuwania taji la Ligi Kuu England kwa kucheza na Newcastle United Agosti 11 mwaka huu.



# *Luiz akaribia kusajiliwa Villa*

**LONDON,** England

ASTON Villa inakaribia kukamilisha mchakato wa kumsajili kiungo wa kati wa Manchester City, Douglas Luiz kwa dau la pauni milioni 15.

Kocha Pep Guardiola alikasirishwa na kitendo cha nahodha huyo wa Timu ya Taifa ya vijana ya Brazil ya umri chini ya miaka 23 akikataliwa kupata kibali cha kazi baada ya kuonekana akiwa "anakula raha" katika ukumbi wa starehe unaomilikiwa na dada yake.

Luiz sasa yuko katika hatua za mwisho za kukamilisha uhamisho wake wa kujiunga na Villa ambayo itavaana na Minnesota United katika mchezo wa kirafiki utakaochezwa nchini Marekani wiki ijayo.

Villa inaamini kuwa itafanikiwa kupata kibali cha kazi cha mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 21 na gazeti la Sportsmail linafahamu kwamba City na klabu hiyo zitamalizana.

Mabingwa hao wa Ligi Kuu England wanarudia kufanya walichofanya msimu uliopita kwa kumuuza Angelino kwa klabu ya PSV Eindhoven.

Luiz aliichezea kwa mkopo wa misimu miwili Girona akitokea Vasco da Gama, akichangia ushindi wa ugenini dhidi ya Real Madrid Februari mwaka huu.

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI ULAYA




# ALVES AMFUATA GUARDIOLA CITY

●●● Ni baada ya kumaliza mkataba wake na mabingwa wa Ufaransa, PSG...

**MANCHESTER,** England

KOCHA Pep Guardiola anajiandaa kumsajili nyota wa zamani wa Barcelona, Dani Alves kwa ajili ya kutua kwenye kikosi chake cha Manchester City katika kipindi hichi cha majira ya joto, gazeti la Daily Mail limeandika.

Guardiola alimsajili Alves akitokea Sevilla mwaka 2008, kwa muda wa misimu minne na kushinda mataji 14 wakiwa pamoja hapo Camp Nou, yakiwamo mawili ya Ligi ya Mabingwa Ulaya na matatu ya Ligi Kuu Hispania maarufu La Liga.

**Beki wa kulia huyo mkongwe kwa sasa ni mchezaji huru, baada ya kumaliza mkataba wake wa miaka miwili na Paris Saint-Germain.**

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 36, alicheza mechi 36 katika msimu uliopita, zikiwamo mechi sita za kikosi cha Timu ya Taifa ya Brazil katika mashindano ya Copa Amerika ambayo yalifanyika kwenye ardhi ya nyumbani kwao.

Gazeti la The Mail limeandika kuwa Guardiola anajiandaa kuungana na Alves, endapo beki mwenzake Mbrazil, Danilo, ataondoka katika klabu hiyo katika majira haya ya joto. Danilo ambaye ana umri wa miaka 27, anahusishwa na mipango ya kujiunga na Inter Milan pamoja na Juventus, klabu ambazo pia Alves aliwahi kuzitumikia miaka ya nyuma.

Awali Alves alitarajia kujiunga na City mwaka 2017, kabla ya kujiunga na PSG. Hata hivyo, alisema katika mahojiano baada ya mwaka mmoja: "Siwezi kuficha namna nilivyokuwa natamani kuwa na Pep na ninatarajia kucheza Ligi Kuu England siku za usoni."

Wakati huo huo Manchester United inakaribia kukamilisha mchakato wa kumsajili, Bruno Fernandes baada ya Sporting Lisbon kukaribia kupata mrithi wa nyota huyo.

Kiungo mchezeshaji wa Timu ya Taifa ya Ureno mwenye umri wa miaka 24, ndiye mchezaji anayewindwa zaidi na klabu mbalimbali katika kutaka kuimarisha vikosi vyao kwenye idara hiyo.

Fernandes, ambaye thamani yake ni pauni milioni 70, alifunga mabao 32 na kutengeneza nafasi 18 za magoli katika mashindano yote aliyocheza msimu uliopita na kuisaidia nchi yake kushinda taji la Mataifa ya Ulaya.

United inatajwa kukutana na maofisa wa Sporting katika kukamilisha mchakato wa usajili wa mchezaji huyo huku taarifa kutoka katika mitandao ya Italia zikionyesha kwamba tayari klabu hiyo ya Ureno imeshapata mrithi wake.

City pia inahusishwa kuwa kwenye mchakato wa kumwania Fernandes.

## ZISIKUPITE

### GRIEZMANN KITAELEWEKA

BARCELONA inakaribia kukamilisha mchakato wa kumsajili mshambuliaji wa Timu ya Taifa ya Ufaransa, Antoine Griezmann (28) kutoka Atletico Madrid baada ya kujiandaa kutoa kaisi cha dau la pauni milioni 107 ambalo limetajwa katika mkataba wake. ***(Mirror)***

### BALE AMTEGA ZIDANE

MSHAMBULIAJI wa Timu ya Taifa ya Wales, Gareth Bale (29), anaendelea kufanya mazoezi na wachezaji wenzake wa Real Madrid ambao wameweka kambi yao Canada, huku akionyesha juhudi za kumlazimisha kocha Zinedine Zidane amjumuishe kwenye mipango yake. ***(Mail)***

### BRUCE KUMRITHI BENITEZ

NEWCASTLE United inajiandaa kumtangaza Kocha wa Sheffield Wednesday, Steve Bruce kuwa mwalimu wake mpya na inaamini ataungana na kikosi cha timu hiyo kilichoweka kambi yake nchini China. ***(Telegraph)***

### SHEFFIELD KUIKAMUA NEWCASTLE

KLABU la Newcastle United inafanya mazungumzo kuhusu kiasi cha fedha inachotakiwa kuilipa Sheffield Wednesday kwa ajili ya kuvunja mkataba wa Steve Bruce. Kiasi kilichotajwa ni pauni milioni 5. ***(Times - subscription required)***

### LONGSTAFF SOKONI

NEWCASTLE United imeiambia Manchester United kuwa inatakiwa kutoa kiasi cha pauni milioni 50 ili kumsajili kiungo raia wa England, Sean Longstaff, wakati klabu hiyo ya Old Trafford imesema kuwa nyota huyo mwenye umri wa miaka 21 thamani yake ni kati ya pauni milioni 18 na 20. ***(Telegraph)***

### UNITED, CITY ZAVUTANA

MANCHESTER United na Manchester City zimeendelea kujiimarisha katika mchakato wa kuwania saini ya Bruno Fernandes (24), wakati Sporting Lisbon inakaribia kukamilisha mchakato wa kujaza nafasi ya kiungo huyo wa Timu ya Taifa Ureno. ***(Alfredo Pedulla - in Italian)***

### LUKAKU AKARIBIA ROMA

MANCHESTER United imeanza mazungumzo na Roma kwa ajili ya kumuuza mshambuliaji wa Timu ya Taifa ya Ubelgiji, Romelu Lukaku, ambaye ana umri wa miaka 26. ***(Goal.com)***

### MILAN, UNITED KUTETA

MKURUGENZI wa Michezo wa Inter Milan, Piero Ausilio, amekwenda jijini London kukutana na mabosi wa Manchester United kwa ajili ya kufanya mazungumzo ya kumsajili straika wa timu hiyo, Romelu Lukaku. Thamani ya Mbelgiji huyo ni pauni milioni 75.***(Guardian)***

### TOBY ATAKIWA ROMA

WAKALA wa beki wa Tottenham, Toby Alderweireld, anaendelea na mazungumzo na Roma kwa ajili ya kumsajili beki huyo Mbelgiji mwenye umri wa miaka 30 ambaye thamani yake imetajwa kuwa ni pauni milioni 22.5. ***(Calciomercato)***

### WEST YAMWANIA ZAPATA

WEST Ham inajipanga kumsajili straika wa Sampdoria na Colombia, Duvan Zapata (28), baada ya kumkosa mshambuliaji wa Uruguay, Maxi Gomez (22), ambaye anatarajia kujiunga na Valencia akitokea Celta Vigo. ***(Sun)***

## Fainali za Mjini Unguja J'tano

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

FAINALI ya Ligi Daraja la Tatu Wilaya ya Mjini Unguja imepangwa kufanyika Jumatano kwenye Uwanja wa Amaani Visiwani hapa, imeelezwa.

Mechi hiyo inatarajia kuwa kati ya Makadara City dhidi ya mshindi wa mechi ya hatua ya nusu fainali kati ya Baja FC dhidi ya Pooling Land ambayo itachezwa leo.

Akizungumza na gazeti hili jana, Katibu Mkuu wa Chama Cha Soka Wilaya ya Mjini (UDFA), Yahya Juma Ali, alisema kuwa mashindano ya mwaka huu yalikuwa na ushindani kuanzia hatua ya kwanza na hakuna timu iliyokuwa ikisindikiza wengine.

Ali alisema kuwa wanaamini bingwa atakayepatikana atakuwa mwakilishi bora wa wilaya hiyo ambaye atapanda daraja.

"Hatua ya Sita Bora ya wilaya inaelekea ukingoni, tunatarajia mchezo wa fainali kwa ajili ya kupata bingwa utachezwa Julai 17," alisema Ali.

Aliongeza kuwa hadi sasa hakuna mdhamini yoyote aliyejitokeza, hivyo chama hicho kitatoa zawadi ambayo itakuwa imepatikana kwa ajili ya kuwaongezea hamasa wachezaji.

## Judo wajipanga kufanya makubwa

**Na Shufaa Lyimo**

KOCHA Mkuu wa Timu ya Judo, Omary Mgowe, ameahidi kikosi chake kitafanya vema katika Michezo ya Afrika ambayo itachezwa kuanzia Agosti 17 hadi 20 mwaka huu nchini Morocco.

Mgowe pia aliishuruku serikali kwa kufanikisha timu yao kusafiri kuelekea katika michezo hiyo ya kimataifa baada ya kufanya maandalizi kwa muda mrefu.

"Tunaendelea kuishukuru serikali kwa uamuzi wa kutusaidia, kupata nafasi ya kushiriki mashindano haya makubwa ni jambo la kujivunia, bila serikali tusingeweza kufanya kitu chochote. Tunapenda kuihakikishia kuwa, tutarudi na ushindi," alisema Omari.

Kocha huyo aliongeza kuwa,muitikio wa mchezo huo unazidi kukua kwa kasi kutokana na ushirikiano wanaopata kutoka kwa mashabiki na wadau mbalimbali wa mchezo huo.

"Hamasa iliyopo sasa ni kubwa kwa sababu mashabiki wetu wanatupa ushirikiano ambao unazidi kuwapa moyo wachezaji wetu, tunazidi kuimarika na kuona tuna deni la kuwapa matokeo mazuri," aliongeza.

# WACHEZA GOFU MALAWI, KENYA KUCHUANA NCHINI

**Na Faustine Feliciane**

WACHEZAJI wa gofu wa Klabu ya Lugalo wanatarajia kuchuana katika mashindano ya Kombe la Mwenyekiti " 'CBA Chairman Trophy" ambayo yamepangwa kufanyika Julai 20 mwaka huu hapa jijini Dar es Salaam, imefahamika.

Mwenyekiti wa klabu hiyo, Brigedia Jenerali Mstaafu, Michael Luwongo, alisema jana jijini kuwa mbali na kushirikisha wachezaji ambao ni wanachama hai wa klabu hiyo, pia wamewaalika wenzao kutoka katika Jeshi la Malawi.

Kiongozi huyo alisema kuwa wamekuwa na ushirikiano na wachezaji wa gofu wa Jeshi la Malawi na katika kudumisha uhusiano wao, mwaka huu wamewaalika kuja nchini kushindana.

**"Tunawashukuru sana CBA kwa kuungana na sisi kufanikisha mashindano haya, tuliwahi kualikwa na Malawi kwenye mashindano haya mwaka 2016, na sisi katika mashindano haya ya mwaka huu tumewaalika wenzetu, watakuja maofisa wakubwa na tupo tayari kuwapokea," alisema mwenyekiti huyo.**

Hata hivyo, Brigedia Jenerali Mstaafu, Luwongo, alisema kuwa wanachama ambao si hai kutoka katika klabu hiyo hawataruhusiwa kushiriki, lakini wakiwaalika wengine kutoka klabu nyingine.

Naye Meneja Masoko wa benki wa CBA, Solomon Frank, alisema kuwa wameamua kudhamini michuano hiyo ili kuunga mkono juhudi kukuza na kuendeleza mchezo huo zinazofanywa na klabu hiyo.

"Sisi kama wadhamini, tumealika wachezaji kutoka Kenya kuja kushiriki mashindano haya ya siku moja ambao yatatumia mashimo 18, tutaleta nyota wanaofanya vizuri kule Kenya," Frank alisema.



Rais wa Lipuli FC, Jesca Msambatavangu (katikati), akimkabidhi nakala ya mkataba mpya, mshambuliaji wa timu hiyo, Paul Nonga (kulia), mkoani Iringa jana. **PICHA: FRIDAY SIMBAYA**

# *Lipuli FC wavunja 'ukuta' wa Mbao*

**Na Friday Simbaya,** Iringa

KATIKA kuhakikisha kikosi chao kinaendelea kuwa na ushindani katika msimu ujao, uongozi wa Lipuli FC ya mkoani Iringa imekamilisha mchakato wa kumsajili beki wa kati wa Mbao FC, David Mwassa, imeelezwa.

Akizungumza na gazeti hili jana, Rais wa Lipuli FC, Dkt. Jesca Msambatavangu, alisema kuwa Mwassa amesaini mkataba wa mwaka mmoja na wanaamini ujio wake utaimarisha safu ya ulinzi ya klabu hiyo.

Msambatavangu alisema pia klabu yake inapenda kutangaza kwamba imempa mkataba mpya wa mwaka mmoja mshambuliaji, Paul Nonga, ambaye msimu uliopita aliisaidia timu hiyo kumaliza katika nafasi ya sita kwenye msimamo wa Ligi Kuu Tanzania Bara.

"Tunapenda kuweka wazi kuwa, tumemsajili David Mwassa Majinge na Nonga, ambaye msimu uliopita alifanikiwa kutufungia magoli saba," alisema Msambatavangu.

Rais wa klabu hiyo maarufu kwa jina la 'WANAPALUHENGO' alisema kuwa kikosi chao kitaanza mazoezi ya msimu mpya, muda mfupi baada ya kukamilisha mchakato wa usajili wachezaji ambao wamejipanga kunasa nyota wenye viwango vya juu.

Msimu uliyopita Lipuli FC ikiwa chini ya Kocha Selemani Matola ambaye kwa sasa amejiunga na Polisi Tanzania pia ilifanikiwa kufika hatua ya fainali ya mashindano ya Kombe la FA, ambapo ilifungwa na Azam FC na "kuzima" ndoto za kushiriki michuano ya kimataifa inayoandaliwa na Shirikisho la Soka Afrika (CAF).

# Michezo

Jumamosi Julai 13, 2019

Nipashe




Alves am[illegible]ata Guardiola City UKURASA 30



Mshambuliaji wa Azam FC, Obrey Chirwa (kushoto), akijiandaa kumtoka mchezaji wa Bandari ya Kenya katika mechi ya Kundi B ya mashindano ya Kombe la Kagame iliyochezwa jana nchini Rwanda. Timu hizo zilitoka suluhu. **PICHA: MTANDAO**

# Yanga haitaki mchezo Afrika

## ●●● Yatangaza kuileta AS Vita katika tamasha lake la 'Siku ya Mwananchi"...

**Na Faustine Feliciane**

TIMU ya AS Vita kutoka Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC) inatarajia kuja nchini kuivaa Yanga katika mechi ya kirafiki itakayochezwa Agosti 4 mwaka huu kwenye Uwanja wa Taifa jijini Dar es Salaam.

**Siku hiyo ndiyo itakuwa kilele cha tamasha la klabu hiyo lililopewa jina la " Tamasha la Wananchi" ambalo litatanguliwa na shughuli mbalimbali za kijamii kuanzia Julai 28 mwaka huu.**

Akizungumza na gazeti hili jijini, Makamu Mwenyekiti wa Yanga, Frederick Mwakalebela, alisema kuwa uamuzi wa kuileta AS Vita umetokana na kiwango cha juu cha timu hiyo ambayo mara ya mwisho kuja nchini ilifungwa na mabingwa wa Ligi Kuu Bara, Simba mabao 2-1 katika mechi ya Ligi ya Mabingwa Afrika.

Mwakalebela alisema kuwa anaamini mchezo huo utakuwa ni kipimo kizuri kwao katika kujiandaa na msimu mpya wa Ligi Kuu Tanzania Bara inayotarajiwa kufanyika kuanzia Agosti 27 mwaka huu, pamoja na mashindano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika ambayo watashiriki.

"Hiki kitakuwa kipimo kizuri kwetu, hawa waliwapa kipigo kitakatifu watani zetu (Simba) walipocheza nyumbani kwao, hivyo tunaamini watatupa mazoezi mazuri kuelekea msimu mpya," alisema Mwakalebela.

Alisema kuwa baadhi ya kazi za kijamii watakazofanya ni kutoa misaada mbalimbali katika vituo vya watoto yatima na maandalizi yanaelekea vizuri.

Wakati huo huo, Yanga imeiteua Kampuni ya GSM kuwa msambazaji mkuu wa jezi na vifaa mbalimbali vya michezo vya klabu hiyo ambayo ina makao makuu yake Mtaa wa Twiga na Jangwani.

"Katika kampuni tatu zilizoomba zabuni, GSM ndio wameshinda, hivi karibuni tutaingia mkataba nao rasmi, muda wa mkataba ambao tutasaini, tutawajulisha siku hiyo ikifika," alisema Mwakalebela.

Alisema pia kikosi chao kinaendelea vema na mazoezi katika kambi yao iliyoko mkoani Morogoro ikiwa na wachezaji wote iliyowasajili.

Yanga inayofundishwa na Kocha Mkuu, Mwinyi Zahera itaanza msimu mpya wa 2019/20 kwa kuvaana na Ruvu Shooting kwenye Uwanja wa Taifa na itashiriki mashindano ya kimataifa baada ya Tanzania kupata nafasi ya kuwakilishwa na timu nne kufuatia Simba kufika hatua ya robo fainali ya msimu uliomalizika wa Ligi ya Mabingwa Afrika.

## Azam FC ngoma nzito Kagame

**Na Mwandishi Wetu**

MABINGWA watetezi, Azam FC, wamejiweka katika nafasi finyu ya kusonga mbele katika mashindano ya Kombe la Kagame baada ya kulazimishwa sare ya bila kufungana na Bandari FC ya Kenya kwenye mchezo wake wa mwisho wa Kundi B uliochezwa jana kwenye Uwanja wa Huye nchini Rwanda.

Kwa matokeo hayo, Azam FC ilifikisha pointi nne sawa na KCCA ambayo jana usiku ilikuwa inaikabili Mukura Victory katika mchezo mwingine wa kundi hilo.

Endapo Mukura Victory yenye pointi moja, itaibuka na ushindi katika mchezo wake huo, itafikisha pointi nne na hivyo itaangaliwa timu yenye uwiano mzuri wa mabao ya kufunga na kufungwa.

Azam FC ni bingwa mara mbili mfululizo wa mashindano hayo yanayoandaliwa na kusimamiwa na Baraza la Soka la Afrika Mashariki na Kati (Cecafa).

## Simba kushusha majembe zaidi

**Na Mwandishi Wetu**

UONGOZI wa mabingwa wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Simba, umesema kuwa bado haujamaliza mchakato wa usajili wa wachezaji wake itakaowatumia kwa ajili ya msimu ujao.

Ofisa Mtendaji Mkuu wa Simba, Crescentius Magori, aliliambia gazeti hili jana kuwa mchakato wa usajili utaendelea kufanywa mpaka pale mipango yao itakapokuwa imetimia kwa kufuata mapendekezo ya benchi la ufundi.

Magori alisema kuwa bado wanaendelea kupambana kuwania saini za wachezaji mahiri ili malengo na ndoto zao za kutwaa taji la Afrika yaweze kutimia.

"Bado hatujamaliza usajili, tuko sokoni kuwania saini za nyota waliong'ara, tulisema tutaingia sokoni kupambana na hili ndilo jambo tunalifanya," alisema Magori.

Kiongozi huyo alisema kuwa tayari kikosi chao kimeshaingia kambini na kinaendelea na maandalizi ya safari ya kuelekea Afrika Kusini, lakini wakianza na kuwafanyia vipimo vya afya na kuwapa semina elekezi kabla ya kuanza kwa msimu mpya.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >